# Sauti ya Kweli Kimataifa

(The Voice of Truth International)

Toleo la 94

Mchapaji (Publisher):

**World Evangelism Team**

Nakala ya Kiswahili (Swahili copy):

**Swahili Gospel Team**

Mawasiliano:

+255 (0) 764 792 979

+255 (0) 784 880 470

+255 (0) 765 098 981

Taarifa (Notice):

Kitabu hiki hakiuzwi, kinatolewa bure na kanisa la Kristo kupitia taasisi ya ***World Evangelism Team (WET).***

This book is not for sale, it is freely given by the church of Christ throuth the institution ***World Evangelism Team (WET).***

# SAUTI YA KWELI KIMATAIFA

## WAFANYA KAZI:

| | | |
|---|---|---|
| Mhariri | : | Louis Rushmore |
| Mhariri Mshirika | : | Jerry Bates |
| Mhariri Mstaaf | : | Byron Nichols |
| Mhariri Mwanzilishi | : | J.C. Choate |
| Meneja wa Ofisi | : | Paula Bates |

## WAANDISHI

| | |
|---|---|
| George Akpabli | Gordon Hogan |
| Felix O. Aniamalu | Wayne Jackson |
| Rex Banks | Ancil Jenkins |
| Wayne Barrier | Jeff Jenkins |
| Paula Bates | John Kachelman, Jr. |
| Roy Beasley | Dayton Keesee |
| Mike Benson | David R. Kenney |
| Ron Bryant | Dalton Key |
| Charles Burch | Michael L. King |
| Kyle Butt | J. Randal Matheny |
| Frank Chesser | Cecil May, Jr. |
| Betty B. Choate | Wes McAdams |
| Glenn Colley | Colin McKee |
| Lance Cordle | Stan Mitchell |
| Sunny David | Kevin L. Moore |
| Hans Dederscheck | Owen D. Olbricht |
| David Deffenbaugh | David Pharr |
| Clarence DeLoach, Jr. | Neal Pollard |
| Bill Dillon | Mark Posey |
| Bobby G. Dockery | Steve Reeves |
| Hershel Dyer | Andy Robison |
| Earl Edwards | Martha Rushmore |
| Demar Elam | Rebecca Rushmore |
| Raymond Elliott | David A. Sargent |
| Reuben Emperado | Darrell Surrette |
| David Everson | David Tarbet |
| Royce Frederick | J.J. Turner |
| E. Claude Gardner | Ken Tyler |
| Gary C. Hampton | Allen Webster |
| Jack Harriman | R.H. Tex Williams |
| Parker Henderson | Nathan Wright |

# Roho ya Ufahamu

Louis Rushmore



“Upofu wa muundo wa kiume” ni msemo niliousikia mahali mwanawake fulani akinung’unika kuhusu wanaume labda hata mke wangu, kunihusu mimi. Usemi huo hutokea, kwa mfano, kama sikupata kitu katika jokofu, ingawa nilichokuwa nakitafuta kilikuwa sehemu ya wazi kabisa. (Nadhani hata hivyo, kama kuna kitu kama hicho kwamba “upofu wa muundo wa kiume” pia wakati mwingine upo “upofu wa muundo wa kike”). Mtu mwingine anaweza kutamka kitu kingine ambacho hakionekani wala kugundulika kwa mfano, “kama ingekuwa ni nyoka angeweza kukuuma” sisi sote, nadhani, kwa sehemu hatujali kile kinachopaswa kuwa dhahiri kwetu. Mara nyingi, ingawa “upofu” wetu ni pale tunapojaribu kutambua kitu kisicho muhimu na kinachohusiana mambo ya kila siku katika maisha.

Hata hivyo, ni jambo zito kushindwa kwa mwanadamu pindi tunapoonekana kuwa vipofu katika mambo ya kiroho, ambayo yanahusika na uzima wa milele. Inashitua pale wana wa Mungu wanapoonekana kujishughulisha kidogo kwa ajili ya roho zao, na kuwa na furaha na kutokuwa na shauku ya usalama wa roho zao na watu wengine. Kipaumbele cha kutafuta roho ni cha kwanza kuliko mahitaji

ya kimwili, vilielezwa kwa uwazi na Bwana wetu Yesu Kristo***. Msisumbuke***, ***basi, mkisema tule nini? Au tunywe nini ? Au tuvae nini? Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anayajua ya kuwa mnayahitaji hayo yote Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake na hayo yote mtazidishiwa. Basi msusumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwa siku maovu yake." (***Mathayo 6:31-33). Hata hivyo, wana wa Mungu wana historia ndefu ya kuwa vipofu wa mambo ya kiroho. ***Na neno la nabii Isaya lina timia kwao, likisema mtasikia, wala hamtaelewa. Kutazama mtatazama, wala hamtaona. Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, Na kwa masikio yao hawasikii vema, Na macho yao wameyafumba; wasije wakaona kwa macho yao, Wakasikia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao, Wakaongoka nikawaponya,***" ( Mathayo 13:14-15; Isaya 6:9-10).

Je, kuna ajabu yo yote kwamba Bwana wetu alipowaambia wanafunzi wake watazame mbali zaidi kuliko katika ulimwengu walimokuwa wakiishi? Yesu Kristo aliwapa wafuasi wake changamoto ya kuwa na **roho ya ufahamu** Aliposema***. "Hamsemi ninyi, Bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama mimi nawaambieni, Inueni macho yenu myatazame mashamba, ya kuwa yamekwisha kuwa meupe tayari kwa mavuno."*** (Yohana 4:35). Yesu alikuwa hazungumzii kuhusu kulima na kuvuna mazao halisi, katika kipindi cha mwisho cha kupanda. Badala yake alitumia mfano kutoka kwenye kilimo ili kusisitiza uhitaji wa mitume wake kushiriki katika huduma yake ya "***kutafuta na kuokoa kile kilichopotea" (***Luka 19:10). Na huu ndio uthibitisho na maneno ya mwisho ya Bwana wetu kwa mitume kabla ya kupaa kwake***."…Enendeni, ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka"*** (Marko 16:15).

**Kwa Mkristo mmoja mmoja anahitaji kuwa na roho ya ufahamu.** Lazima tutambue kwamba miili yetu ni magari tu ambayo ni nguzo ya

roho zetu. Roho iliyo ndani ya mtu inafananishwa na mtu aliye ndani ya gari akiliendesha. Gari si mtu, lakini mtu yupo ndani ya gari, na anayeendesha ni tofauti. Hatimaye msafiri ataliacha gari na mwishowe roho itaicha mwili. (Yakobo 2:26) Isipokuwa kama ujio wa pili ukitokea katika maisha ya mtu (1 Wathesalonike 4:15).

Ni lazima kwanza tujitambue wenyewe na kimsingi kama roho wakati huohuo upande wa pili tukitambua kwamba miili ni ile nyumba inayohifadhi roho zetu. Wakristo wanahitaji kutazama watu wa familia zao, marafiki, majirani, wafanyakazi wenzao, wanafunzi wenzao na watu wote kwa ujumla kwa namna tofauti na tunavyowatazama. Kusudi la kuwatazama kutoka nje-ndani ni kuwatazama kama roho kabla ya kutazama miili yao ilivyo, (kwa mfano, nyuso, maumbile, jinsia na kabila). Kila mtu roho yake ni muhimu na ya thamani, kila roho ni ya thamani sana kuliko utajiri wote uliopo duniani (Mathayo 16:26). Wakristo lazima wawe na roho yenye ufahamu.

## Je, unaona nini pindi unapowatazama watu unaokutana nao?

**Makanisa ya Kristo yanahitaji kuwa na roho ya ufahamu.** Kila kusanyiko na mjumuiko wa makusanyiko ambayo yanayounda undugu, au kanisa la ulimwengu linahitaji kuutazama ubinadamu katika misingi ya roho zao. Kanisa lenye ufahamu litajitazama lenyewe kwanza kama kusanyiko la roho na kwa upande wa pili kujifikiria kama kusanyiko la miili (watu). Badala ya kufikiria juu ya jinsia, kizazi na kabila, kwanza fikiri juu ya roho pamoja na wana wa Mungu. Tazama zaidi na weka mpaka kwa washirika wa kusanyiko, utazame ulimwengu ambao ni wa

kiroho mabilioni ya roho zenye thamani ambazo zipo katika miili ya nyama.

(Kwa kweli, Wakristo waaminifu wanapaswa kutambua majukumu mahususi ya kijinsia yaliyopangwa katika Maandiko kwa wanaume na wanawake. Mkazo hapa ni pekee kuangalia katika asili ya kiroho ya mwanadamu ili kukuza afya ya kiroho, tabia na kuimarisha uinjilisti ili kuwafikia wasio Wakristo na Wakristo wasio waaminifu).

Wazazi, roho za watoto wenu zimefungwa na kukaa katika miili ya muda. Ndugu, roho za watu wafamilia yako, roho zao zimefungwa katika miili. Roho zipo kila mahali tulipo na wakati wo wote tunapomuona mtu. Kila mtu katika sayari ya dunia ni roho ambayo inahitaji Injili ya Yesu Kristo na wokovu alioutoa na uzima wa milele aliouahidi. Na roho zinazomzunguka kila mmoja wetu ni shamba la kiroho lililotayari kwa mavuno.)

**Kuwa roho yenye ufahamu! Ona roho kwa kutumia miwani ya kiroho**. Wokovu wetu wenyewe na ukombozi wa roho za watu wengine unakutegemea wewe pamoja na Kanisa la Bwana kuwa na roho ya ufahamu. Je, unaona nini pindi unapowatazama watu unaokutana nao?

> **Ayubu 11:12** "Lakini mpumbavu aweza kupata ufahamu, Ingawa mwanadamu huzaliwa kama mtoto wa punda-mwitu."
>
> **Ayubu 28:20** "Basi hekima yatoka wapi? Na mahali pa ufahamu ni wapi?
>
> **Ayubu 28:28** "Kisha akamwambia mwanadamu, Tazama, kumcha Bwana ndiyo hekima, Na kujitenga na uovu ndio ufahamu."



# Ni nini Kinachotokea Katika Ubatizo?

Jerry Bates

Kuna matendo machache ya kidini ambayo yana utata zaidi kuliko ubatizo. Wakristo wengi duniani hawaamini kuwa kuna kitu cha kufanya katika wokovu wetu, wengi wanasema kuwa ni taratibutu za ishara kuonesha kile ambacho tayari kimeshatokea katika mioyo na maisha yetu yaani msamaha wa dhambi zetu. Hakuna kifungu kinachozungumzia mtazamo huu kwa uwazi zaidi kuliko kitabu cha Warumi. Warum 6:3-4 "***Basi tulizikwa Pamoja naye kwa nia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo nasisi tuenende katika upya wa uzima"***.

Tunahitaji kufahamu kuwa Warumi 6 haihusiani na ubatizo, bali inahusu dhambi. Neno "Dhambi limejitokeza mara 16 katika hii sura. Paulo alikuwa akiwasisitiza Wakristo kukumbuka kitu kilichotokea wakati walipobatizwa. Sijui kama kuna mtu ye yote mwenye swali kuhusu uhakika wa imani na dhabihu ya Yesu Kristo juu ya msamaha wetu. Na hilo swali ni, **"Ni wakati gani dhambi zetu zinaondolewa?"**

Paulo alisema hili linatokea katika ubatizo. Ubatizo ni zaidi ya taratibu au ishara. Ni zaidi ya kufanya tendo la mwili la utii. Katika Warumi 6:2, Paulo alifundisha kwamba tulikufa katika dhambi pale tulipobatizwa. Kataika Warumi 6:3 Paulo aliweka wazi kuwa tulibatizwa katika Yesu Kristo, pia tulibatizwa katika mauti yake.

Watu wengi watakubali kwamba ni damu ya Yesu inayotuosha dhambi zetu (Ufunuo 1:5), lakini kwa namna gani tunaweza kukutana na damu ya Yesu? Damu ya Yesu ilimwagika pale msalabani. Wakati Yesu alipokufa, askari alichoma mkuki ubavuni mwa Yesu, ikatoka Damu na maji (Yohana 19:34). Wakati tunapobatizwa, tulibatizwa katika mauti ya Yesu Kristo, ambapo ndipo damu inapomwagika. Hivyo, tunakuja kuunganika katika damu ya Yesu ambayo inatuosha dhambi zetu. Hakuna mtu hata mmoja atakayeweza kuokolewa bila ya kuifia dhambi. Hakuna mtu hatammoja atakayeweza kuokolewa bila ya kuunganika na damu ya Yesu Kristo.





Haya yote yanatokea katika ubatizo kulingana na mtume Paulo.

Pia Paulo alisema kwamba baada ya ubatizo, tunafufuka na kutembea katika maisha mapya ya ubatizo. Paulo aliandika ni jinsi gani ubatizo wetu ni uumbaji mpya kutoka mautini, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu. Yesu alimaliza Maisha yake ya kimwili, lakini alianza maisha mapya ya ufufuo. Na kwa mfano huo tuliifia dhambi, hivyo ukawa mwisho wa maisha ya dhambi yaliyopita na kuanza maisha safi. **Hatubadilishi vitu vichache tu wala kufuta makosa machache. Tunaanza maisha mapya.** Hii inafanya ubatizo kuwa ni mwisho wa maisha yetu ya zamani na mwanzo wa maisha yetu mapya. ***"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.*** (2 Wakoritho 5:17). Kwa hiyo, tunaanza maisha mapya yenye lengo moja na uchaji mkubwa kwa Yesu.

Zingatia alichoandika Paulo ambacho hutokea katika ubatizo, Je, ni kwa jinsi gani mtu anaweza kusema kwamba ubatizo ni desturi au ishara? Ikiwa ni ishara, basi kile unachowakilisha kwa hakika kitapita, si kwa nguvu za mwanadamu ye yote, au maji bali ni kwa nguvu za Mungu.

**Yohana 1:12-13**

"Bali wote waliompokea [Yesu] aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu."

# Huwezi Kubishana na Neno la Mungu

J.C. Choate



1932 - 2008

Watu wengi wanataka sehemu ndogo tu ya neno la Mungu ambalo ni zuri kwa imani yao, matendo, na hali zao. Hii inawapelekea wao kulikubali kwa sehemu na kukataa yaliyobaki. Wanajaribu kuelezea na kujenga hoja kwa njia mbalimbali. Huku ni kutukana na kutumia Biblia vibaya. Tunapaswa kuhitaji ukweli na ukweli wote katika aya za Maandiko. Hata hivyo, hatupaswi kuishia hapo, bali kuendelea kukubali ukweli katika aya nyingine. Tunapaswa kutaka kujua mapenzi yote ya Mungu. Tunapaswa kutii ukweli wote na kuufundisha kwa wengine. Ujinga wa makusudi, au kukataa sehemu yo yote ya neno la Mungu haitatusaidia au hata mtu mwingine. **Sehemu ndogo ya ukweli haitoshi.**

Kuna watu ambao wanafundisha kwamba, mtu anachotakiwa kufanya ili aokoke ni **kuamini tu**. Aya kama Yohana 3:16,3:36,5:24 na Matendo 16:31 zinatumika kutetea hoja hiyo. Kwa kuangalia kile

mistari mingine inafundisha, kunaweza kukawa na kupingana, kana kwamba haya ndiyo yote anayohitaji Mungu, lakini kunaweza kusiwepo kupingana kuhusu umuhimu wa kuamini au imani yenyewe. Bila shaka tunafahamu mistari hii inafundishwa ili kwamba mtu aamini. Hata hivyo, hii si mistari pekee ya Maandiko inayotarajiwa kujadiliwa wakati linapokuja swala la wokovu wa roho. Labda hao wanaotumia hii mistari kufundisha **"imani tu"** wameitenga. Labda wameshindwa kuielewa na kuweka mipaka ya maana ya imani.

Kristo alituambia kwamba lazima mtu atubu vinginevyo ahukumiwe [Luka 13:3]. Paulo anasema kwamba Mungu aliamuru watu wote wa kila mahali watubu (Matendo 17:30). Kuna aya nyingine ambazo zinafundisha na kusisitiza uhitaji wa kutubu. Mtu anaweza kuhitimisha kwamba jambo la muhimu sana la mtu kufanya ili aokoke ni kutubu dhambi zake. Na wakati huo huo mtu anaweza kupinga kwamba kuna jambo la kufanya zaidi ya hilo. Bila kujali, kuna hoja moja ambayo kwa hiyo kunawezekana kusiwe na ubishi na hilo ni kwamba Mungu anamtaka mtenda dhambi atubu dhambi zake.

Kuna aya kadhaa ambazo zinasisitiza umuhimu wa **ubatizo** (Matendo 22:16; Warumi 6:3). Je, hii ina maana kwamba **"ubatizo pekee "** unaokoa? Je, **imani** si muhimu? Vipi kuhusu **kutubu**? Lakini haya maswali yanaweza kuletwa na kujadiliwa, lakini panaweza kusiwe na shaka kuhusu ulazima wa ubatizo, kama mtu atakubali ukweli wote wa mapenzi ya Mungu.

Petro aliwaambia watu katika siku ile ya Pentekoste kwamba wanapaswa **kutubu** na **kubatizwa** kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao (Matendo 2:38). Ingawa hakuna cho chote alichosema kuhusu **imani**, swali lililoulizwa kuhusu wokovu linaonesha wazi kwamba tayari **walishaamini**. Pamoja na hayo, bila kujali ni mambo gani yaliyoachwa, imeelezwa nini? ***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu,.."*** kunaweza kusiwepo na majadiliano katika hoja hii. **Tunaloweza kufanya ni kukubali**.

Kama tukijishughulisha katika mpango wa wokovu au somo lingine tunapojifunza Biblia tunapaswa kuwa na nia ya kwamba

tutakubali ukweli wote katika kila aya na kwa hivyo tutakubali kila amri katika kila agizo.

Ni wazi kuwa Bwana hajatoa ukweli wote katika mstari mmoja au hata katika aya kadhaa. Hata hivyo, hakutoa amri zote za Injili katika mstari mmoja. Hatuwezi kuishia katika mstari mmoja au mistari miwili katika somo lo lote, lakini lazima tuendelee kusoma na kujifunza maneno yote ya Mungu na kuyaunganisha. Lazima tuukubali ukweli wote uliotolewa katika mstari ndipo tuenendelee na mstari mwingine. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa na uwezo wa kufahamu yote Bwana anayohitaji kwetu. Ni kwa kuamini tu na kutii ukweli wote tunaweza kuokolewa. Kunaweza kusiwe na ubishi katika hili.

Hakika, hatupaswi kuwa kwenye hali ambayo italazimisha mabishano juu ya neno la Mungu. Hata hivyo, hatupaswi kuwa katika nafasi ambayo itatufanya tukatae ukweli wo wote ili tuweze kudumu na imani ambayo tayari tulishaikubali. Kama tukifanya hivyo, tutapoteza wakati na mwishowe, **kukataa sehemu ya Neno la Mungu kutasababisha roho zetu kupotea milele.** Ni huzuni kiasi gani kulipa gharama kwa ajili ya kiburi, ukaidi, au hata tabia nyingine yo yote inayoweza kusababisha kupoteza ufahamu wetu kwamba hatutaki kukubali ukweli!

Ni muhimu tukumbuke maneno ya Bwana***, "Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho. Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema. Nami najua ya kuwa agizo lake ni uzima wa milele; basi hayo ninenayo mimi, kama Baba alivyoniambia, ndivyo ninenavyo."*** (Yohana 12:48-50).

Hata Bwana wetu hakuwa na ujasiri wa kubadilisha ujumbe wa Mungu. Hakika hakuna mwanadamu atakayeweza kujaribu kufanya jambo kama hilo.

**j.C. Choate, sasa ni hayati, alitumia maisha yake katika kazi ya umisheni huko Asia, kwa njia ya redio, Luninga na majarida. Jarida: Sauti ya Kweli Kimataifa ilikuwa ni ndoto yake.**

## YALIYOMO

### Mungu

Mungu Alifinyanga Tundu ndani Yetu ........ Claude Thompson ...........17
Mungu Anaposema “Hapana” .............................. Jim Poland ..........19
Hatari, Upendo na Dhabihu ...........................Charles R. Rose ............21

### USHAHIDI

Siku Sita za Uumbaji zilukuwa ni Siku zenye masaa 24? ....Kevin L. Moore ....................................................................................................24
Kwa nini Ninamwamini Mungu ............. Michael Hooper ...................25

### NENO LA MUNGU

Kitabu cha Watu ..........................Dan R. Owen ..................................28
Kutafakari ...................................Dwight Fuqua ................................30
Kanisa la Kristo.......................... Wes McAdams ................................32

### WOKOVU

Ikiwa Napaswa Kufa kabla ya Kuamka ......... Steve Higginbotham ......38
Ubatizo wa tamaa? .......................... E. Claude Gardner ......................40
Mbinguni: Yote Yaliyobaki.................... Charles Box ...........................42

### KANISA

Lazima Mtu Awe Ndani ya Kanisa ili Aokolewe....Sunny David ...........45
Kanisa la Mungu katika Utamaduni Ulioharibika......Greg Tidwell ……..48
Ukristo – Matembezi ya Furaha pamoja na Mungu!......Thomas R. Dohling ...........................................................................................50
Mambo Magumu ambayo Hayapo katika Kanisa la Kristo…Moris S. Chiuyo…54

### FUNDISHO LA KUISHI KWALO

Maswali 4.................Doug Greenway & David A. Sargent ..................55
Nipeleke Mlangoni Bwana..................Patrick Morrison …..................57
Maisha Mapya Utakapobatizwa................Owen D. Olbricht ….............59

**UKRISTO KATIKA MATENDO**

Kuhubiri katika tamaduni za Leo................Andy Robison ....................62
Acha Nuru Yako Iangaze katika Jamii ........Martha Lynn Rushmore.....65
Sikia na Mtii Bwana Yesu.....................Tim Childs ..............................67
Mmeuzunguka Mlima Huu Kiasi Chakutosha..........Jeff Archey ...........68

**IBADA**

Burudani na Ibada ya Kweli ................. Basil Overton .........................70
Je! Upo Tayari Kwenda Mbali Kiasi Gani ili Kuabudu?..................Mark T. Tonkery ..........................................................................................73
Je, Ni Sahihi Kupiga Makofi Katika Ibada?..........T. Pierce Brown ........75

**MAISHA YA KILA SIKU YA MKRISTO**

hamasa......................................... Arlis Richardson............................82
Mambo Ya Kila Siku....................... Derek Broome ..............................84
Alexanda Mwenye Hasira............... Bill Dillon ...................................86
Fursa ya Maombi...................... Jack W. Carter ..................................87

**NYUMBA YA KIKRISTO**

Sifa za Nyumba Nzuri...................... Jimmy Clark ...............................88
Jinsi Ya Kuboresha Hali Ya Familia Yako Kiroho...........Ken Tyler .........90
Neno Kwa Wake................... Dalton Key ..........................................91

**UCHUNGUZI WA KIFUNGU**

Sifa Sita Za Uongozi Bora.................... Neal Pollard ............................92

**WAHUSIKA KATIKA BIBLIA**

Watu Waliosahaulika Katika Biblia: Yethro......Rebecca Rushmore.....95
Sabau Za Kuwa Na Furaha Katika Majaribu........ Gary C. Hampton......99
Mkristo Ni Nani? ....................Maxie B. Boren ................................102

**MASWALI KATIKA BIBLIA**

Je, Mkristo Mwaminifu Ataokoka Kwa Shida?...Dennis Gulledge ......104
Kwanini Wengi Hujifunza Bila Kuufikia Ukweli?.....Ardron Hinton......105

## CHATI NA MUHTASARI

Kuhudhuria Kwa Uaminifu !.............. Mark N. Posey ......................106

## HISTORIA YA KANISA

Harakati Za Urejeshaji Ni Kitu Gani?.........Jimmy R. Canup ..............107
Jihoji Mwenyewe kama Upo katika Imani Ndani ya Kanisa.......Ernest S. Underwood ..........................................................................110
Njiani Kuelekea Derbe .................... Betty Burton Choate .................112

## MAKALA, MASHAIRI NA VIJAZI

Roho ya ufahamu......................Louis Rushmore ................................03
Nini Kinatokea Katika Ubatizo?...................Jerry Bates ......................07
Huwezi Kubishana Na Neno La Mungu .................J.C. Choate ...........10
Dakika 5 za Kujifunza Biblia........................Paula Bates ......................16
Mlango Uliofunguliwa Kwa Ajili Yangu........ Cliff Holmes ....................27
Sarafu Za Kenny ......................David R. Kenney .......................101,109
Tafuta Aya ......................................Jerry Bates ................................36
Ungeweza Kutaka Nini Zaidi?................J. Randal Matheny ................39
Maoni Ya Haraka katika Aya Muhimu.... Betty Burton Choate ............61
Ucheshi ........................................Jerry Bates ..................................79
Unapimaje? ...................... Betty Burton Choate ...............................81
Je , Wajua? ...........................Rebecca Rushmore ............................111
Msaka Tonge.............................Rebecca Rushmore .........................94
Dondoo za Shadrack S. Msambaza…………………………………20,49,98,101

# Dakika 5 za Kujifunza Biblia



**Paula Bates**

## Watakatifu na Ndugu



1. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; kwa __________zote na ________mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea _______wote; Efe 6:17-18
2. Kwa mahitaji ya _____,mkifuata _____; katika kukaribisha ____ mkijitahidi. Warumi 12:13
3. Hapa ndipo penye _________ ya watakatifu, hao wazishikao amri za ________, na imani ya ___________. Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa Naam, asema __________, wapate _____________ baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao **Ufunuo 14:12-14**.
4. Wasalimuni _______ walioko ________, na Nimfa, na _________ lililo katika nyumba yake **Wakolosai 4:15**.
5. Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni _________ kuwaita ____________ zake; **Waebrania 2:11**.
6. Sisi tunajua ya kuwa tumepita toka mauti kuingia uzima, kwa maana ___________, ____________. ___________ asiyependa, akaa katika mauti. **1Yohana 3:14**

**Majibu**

Sala, maombi, watakatifu

Ukarimu,wageni

Subira, Mungu ,Yesu Roho,pumzika

Ndugu, Loudokia,Kanisa

Haya,ndugu

Twaawapenda, ndugu Yeye




Blaise Pascal alikuwa mwana mahesabu na mwanasayansi maarufu sana wa miaka ya 1600. Yeye ndiye aliyeendeleza kanuni za ***Hydraulics***, na ambaye sheria zake za msingi zimetajwa. Pascal ndiye wa kwanza kurasimisha nadharia ya uwezekano, na pia alitengeneza mashine za hesabu za kwanza. Alijulikana kama mtu mwenye kipaji kipindi cha uhai wake na hata leo.

Hata hivyo, imani ya kiroho ilikuwa ni ya muhimu zaidi kwa Pascal, akawa mtawa, ambapo aliandika vitabu vingi vya kidini kikiwemo *"An apology for the Chriatian Religion"* ('Apology' ni neno la Kilatini la "utetezi") – hoja juu ya utetezi wa Ukristo. Alifundisha kwamba maarifa yote hupatikana kupitia ufunuao wa Mungu – uumbaji wake wa asili na maneno yake yaliyoandikwa. Pascal alijadili kuwa imani ya kiroho lazima ilingane na Neno la Mungu kuliko akili za kibinadamu, au sababu za kisayansi au mantiki ya hisabati. Aliandika kuwa, "kuna tundu ndani ya kila mmoja wetu ambalo Mungu alililifinyanga, na tunateseka kwa kuwa tunajaribu kulijaza kwa vitu vingine kuliko Mungu." Kweli hili ni hitaji la muhimu zaidi kati ya mahitaji ya muhimu ya mwanadamu – kumtafuta Mungu na kumfanya tena kuwa sehemu yetu (Zaburi 16:9-11; Waefeso 2:12).

Leo wanaume na wanawake wamekata tamaa ya kutafuta kitu ambacho kinajaza pengo kubwa katika maisha yao, na wanajaribu kila

kitu kinachokuja, kutoka kwenye madawa na kuridhika na ngono kwa kufanya kazi ngumu na raha ambayo pesa inaweza kununua. Pia baadhi wanajaribu mambo ya siri ya zama mpya au taratibu za kisheria katika dini. Hata hivyo, kama Pascal anavyotukumbusha, utupu wetu ulifinyangwa na Mungu kwa kuwa Yeye Mwenyewe Ametuumba na tamaa ya asili na pia hata haja ya kumtafuta Yeye (Matendo 17:24-27). Ni Mungu wetu ndiye tunayemkosa – Muumbaji wetu – Mungu tunayemtaka na Mlinzi wetu –Mungu tunayemuhitaji.

Mtunga Zaburi alitambua dhana hii kitambo na kumwomba Mungu kumfunulia na kumfundisha "njia" zake, "mapito" yake na "ukweli" wake (Zaburi 25:4-5). Mungu anadhihirisha, njia na mapito yake kwa mwanadamu kupitia ukweli wake, na ukweli huo ni maneno yake yaliyoandikwa, yaliyodhihirishwa, Maandiko au Biblia (Yohana 17:17; Luka 16:29-31; Waebrania 1:1-2). "Ukweli" wa Mungu tu utaweza kujaza uwazi wetu, tundu lililofinyangwa na Mungu na kutuweka huru na dhambi, hatia yake na huzuni (Yohana 8:31-32; Wagalatia 5:1).

Tumempata Mungu na kutimiza mahitaji yetu ya kibinadamu kwa kusikia tu (Warumi 10:13-14), kuamini (Matendo 16:30-33), kutii (1 Samweli 15:22-23; Warumi 6:16-17) kwa, ufunuo wake ulioandikwa. Mungu hufanya kazi kupitia Neno lake kwa wale walio miongoni mwetu wanaoamini (1 Thesalonike 2:13). Kadiri tunavyojijaza neno lake tunajijaza na Mungu mwenyewe, Roho wake Mtakatifu na Mwanawe Yesu Kristo (Yohana 16:12-13; Waefeso 5:18-19; Wakolosai 3:16). Ni uhusiano wetu wa kiroho wa kudumu na Mungu ambao hutupa amani ya kweli (Yohana 14:27; Warumi 5:1-5) kuliko vitu vya kimwili vya dunia hii. Wote, Pascal na mtunga Zaburi (Zaburi 23) walitambua kwamba kamwe hatutaweza kuridhika na vitu mbadala. Mungu na neno lake pekee linatosheleza kuziba tundu la kiroho lililopo ndani yetu na kutufanya wakamilifu wa kweli.

**Claude Thomson anaishi huko Dallas, Texas, Marekani.**

# MUNGU ANAPOSEMA “HAPANA”

Jim Poland



“Hapana” ni neno linaloonekana kuwa la ghafla na la mwisho kabisa. Ni neno ambalo wengi wetu hatupendi kulisikia pale tunapoomba kitu tunachokihitaji. Pia inakuwa ni mbaya zaidi pale ambapo jibu “hapana” linapotoka kwa Mungu wakati anapojibu sala zetu.

Wakati mwingine Mungu husema “hapana”. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa Yeye ni Mungu asiyejali wala asiyependa. Ameonesha upendo wake mkuu kwetu kwa njia yenye kuhuzunisha

sana! ***"Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi"*** (Warumi 5:6-8).

Mungu amesema "Hapana" kwa baadhi ya watumishi wake wakuu. Mungu alisema "Hapana" kwa mtume Paulo, mtu aliyeacha kila kitu na kuhubiri Injili ya upendo wa Mungu unaookoa na neema ulimwenguni. Paulo alipomuomba Bwana kuondoa tatizo la afya ya mwili, Mungu alimwambia, ***"Neema yangu yatosha, maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu….."*** (2 Wakorintho 12:7-10).

Mungu Baba, pia alisema "Hapana" kwa Mwanawe, Yesu. Yesu alipokuwa akikabili kifo kwa ajili ya dhambi zetu, aliomba mara tatu, ***"Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe"*** (Mathayo 26:36-46). Kama tunavyojua, jibu lilikuwa wazi, "Hapana." Yesu alikinywea kikombe kile cha mateso kwa ajili ya dhambi zetu.

Mungu anaposema "Hapana," anayo sababu, na sababu zake ni za juu kuliko za mwanandamu. ***"Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu."*** (Isaya 55:8-9).

**Jim Poland ni mhubiri wa kanisa la Kristo huko Carthaga, Missouri, Marekani.**

Kutoka 23:29-30 ***"Sitawafukuza mbele yako katika mwaka mmoja; nchi isiwe ukiwa, na wanyama wa bara wakaongezeka kukusumbua. Nitawafukuza kidogo kidogo mbele yako, hata utakapoongezeka wewe, na kuirithi hiyo nchi."*** Kuna wakati Mungu huondoa matatizo yetu kidogo kidogo kwa faida yetu wenyewe.

**(Shadrack S. Msambaza).**

## MUNGU

# Hatari, Upendo na Dhabihu

Charles R. Rose

Ilikuwa ni mwanzo wa wakati, kwa kweli, ilikuwa ni kabla ya wakati kama tujuavyo na kupima kwake kulianza. Baba na Mwanawe walikuwa wakiweka mipango ya kuweka msingi kwa ajili ya tukio kuu kutokea katika historia ya ulimwengu kabla ya kuzaliwa kwa Mtoto Yesu. Tukio hilo linaoneshwa katika mstari wa kwanza wa kitabu cha kwanza cha Biblia Takatifu, ***"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi"*** (Mwanzo 1:1).

Kujua kwamba katika mipango Yao kulikuwa na uumbaji wa mwanadamu kwa mfano Wao (Mwanzo 1:26), akiwa na uwezo wa kuchagua jema na baya (Mwanzo 3:522), uamuzi ulifanywa kwa Mwana kufanyika mwili kurudisha utu uliopotea kwa Baba, mwanadamu anaweza kuchagua njia za uovu. ***"Naye amejulikana kwetu tangu zamani kabla haijawekwa misingi ya dunia, lakini alifunuliwa mwisho wa zamani kwa ajili yetu"*** (1 Petro 1:20).

### HATARI

Alipokuja katika mwili, ilihitajika kuwa Yesu apitie kila hatua ya maisha ya mwanadamu, ikiwepo kuzaliwa (Mathayo 1:18-23; Luka 2:1-7); Akikua katika kila hatua ya maisha (ikiwa ni kiakili, kimwili, kiroho na kijamii) (Luka 2:52); na kujifunza kuwa mtiifu (Waebrania 5:9). Zingatia kuwa haukuwa ukweli uliosahaulika kuwa moja kwa moja angeweza kutii kila kitu alichoamriwa na Baba. Kama ilivyo kwa wanadamu wote, alijifunza hili.

Tunapotafakari maisha na kifo cha Mwana pekee wa Mungu, tunapaswa kutambua hatari ya kushangaza aliyoichukua alipokuwa ***"…yuna namna ya Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu"*** (Wafilipi 2:6-7).

Alizijua nguvu za Shetani na majaribu yake “kabla ya misingi ya ulimwengu” uamuzi huu ulifanywa. Alipokuwa mbinguni, alikuwa Mwana wa Mungu akiwa na uwenyeji wote wa mbinguni ukimsaidia katika makao yake. Duniani, lazima “azipinge hila za Shetani” (Waefeso 6:11) kwa namna hiyo hiyo lazima “watu” wote wazipinge.

Vipi kama alijitoa mara moja tu kwenye majaribu ya Shetani? Matokeo yangeweza kuwa ya kukatisha tamaa kabisa. Mwanadamu, kuanzia Adamu hadi kizazi cha leo na kuendelea kingetupwa Jehanamui kwa Shetani milele kwa sababu dhabihu Yake ndio pekee ambayo inaweza kutoa aina yo yote ya tumaini. Kama ingekuwa na dawaa kwa dhambi moja tu kila mwanandamu aliyefikia umri wa kujua jema na baya (angalia Kumbukumbu la Torati 1:39; Isaya 7:16), akiwemo Mwana pekee wa Mungu, Yesu wa Nazareti, asingekuwa na tumaini. Hivyo tunaweza kuona ukubwa wa hatari wa kuacha Mbingu na kuja ulimwenguni.

## UPENDO

Tukizitambua hatari zilizochukuliwa na Mwana wa Mungu, kutanisababisha mimi kushukuru zaidi sana juu ya upendo uliooneshwa kwa mwanandamu. Kama baba wa watoto watatu, nitakueleza bila shaka, sitaruhusu hata sehemu kidogo tu kwa mmoja wa watoto wangu kufanya kitu cho chote kitakacho hatarisha roho zao za milele. Hata hivyo, hiki hasa ndicho Baba yetu wa mbinguni alikuwa tayari kufanya kwa kuwa alitupenda sana. Upendo wake kwa mwanadamu ambaye alimuumba kwa mfano wake na kumpa pumzi ya uhai (Mwanzo 2:7), ilikuwa ni vizuri kuwa ***“…akamtoa Mwana wake wa pekee ili kila amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele”*** (Yohana 3:16)

Ni maumivu kiasi gani ya roho anayopata kwa kizazi kilichopotea! Ni huruma kiasi gani aliyonayo kwa wale ambao hawafanyi cho chote kujiokoa wenyewe (Yeremia 10:23)! Ni upendo wa ajabu ulioje – si tu kwa Baba, na kwa Mwana pia! ***“Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni , ili tupate uzima kwa Yeye. Hili ndilo pendo, si kwamba***

***sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba Yeye alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu”*** (1 Yohana 4:9-10). ***“Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu…..”*** (1 Yohana 4:17).

Ndio, kwa ujasiri, kwa kujiamini bila hofu wala shaka, tunaweza kusimama mbele zake katika hukumu kwa kuwa tumezishika amri zake (1 Yohana 3:21-24).

**DHABIHU**

Tunao ujasiri huu, kwa kuwa tunajua upendo wake na kuelewa umuhimu wa dhabihu yake. ***“Kwa hiyo ajapo ulimwenguni, asema dhabihu na toleo hukutaka, lakini mwili uliniwekea tayari. Ndipo niliposema, tazama nimekuja (katika gombo la chuo nimeandikiwa) nifanye mapenzi yako, Mungu”*** (Waebrania 10:5,7). ***“Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu, tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake. Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa”*** (Waebrania 10:12-14).

***“Basi ndugu kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, njia ile aliyotuanzia iliyo mpya, iliyo hai, ipitayo katika pazia, yaani mwili wake, na kuwa na kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu; na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi. Na mlishike sana ungamo la tumaini lenu, lisigeuke; maana yeye aliyeahidi ni mwaminifu; tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri. Wala tusiache kukusanyika pamoja kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia”.*** (Waebrania 10:19-25).

Alichukua hatari, akaudhihirisha upendo na Alitoa dhabihu. ***“Basi ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu si bure katika Bwana”*** (1 Wakorintho 15:58).

USHAHIDI

# Je, Siku Sita za Uumbaji Zilikuwa ni Nyakati za Kijiolojia au Masaa 24 Halisi katika Siku?

Kevin L. Moore

Nadharia ya mafundisho fulani hudai kwamba kila siku za uumbaji katika Mwanzo 1 huwakilisha zama za kijiolojia (mamilioni ya miaka) badala ya masaa 24 ya kawaida ya siku. Hapa kuna sababu sita rahisi za kukataa dhana hii kwa msaada wa Maandiko.

1. Wakati wo wote neno la Kiebrania *yom* ("siku") likitanguliwa na namba, mara zote linarejelea jua (masaa 24) siku (Mwanzo 1:5, 8, 13, 19, 23, 31; Hesabu 13:25; 14:33-34; Kutoka 20:9-11).
2. Kirai, "Ikawa jioni ikawa asubuhi siku ya kwanza" (Mwanzo 1:5), kimetumika zaidi ya mara 100 katika Agano la Kale na mara zote linarejelea siku yenye masaa 24.
3. Ikiwa "siku" katika kifungu hiki inarejelea zama za kijiolojia, basi kila siku ingekuwa ni mamilioni ya miaka ya kuendelea kuwa na giza ikifuatiwa na mamilioni ya miaka ya kuendelea kuwa na mwanga.
4. Adamu aliishi katika siku ya sita na ya saba (Mwanzo 1:26-2:3), lakini hakuishi zama za kijiolojia. (Mwanzo 5:5)
5. Wayahudi waliamriwa kufanya kazi siku sita na kupumzika siku moja katika kila wiki kwa sababu hicho kilikuwa kielelezo cha uumbaji kilichoandikwa katika kitabu cha Mwanzo habari za Mwanzo (Kutoka 20:8-11).
6. Kama Mungu angetaka kuelezea uumbaji katika siku 6 halisi zenye masaa 24, je angewezaje kuelezea kwa usahihi zaidi?

**Kevin Moore anahudumu kama Mkurugenzi wa Misheni ya mafunzo katika chuo Kikuu cha Freed-Hardeman huko Henderson, Tennessee, Marekani.**

# Kwa nini Ninamwamini Mungu

Michael Hooper

**Namwamini Mungu kwa sababu ya uwepo wake na matokeo yake.** Matokeo hayawezi kuwepo bila kuwa na sababu nyuma yake. Ipo dunia ya viumbe hai. Hayo ndiyo matokeo. Si sababu za falsafa ili mtu ahitimishe kwamba matokeo yanatokana na vitu visivyo hai vya asili. Matokeo ya uhai yanahusisha asili ya uhai. Kumwamini Mungu aliye hai ni kama asili ya ulimwengu wa vitu vilivyo hai na kwa hiyo falsafa ni ya kweli. ***"Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru"*** {Warumi 1:20}

**Namwamini Mungu kwa sababu ya uwepo wa ubunifu.** Asili ilibuniwa kwa akili. Samaki alibuniwa kuogelea ndani ya maji. Ndege alibuniwa kuruka angani. Daima mbunifu huonekana palipo na ubunifu. Kwa kuwa hii dunia ambapo tunaishi imebuniwa, basi kuna mbunifu aliyeibuni. Kwa hiyo, hii ndiyo sababu ya kumwamini Mungu aliye hai kama Mbunifu wa ubunifu huu uitwao Dunia. Pia haikubaliki kuhitimisha kuwa mbunifu hayupo wakati ubunifu unaonekana dhahiri kabisa.

**Namwamini Mungu kwa sababu ya uwepo wa "wema"** na "**ubaya."** Hebu tufikiri kwa muda kwamba hakuna Mungu, lakini kivipi, ingeamuliwaje kuwa jambo fulani ni sahihi au si sahihi? Nini sahihi au si sahihi ingekuwa ni zao la fikrai za kibinadamu. Jamii mbalimbali zingekuwa na vipimo vyao vya wema na ubaya. Jamii ya Nazi iliyoongozwa na Adolph Hitler walifikiri kuwa ni sahihi kuwaangamiza mamilioni ya Wayahudi.

Bila ya kuwa na kipimo kutoka katika chanzo cha juu kuliko akili ya mwanadamu au jamii kitakachoamua kati ya sahihi na kisicho sahihi,

jamii ya Nazi isingekuwa na hatia ya ukosaji. Tungebaki kudhani tu kuwa walikosea, lakini tusingeweza kuthibitisha hilo. Ingekuwa ni mashidano tu kati ya maneno yao dhidi ya maneno yetu bila ya kuwa na kipimo cha ukweli.

Tumefanywa kuwa viumbe tunaowajibika kwa chanzo cha juu kuliko jamii za kibinadamu. Sisi, kwa hiyo, tunawajibika kwa chanzo hicho. Hivyo tukio hilo lote ni uthibitisho wa uwepo wa Mungu aliye hai aliyetuumba, na tunawajibika kwake kwa chaguzi tunazofanya. Pia ni uthibitisho kwamba Mungu alifunua ufahamu wa mwanadamu [kwa Neno lake au Kweli] kile kilicho sahihi. Katika msingi huo, mabaya yote yanaweza kujulikana. Kwa sababu hiyo, Imani ya uwepo wa Mungu ni, jambo la busara.

**Namwamini Mungu kwasababu akili ipo**. Akili yangu isingeweza kuwa ni zao la kitu kilichokufa, mwamba au gesi, vyote hivi ni tupu havina akili yo yote. Vilevile akili yangu isingewezekana kutokea pasipo kitu. Daima hakuna huzaa hakuna. Daima kitu huzaa kitu. Ikiwa kulikuwa na wakati ambapo hapakuwa na akili, basi kusingekuwepo na akili kabisa. Hiyo inaonesha kwamba inayoitwa akili imekuwepo milele. Kwa hiyo, ni busara kuamini katika umilele na Mwenyeakili aitwaye “Mungu.”

**Namwamini Mungu kwa sababu ya Yesu**. Hakuna mwana historia atakaye kataa kwamba Yesu aliishi. Taarifa za Maisha ya Yesu na huduma yake zilikuja kwetu kupitia mashuhuda wake waliokuwa tayari kutoa maisha yao kwaajili ya ushuda wao kuhusu Yeye. Hivyo ni ngumu kupuuza uaminifu wao na ujumbe wao. Kutokana na maelezo yao, Yesu alithibitisha madai yake kuwa yeye ni Mwana wa Mungu kwa kupitia miujiza aliyoifanya. Hivyo bila shaka inathibitisha kwamba Mungu yupo.

**Michael Hooper ni mhubiri wa Injili na mwinjilisti wa runinga wa kanisa la Kristo. Anaishi na mfanyakazi wa Yesu Kristo huko Guyana, Marekani ya Kusini.**

# Mlango Ulipofunguliwa Kwa Ajili Yangu



Cliff Holmes

*Wakati wa Kwenda unapokuwa ni ngumu,*
*Na njia yangu ni ya taabu,*
*Kuna mlango uliofunguliwa kwa ajili yangu.*

*Wakati milima inapokuwa na mwinuko mkali,*
*Na katikati ya bonde na giza nene,*
*Kuna mlango uliofunguliwa kwa ajili yangu.*

*Wakati roho zinapokuwa zimepotea,*
*Kwa sababu hawahesabu gharama,*
*Kuna mlango uliofunguliwa kwa ajili yangu.*

*Wakati ninapokuwa huru mbali na dhambi zote,*
*Na nina jitihada za kuingia ndani,*
*Kuna mlango uliofunguliwa kwa ajili yangu.*

*Wakati safari yangu itakapofika mwisho,*
*Nitamwona Yesu rafiki yangu,*

# Kitabu cha Watu

Dan R. Owen

Tangu kipindi cha Musa, Mungu alizungumza na watu wake kwa uthabiti kwa ufunuo wa Maandiko. Na akatupa Neno lake takatifu, akitegemea tulifuate kwa ukamilifu. Kuwa watu wa Mungu, maana yake ni kuwa watu wa kitabu.

Katika mwaka 622 K.K watu wa Yuda walikuwa watu wa kitabu. Baadae wakaiga utamaduni wa wenyeji. Walikuwa wameharibika katika kufikiri na katika kutenda kwao. Walikuwa wapagani ambao walitenda machache na kuchunguzaa ukweli wa dini.Kitabu cha Mungu kilisahaulika kwa muda mrefu.

Siku moja, Kuhani ndani ya hekalu ilitokea akakipata kitabu cha Sheria. Ugunduzi wa kundi hili ni katika mzunguko na mlolongo wa matukio na majanga ambayo yalijirudia ni upande wa hasi wa taifa lote kwa muda. **Je, umewahi kupata Kitabu cha Mungu katika nyumba yako?**

*"**Naye Hilkia, kuhani mkuu, akamwambia Shafani, mwandishi, Nimekiona kitabu cha torati katika nyumba ya Bwana. Hilkia akampa Shafani kile kitabu, naye akakisoma. Shafani mwandishi akamwendea mfalme, akamletea mfalme habari tena, akasema, Watumishi wako wamezitoa zile fedha zilizoonekana ndani ya nyumba, nao wamewakabidhi wafanya kazi wanaoisimamia nyumba ya Bwana. Kisha Shafani mwandishi akamwambia mfalme, akasema, Hilkia kuhani amenipa kitabu. Shafani akakisoma mbele ya mfalme. Ikawa, mfalme alipokwisha kuyasikia maneno ya kitabu hicho cha torati, alirarua nguo zake.**"* (2 Wafalme 22:8-11).

Baada ya ugunduzi, baadhi ya watu wa Yuda walikisoma Kitabu cha Sheria. Walikielewa, wakatiwa hatiani na wakagundua jinsi kilivyo chamuhimu. Inaonekana kuwa ni ujinga kupendekeza kwamba tukisome Kitabu. Hata kwa kukisoma tu tunaweza kufahamu umuhimu wake na kuwa na njia ya kuishi kwa kadiri ilivyowekwa wazi kwetu.

Mfalme wa Yuda alirarua vazi lake wakati aliposoma kitabu cha sheria. Hakukisoma katika haliya kawaida wala kukichukilia katika hali ya kitaaluma. Alimsikia Mungu akizungumza naye pamoja na watu wake katika maneno ya Kitabu. Aligundua kuwa yeye na watu wake walikuwa katika hali ya uvunjifu wa amri za Kitabu. Akararua mavazi yake kwa majuto makubwa. Je kusoma Kitabu kumewahi kukufanya urarue mavazi yako? Je, uko tayari kukabiliana nacho na kukiweka moyoni?

Hatimaye mfalme Yosia na jamaa yote ya viongozi walitii kitabu. Walifanya kitu kulingana na kile walichokisoma. Waliangamiza upagani katikaardhi yao, wakarejeza matendo ya kibiblia na kwa ujumla kutafuta kutenda kile Kitabu cha Mungu kilichowaongoza kutenda, kwa sababu walijua kilikuwa ni Neno la Mungu.

Katika Agano hili la kale ni ukweli mwepesi kusu kile Mungu anachotutaka tufanye. Tafuta Kitabu cha Sheria ya Mungu. Soma Kitabu. Rarua mavazi yako (ni lugha ya kiroho). Fanya kile Kitabu kinachokwambia ufanye. Kwa hakika, **Mungu atatubaliki ikiwa tutaiga unyenyekevu wa Yosia.**

**Dan R. Owen anafanya kazi na kusanyiko la Broadway huko Paducah, Kentucky, Marekani.**

Yoshua 1:8 **"Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana."**




Dwight Fuqua

Paulo alimwelekeza Timotheo,*”Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha”.* (1 Timoth 4:13). Mistari miwili baadae Paulo alionya, ***“Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote.”*** ( Mstari 15) Tunapo tafakari mapenzi ya Mungu na kujitoa kabisa kwa ajili ya hayo tunakua kiroho na kuwa watumishi wazuri wa Mungu.

Je, unatafakari? Kwa sababu za kiimani za kidini, kutafakari kumekuwa katika wakati mgumu. Kutafakari maana yake ni “waza au fikiri ni kuakisi juu ya kile unachokitafakari.” Neno la Kiyunani katika kifungu hiki ni {*Meletao*} ikiwa na maana “kujali,” au “kufikiri” au “kuwaza.” ***“Mwe na hofu wala msitende dhambi, Tafakarini vitandani mwenu na kutulia.”*** (Zaburi 4:4). Hii ni changamoto kweli katika dunia yetu ya sasa.

Daudi alikuwa mtu anayempendeza Mungu .**Kwanza:**, Alidumu katika kutafakri juu ya kazi ya Mungu. ***“Bwana wetu ni mkuu na mwingi wa nguvu, Akili zake hazina mpaka.”*** (Zaburi 143:5). **Pili:** Alidhamiria kutafakari ***“Nitayakumbuka matendo ya Bwana; Naam,***

***nitayakumbuka maajabu yako ya kale. Pia nitaitafakari kazi yako yote; Nitaziwaza habari za matendo yako***." ( Zaburi 77:11-12.). **Tatu**: Daudi aligundua kuwa kutafakari ni hisia chanya za kuomba. ***"Kutafakari kwangu na kuwe kutamu kwake; Mimi nitamfurahia Bwana"*** (Zaburi 104:34). **Nne**: Alitafakari kwa sababu alipenda sheria ya Mungu. ***"Sheria yako naipenda mno ajabu, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa."*** (Zaburi 119:17). **Tano**: Akifikiri kuhusu Mungu kuwa wa thamani kwake. ***"Mungu, fikira zako zina thamani nyingi kwangu; Jinsi ilivyo kubwa jumla yake!"*** (Zaburi 139:17). Si ajabu Daudi kuwa mtu aliyependwa na Mungu!

Tunapaswa kutafakari katika Neno la Mungu, Daudi aliwaandikia watu wenye haki. ***"Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku."*** (Zaburi 1:2). Wale ambao waliweza kuongoza watu wa Mungu hasa katika uhitaji wa kutafakari. Mungu alimwelekeza Yoshua, ***"Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, bali yatafakari maneno yake mchana na usiku, upate kuangalia kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo; maana ndipo utakapoifanikisha njia yako, kisha ndipo utakapositawi sana."*** (Yoshua 1:8).

Tunapaswa kutafakri Neno la Mungu kwa sababu ni furaha kwetu (Zaburi 1:2 ), kwa sababu tunataka kulishika Neno la Mungu na kuwa na mafanikio (Yoshua 1:8), kwa sababu linaleta ufahamu, (Zab 49:3), kwa sababu linatufanya tuwe na furaha (Zaburi 104:34), kwa sababu linatuweka mbali na dhambi (Zab 119: 11), kwa sababu tunalipenda Neno lake (Zaburi 119:97), kwa sababu kufikiri kuhusu Mungu kuna thamani (Zaburi139:17) na, kwa sababu linaleta maendeleo ya kiroho (1Timotheo 4:15). ***"Maneno ya kinywa changu, Na mawazo ya moyo wangu, Yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, Mwamba wangu, na mwokozi wangu."*** (Zaburi 19:14).

**Dwight Fuqua ni mhubiri wa kusanyiko la Findlay huko Sparta, Tennessee, Marekani.**

# Kanisa la Kristo

Wes McAdams

Wakati mwingine tumekuwa tukizungumza kuhusu kuwa katika kanisa la Agano Jipya au tunazungumza kuhusu kuwa kama Kanisa la karne ya kwanza. Bila shaka hatumaanishi tunataka kurudia dhambi za kanisa la Korintho au kukubali Injili ya uongo kama baadhi ya makanisa ya Galatia yalivyofanya. Makanisa ya karne ya kwanza hayakuwa makamilifu.

Tunaposema tunataka tuwe kama Kanisa la karne ya kwanza, tunasema zaidi ya miaka 2000 iliyopita, Upagani, Ukatoliki, Umadhehebu na mengine yasiyohesabika yenye ushawishi yamewasababisha elimu ya Kikristo na matendo kuibuka na kuwa kitu fulani ambacho si sawa na matendo ya Ukristo wa karne ya kwanza. Tunaposema tunataka kuwa kama Wakristo wa Karne ya kwanza, tunasema tunataka kurudi katika Agano Jipya ili kujua kile ambacho Wakristo walipaswa kufanya na kuamini.

Hata hivyo, Kanisa la Agano Jipya halikuwa na Agano Jipya tayari, lakini bado, Kanisa la Korintho, Kwa mfano, walikuwa na barua walizoandikiwa na Paulo, na uenda hata walikuwa na barua kadhaa, ambazo walizinakili na kupeana. Lakini inawezekana hawakupata vitabu vyote 27 vya Agano Jipya katika kipindi cha karne ya kwanza.

Kwa hiyo, kama mamlaka yetu yanatoka katika Agano Jipya, je, mamlaka yao yalitoka wapi? Ni kwa namna gani walifahamu nini wanapaswa kufanya?

### Mitume na Manabii

Tangu mwanzo wa kila Kanisa, Wakristo walielewa kuwa walihitaji kufahamu mapenzi ya Yesu, lazima wajitoe wenyewe katika mafundisho ya mitume (Matendo 2:42). Mitume walikuwa wawakilishi

rasmi wa Yesu. Walikuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu katika kweli yote (Yohana 16:13). Roho Mtakatifu alikuwa akiwakumbusha yote ambayo Yesu aliwafundisha (Yohana 14:26) Walikuwa na ufahamu wa Yesu Kristo (1 Korintho 2:16). Tunaposema tunataka kuwa kama Kanisa la Agano jipya la karne ya kwanza, tunamaana tunataka tujitoe katika mafundisho ya mitume.

Paulo alisema katika (Waefeso 4:11-12) ***"Naye [Yesu] alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe;"*** Nyongeza kwa mitume, ambao walikuwa wamebeba miujiza kwa njia ya Roho Mtakatifu, pia walikuwepo manabii wengine ambao Bwana alizungumza nao. Bado mtume Paulo alilionya kanisa la Korintho kwamba hivi vipawa vya miujiza vitapita. Aliandika ***"Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika."*** (1 Wakorintho 13:8). Naamini hivi vipawa vilipita wakati ambapo mapenzi yote ya Mungu yalipofunuliwa kupitia mitume na waliandika yote katika vitabu 27 vya Agano Jipya. Pamoja na hayo, wakati hivi vipawa vipo, kanisa la la karne ya kwanza walikuwa na uwezo wa kusikia ujumbe wa kinabii kutoka kwa Bwana.

## Wainjilisti, Wachungaji na Walimu

Haikuwa ni mitume na manabii tu ambao walifundisha kanisa la karne ya kwanza lipi la kufanya na nini cha kuamini. Mitume waliwafundisha wainjilisti, watu kama Timotheo na Tito. Waliwatumia hawa wainjilisti kwenye makusanyiko kufundisha kile walichofundishwa na mitume.

Hawa watu ***"walikaripia, walikemea, na kuonya"*** (2 Timotheo 4:2). Walichagua wazee kwenye kila kusanyiko (Tito 1:5), na walikuwa wakipeleka kile walichokuwa wamekisikia kwa mitume na

***"uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."*** (2 Timotheo 2:2).

Wainjilisti wa leo waliojitoa kujifunza mafundisho ya mitume na kuwafundisha wengine, wanafuata nyayo za wainjilisti wa karne ya kwanza. Hatuna tena mitume, lakini tuna mafundisho yao katika kurasa za Agano Jipya na bado tunahitaji wainjilisti ambao watafundisha ujumbe wa mitume, ujumbe wa Yesu Kristo.

Hivyo, Kanisa la karne ya kwanza lilikuwa na wainjilisti ambao walifundisha mafundisho ya mitume pamoja na kuchagua watu waliokomaa kiroho kutumika kama wachungaji, na walimu katika kila kusanyiko. Wachunga hawa ji walipewa kulisimamia kusanyiko pamoja na kuwajibika kwa roho zao kuwa salama. Wakristo katika Kanisa la karne ya kwanza walikuwa wakisikiliza wachungaji. Mwandishi wa Waebrania aliandika ***"Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu, ili kwamba wafanye hivyo kwa furaha wala si kwa kuugua; maana isingewafaa ninyi.***" (Waebrania13:17).

Wainjilisti na wachungaji bado wanashikilia nafasi katika kanisa, lakini hususani walicheza katika nafasi muhimu katika kipindi ambacho Agano jipya likiwa katika matengenezo. Kwa sababu tu tuna nakala ya Agano Jipya haitupi haki ya kupuuzia uchaguzi na mamlaka ya Mungu kuhusu muundo wa Kanisa.

## Maandiko ya Agano la Kale

Hatuwezi kusahau kuwa kanisa la karne ya kwanza lilikuwa halijakamilika bila Maandiko. Bado walikuwa na Maandiko ya Agano la Kale. Walikuwa wakisoma Maandiko ya Agano la Kale katika mikusanyiko yao ya wazi (1 Timothe 4:13). Walikuwa wakihubiri na kufundisha kutoka humo. Walikuwa wakifundisha ni namna gani Yesu alivyokuwa Kuhani wao Mkuu, Jinsi gani Alikuwa dhabihu ya upatanisho kwa ajili ya dhambi zao, Jinsi gani kanisa lilikuwa Israeli

mpya, na ni namna gani wanapaswa kutafakari Imani ya Nuhu, Ibrahimu, Musa, Danieli na wengine (Waebrania 11).

Ilikuwa ni kuhusu haya Maandiko mtume Paulo aliyoandika, ***"Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini."*** (Warumi15:4).

## Maandiko ya Agano Jipya

Hatimaye, pia kanisa lilikuwa na Maandiko ya Agano Jipya. Inawezekana hawakuwa na Agano Jipya lote, lakini unapozingatia kila kitu walichokuwa nacho katika mamlaka yao, kitabu kimoja au viwili ingekuwa ni baraka Kubwa. Nafikiria Kanisa kama Kanisa la Efeso walipokea waraka wa Paulo, sit u kwamba waliunakili na kuutuma kwa makanisa mengine, lakini pia kanisa waliusoma waraka tena na tena, wakihifadhi kwa upendo mkubwa kila neno.

Mtume Petro aliandika kuwatia moyo Wakristo kusikiliza nyaraka za mtume Paulo. Aliandika, ***"Nanyi uhesabuni uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu, kama vile na ndugu yetu mpenzi Paulo alivyowaandikia kwa hekima aliyopewa; vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe."*** (2Petro 3:15-16).

Tumebarikiwa sana kwa kuwa na vitabu vyote 27 vya Agano Jipya leo. Kama tunataka kuwa katika kanisa ambalo ni mali ya Yesu, lazima tufanye kile walichokifanya baada ya Pentekoste, tujitoe katika mafundisho ya mitume.

**Wes McAdams ni mhubiri wa kusanyiko la Baker Heights huko Abilene, Texas, Marekani.**




1. Je, Paulo alimwona Yesu yeye binafsi? Wakati gani? (mstari wa 1)
2. Ni nini kilikuwa mhuri wa utume wa Paulo? (mstari wa 2).
3. Kulingana na Paulo, ni nani alikuwa na haki ya kuwa na mke na kuondoka nae anaposafiri? (mstari wa 5).
4. Ni mfano gani ambao Paulo aliutumia kuthibitisha kuwa yeye na Barnaba walikuwa na haki ya kusaidiwa na kanisa? (mstari wa 6).
5. Ni kufungu kipi kilichoandikwa na Musa ambacho Paulo alikinukuu kuthibitisha jambo lile lile lililoko katika swali la 4?
6. Yeye alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa _______naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini ____________ (mstari wa 10).
7. Ikiwa tuliwapandia ninyi vitu vya ____________je, ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya ____________ (mstari wa 11).
8. Kwa nini Paulo hakuchukua msaada kutoka kanisani?
9. Wale waliohudumia madhabahu walishiriki nini?
10. Kulingana na Paulo, Mungu alisema wale wanaoihubiri Injili wanapaswa kuishije? (mstari wa 14).
11. Kwa nini Paulo alisema hakuwa na cha kujivunia ingawa alikuwa akihubiri Injili? (mstari wa 16).
12. Paulo aliaminiwa kwa ______________ wake. (mstari wa 17).

**1** Je, mimi si huru? Mimi si mtume? Mimi sikumwona Yesu Bwana wetu?
Ninyi si kazi yangu katika Bwana? **2** Kwa maana ikiwa mimi si mtume kwa
wengine, lakini ni mtume kwenu ninyi; kwa maana ninyi ndinyi muhuri ya
utume wangu katika Bwana. **3** Hilo ndilo jawabu langu kwa wale
wanaoniuliza. **4** Je, hatuna uwezo wa kula na kunywa? **5** Hatuna uwezo
kuchukua pamoja nasi mke aliye ndugu, kama wao mitume wengine, na
ndugu wa Bwana, na Kefa? **6** Au je, ni mimi peke yangu na Barnaba tusio na
uwezo wa kutokufanya kazi? **7** Ni askari gani aendaye vitani wakati wowote
kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika
matunda yake? Au ni nani achungaye kundi asiyekunywa katika maziwa ya
kundi?

**8** Je, ninanena hayo kwa kibinadamu? Au torati nayo haisemi yayo hayo?
**9** Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa, usimfunge kinywa ng'ombe
apurapo nafaka. Je, hapo Mungu aangalia mambo ya ng'ombe? **10** Au
yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam, yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa
kuwa alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini, naye apuraye
nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake. **11** Ikiwa sisi tuliwapandia
ninyi vitu vya rohoni, je ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya mwilini? **12**
Ikiwa wengine wanashiriki uwezo huu juu yenu, sisi si zaidi? Lakini
hatukuutumia uwezo huu, bali twayavumilia mambo yoye tusije tukaizuia
Habari Njema ya Yesu. **13** Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni
hula katika vitu vya hekalu, na wale waihudumiao madhabahu huwa na fungu
lao katika vitu vya madhabahu? **14** Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba
wale waihubirio injili wapate riziki kwa hiyo injili.

**15** Lakini mimi sikutumia mambo hayo hata moja. Wala siyaandiki hayo
ili iwe hivyo kwangu mimi, maana ni heri nife kuliko mtu awaye yote
abatilishe huku kujisifu kwangu. **16** Maana ijapokuwa naihubiri Injili, sina la
kusifia; maana nimewekewa sharti; tena ole wangu nisipoihubiri Injili. **17**
Maana nikiitenda kazi hii kwa hiari yangu nina thawabu; ila ikiwa si kwa hiari
yangu, nimeaminiwa uwakili. **18** Basi thawabu yangu ni nini? Ni hii, ya kuwa
nihubiripo, nitaitoa Injili bila gharama, bila kutumia kwa utimilifu uwezo
wangu nilio nao katika Injili.

# IKIWA NAPASWA KUFA KABLA SIJAAMKA...

Steve Higginbotham

Nilipokuwa mtoto, wazazi wangu walinifundisha kusema sala hii. Je, na wazazi wako walifanya hivyo hivyo? Unajua, mara nyingi sala ya mtoto iliyokaririwa huwa hivi:

Sasa najilaza ili nilale,
Naomba Bwana uihifadhi roho yangu,
Ikiwa nitakufa kabla sijaamka,
Nakuomba Bwana uichukue roho yangu.

Uwezekano wa kufa kabla hujaamka umejaa vidokezi? Hata hivyo, wazo kuu ni, "Je, umeshafanya maandalizi ya hatima hiyo?" Umeshajiandaa kufa? Je, umilele wako ni salama? Swali zuri. Hasa wakati umetulia, ukapata wakati ufukiri na tathimini kusimama kwako mbele za Mungu. Itakuwaje ukifa kabla hujaamka? Je, yote yatakuwa ni mema? Labda, sisi sote tutakuwa tumefanya vema kujiuliza swali kama hilo, lakini swali hilo silo ninalotaka wewe ulitilie mkazo kwa sasa.

Ningependa kukuuliza kama umeshafanya maandalizi kwa ajili ya hatima ya "kuamka?" Ni jambo moja kuwa tayari "kufa katika Kristo," na "kuishi kwa ajili ya Kristo" ni jambo lingine. Ni maandalizi gani umeyafanya ikiwa hutakufa kabla hujaamka? Je, umeshapanga na kujiandaa kutumia muda, talanta na nguvu zako katika kumtumikia Mungu?

Ikiwa utaamka kabla hujafa, utaitumiaje kesho? Ni mipango gani umeiweka? Je, mipango yako inahusisha Neno la Mungu? Je, kuna mtu ye yote atakayechunguza mipango yako na kutambua kuwa wewe ni mwanafunzi wa Yesu?

Ikiwa utaamshwa kabla hujafa, na unasalimiwa kwa siku nyingine, utafanya nini kwa muda wako? Je, una mipango maalum ya kushiriki Injili? Je, una mipango maalum ya kutoa huduma katika jina la Yesu kwa muhitaji? Je, una mtazamo maalum kwa yule unayemwombea na kujaribu kumfikia? Je, umeshawahi kutoa mawazo ya namna ambavyo utatumika vema na kulitia nguvu kanisa unaloabudia?

Rafiki, sidhani kwa hakika kama mtu anaweza kujiandaa kikamilifu "kufa katika Kristo" mpaka awe amejiandaa "kuishi katika Kristo." Kiukweli ili uweze kujiandaa kufa katika Kristo ni lazima mtu awe ndani ya Kristo.

Hivyo, kurudi katika swali, "Ni nini kitakutokea ikiwa utakufa kabla hujaamka? Mbali na swali hilo, ingawa lina umuhimu, sawa, "Itakuwaje ikiwa utaamka kabla hujafa?" ikiwa utakufa kabla hujaamka, ninamwomba Bwana aichukue roho yako. Lakini kama utaamka kabla hujafa, halafu nini?

## Je, utataka nini zaidi?

**J. Randal Matheny**

- Kuwa na mvuto, shujaa, mwonekano?
- Maneno yenye nguvu na hekima za kale?
- Hisia ya utambulisho?
- Kundi la marafiki waaminifu?
- Kazi iliyo bayana?
- Hadithi ya kusisimua?
- Shughuli yenye maana?
- Motisha thabiti?
- Uwezeshaji kwa ajili ya mafanikio?

Njia ya Kristo in hayo yote
***"Kristo ni kila kitu"***
(Wakolosai 3:11).

**Steve Higginbontham mhubiri wa kanisa la Kristo Karns huko Knoxville, TN, Marekani.**

# UBATIZO WA TAMAA?

E. Claude Gardner

Mtu maarufu wa Runinga alisema kuwa fundisho ambalo ni mbadala wa ubatizo ni "ubatizo kwa tamaa." Kama mtu atashindwa kubatizwa, tena kwa sababu ya maisha na tabia njema, itakuwa ni sawa na "ubatizo wa tamaa." Hii ilikuwa ni nadharia potofu na ya kitabia mpya kwangu. Mpango huu mbovu umeunganisha mawazo tofauti tofauti ya uongo kwa kukataa amri rahisi na iliyo wazi ya Mungu.

Muheshimiwa Marshall Keeble alikuwa amezoea kusema, "Biblia iko sahihi," na huu ni ukweli kuhusu ubatizo. Hapa kuna ukweli kuhusu ubatizo.

Unatuokoa katika dhambi. ***"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumuiwa"*** (Marko 16:16).

Ni amri. ***"Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"*** (Matendo 2:38); ***"Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo"*** (Matendo 10:48).

Ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi. ***"Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake"*** (Matendo 22:16).

Unatuokoa na kutupa dhamiri safi. ***"mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu ) kwa kufufuka kwake Yesu Kristo"*** (1 Petro 3:21).

Unamwongeza mtu katika kanisa la Kristo. ***"Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa"*** (Matendo 2:47b).

Ni maziko, si kunyunyiza. ***“Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima”*** (Warumi 6:3-4).

Ni muhimu katika kuzaliwa upya. ***“Yesu akajibu, amin, amin, nakuambia, mtu asipizaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu”*** (Yohana 3:5).

Unamuwezesha mtu “kufurahi” baada ya ubatizo. ***“Kisha walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, Yule towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi”*** (Matendo 8:39).



Unamuweka mtu ndani ya Kristo, Mwokozi**.** ***“Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo”*** (Wagalatia 3:26-27).

Ni wazi, ubatizo unahitajika zaidi ya “tamaa.” Ubatizo hauwezi kukataliwa na kuwa na mbadala  kwa, sala ya toba, imani pekee, maadili mema au maagizo ya kindugu. Kwa nini unasubiri?

**E. Claude Gardner ni Raisi Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Freed-Hardman huko Henderson, Tennessee, Marekani.**

# Mbinguni: Yote Yaliyobaki

Charles Box



Mbinguni ni mahali pa upendo, furaha na amani isiyo na mwisho. ***"Huko waovu waacha kusumbua; huko nako hao waliochoka wapumzika"*** (Ayubu 3:17). Mungu yupo Mbinguni (Mathayo 5:16), na ametoa Mbingu kama mahali pa pumziko kwa wana wa Mungu (Waebrania 4:9-11). Tujifunze kutoka Mbinguni.

## YESU ALIKUJA KUTOKA MBINGUNI

***"Kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka"*** (Yohana 6:38). Wakati wa Mungu ulipotimia, Yesu alizaliwa na bikira aliyeitwa Mariamu (Wagalatia 4:4). Yesu alizibeba dhambi zetu ili mbinguni kuwe nyumbani kwetu (1 Petro 1:18-20). Alikuja duniani ili twende mbinguni.

## JINA LANGU LIMEANDIKWA MBINGUNI

***"Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya malaika elifu nyingi.***

***Mkutano mkuu wa kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika"*** (Waebrania 12:22-23). Jina lako lipo mahali pengi, labda kwenye hati ya ndoa, hati ya mali, hundi, stashahada, hati ya kusafiria, karatasi ya malipo na vitu vingine vingi. Ikiwa umemvaa Kristo katika ubatizo na kuwa mwaminifu katika kanisa lake, jina lako limeandikwa mbinguni. Yesu atarudi kutoka mbinguni kuwakusanya waaminifu wake kuwa pamoja naye milele. (1 Thesalonike 4:16-17).

## MBINGUNI NI MAKAO YA MILELE YA ROHO

***"……Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi muwepo"*** (Yohana 14:1-3). Miili yetu itakufa, lakini kuna nyumba ya milele ambayo haijatengenezwa kwa mikono inatungojea mbinguni (2 Wakorintho 4:16-5:8). Kutakuwa na mwili wa utukufu pamoja na jumba la kifahari mbinguni.

## MBINGUNI NDIO LENGO LETU NA MALIPO YETU

***"Furahini na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni;…."*** (Mathayo 5:12). Mbinguni ni faida kuu ya mwanadamu. Ili uende mbinguni, sikia (Warumi 10:17), amini (Yohana 8:24), tubu (Luka 13:3), mkiri Yesu kama Bwana na Kristo (Warumi 10:9-10), batizwa (Matendo 22:16) na baki kuwa mwaminifu (Ufunuo 2:10). Yesu anataka wale wote wanaomfuata wawe mbinguni. ***"Baba, hao ulionipa nataka wawe pamoja nami popote nilipo, wapate na kuutazama utukufu wangu ulionipa; kwa maana ulinipenda kabla ya kuwekwa msingi ulimwengu"*** (Yohana 17:24). Mbinguni ni mahali palipoandaliwa kwa kila Mkristo wa kweli.

**Charles Box ni mhubiri wa Kanisa la Kristo Walnut St, huko Greenville, Alabama, Marekani.**



# Tafuta Katika Biblia

Martha Rushmore

**NUHU NA FAMILIA YAKE**

1. Nuhu alikuwa mtu wa__________ (Mwanzo 6:9).
2. Safina ilikuwa na miangaza mingapi? (Mwanzo 6:16).
3. Nuhu aliijenga Safina kwa mbao za mti gani? (Mwanzo 6:14)
4. Watu wangapi waliingia ndani ya Safina? (Mwanzo 7:1)
5. Matokeo ya mvua yalikuwa nini? (Mwanzo 7:17)
6. Mtoto wa pili wa Nuhu aliitwa nani? (Mwanzo 6:10)
7. Ni ndege gani wa kwanza ambaye Nuhu alimtuma? (Mwanzo 8:7)
8. Nani aliufunga mlango wa Safina? (Mwanzo 7:16)
9. Nuhu alitumia nini kuifunika Safina ndani na nje? (Mwanzo 6:14)
10. Ni aina gani ya jani alilorudinalo njiwa? (Mwanzo 8:11)
11. Mtoto wa tatu wa Nuhu aliitwa nani? (Mwanzo 6:10)
12. Ni mwana gani wa Nugu ambaye alikuwa katika ukoo wa Yesu? (Luka 3:36)
13. Nuhu __________pamoja na Mungu (Mwanzo 6:9)
14. Mvua ilinyesha kwa siku ngapi mchana na usiku? (Mwanzo 7:4, 12)
15. Kulikuwa na milango mingapi katika Safina? (Mwanzo 6:16)
16. Safina ilitua juu ya mlima gani? (Mwanzo 8:4).

# Ni Lazima Mtu Awe Ndani Ya Kanisa ili Aokolewe Na Hatimaye Aingie Mbinguni

**Sunny David**

Biblia inafundisha kuwa Yesu Kristo alikuja duniani ili awaokoe wenye dhambi (1 Timotheo 1:15). Kuokolewa kutoka katika dhambi, ni lazima mtu afundishwe, amwamini Yesu na kubatizwa (Marko 16:16). Wale aliowaokoa, aliwaongeza katika kanisa lake (Matendo 2:47), ambalo ni ufalme wake (Mathayo 16:18-19; Wakolosai 1:13). Katika kuja kwake tena siku ya mwisho, Yesu ataupokea ufalme wake Yeye mwenyewe, na kumpa Mungu Baba ufalme huo ambao ni kanisa (1 Wakorintho 15:24). ***"Na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele"*** (1 Thesalonike 4:17)). Hivyo, mtu anapaswa kuwa katika kanisa ili aokolewe na mwishowe aingie mbinguni. Hata hivyo, kama vile inavyotakiwa kuamini na kutii Injili ili uokolewe na kuwa mshirika wa kanisa la Kristo, pia ni muhimu vile vile kubaki umeokoa katika Yeye hadi mwisho. Kristo alifundisha, ***"Uwe mwaminifu hata kufa nami nitakupa taji ya uzima"*** (Ufunuo 2:10).

Watu hufanyika kuwa wafuasi wa Yesu Kristo baada ya kuisikia Injili yake, kumwamini, kutubu dhambi zao, kumkiri yeye kuwa ni Mwana wa Mungu na kubatizwa kwa ondoleo la dhambi zao. Kristo, kulingana na ahadi zake, huwaongeza katika kanisa, na kujaribu kuwa waaminifu kwake kwa kuhudhuria ibada za kanisa kila Jumapili pamoja na kukaa mbali na vitu vyote viovu na tabia mbaya ambazo walizifanya hapo awali. Hata hivyo, mvuto wa dhambi na shinikizo la rika, wengi huanguka tena katika mambo ya dunia. Biblia imewaelezea Wakristo wa aina hiyo.

***“Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua, kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, “mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe,” na “nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaa-gaa matopeni.”*** (2 Petro 2:20-22).

Dhambi, ikiendelea, ni mwendelezo ambao hatua kwa hatua inafanya mioyo kuwa migumu. Mkristo anayerudia maisha yake ya awali ya dhambi, anakuwa haisikii kabisa sauti ya Mungu, pia hata dhamiri yake. Pia itakuwa kwamba hali ya sasa itakuwa mbaya zaidi kuliko ile hali aliyokuwa nayo kabla ya kufanyika Mkristo. Hapo awali alikuwa na hali ambayo ilikuwa ni rahisi kwa mtu kumfikia na Injili, kuliko baada ya kugeuka kutoka katika kile alichofundishwa. Pia, hali ile ya awali ni bora kama sifa za kanisa zinavyohusika, kwa wale ambao hawajawahi kujua na kuitii Injili ya Yesu Kristo hawaliletei kanisa lake aibu kama wale walioanguka na kurudi tena duniani.

Kubaki kuwa mwaminifu kwa Bwana Yesu Kristo, wafuasi wa Kristo wanafundishwa, ***“Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani tama ya mwili, na tama ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tama zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele”*** (1 Yohana 2:15-17).

Mapenzi ya Mungu Baba kwa watu wake ni yapi? Katika barua zake kwa Wakristo, mtume Paulo aliandika: ***“Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewa. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. Naam, kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema***

***wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katikautauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. Kwa hiyo ndugu, jitahidi zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo."*** (2 Petro 2:3-11).

Wakristo ni raia wa ufalme wa Kristo duniani; wanaingia katika ufalme wa Kristo wakati ule ule ambao Bwana anawaongeza katika kanisa lake katika kuongoka kwao (Wakolosai 1:13). Bado, mlango wa kuingia katika ufalme wa milele wa mbinguni ambao watauingia wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili, itategemea kama wamekuwa waaminifu kwa Bwana hadi kufa kwao hapa duniani [au kama wataishi hadi kurudi kwa Yesu]. Hiki ndicho kile kile ambacho Kristo alifundisha katika mfano wake wa magugu, unaopatikana katika sura ya kumi na tatu ya kitabu cha Mathayo katika Injili. Aliandika: ***"Basi, kama vile magugu yakusanywavyo na kuchomwa motoni; ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia. Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi, na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenye masikio na asikie"*** (Mathayo 13:40-43).

Kumbuka, Yesu alisema hilo katika siku ya hukumu na zawadi, malaika zake watakusanya katika ***"ufalme wake"*** vitu vyote vikwazavyo na wale waliotenda maovu! Ufalme ni nini? Ni kanisa. [Ni mwili wa waliookolewa, ambao Yesu Kristo atarudi na kuwachukua].

**Sunny David anaishi huko New Delhi, India na ni mchungaji na mwinjilisti**

# Kanisa la Mungu katika Tamaduni Iliyoharibika

**Greg Tidwell.**

Dunia inayotuzunguka inajaribu kuharibu kila mmoja na kuwaibia uchaguzi wao, na kuleta mwelekeo wa kisasa katika jamii kwa sababu matokeo yake hayaepukiki na hakuna hata mmoja anayeweza kuyaepuka. Wakati Wakristo wanapokubali kuwa katika mawazo ya kushindwa tunakuwa wenye huzuni na wenyekuvunjika moyo na mara nyingi tunapoteza mwelekeo. Hata hivyo, Mungu wetu hajatuita tushindwe bali tushinde. Mungu ametubariki kuwa na utashi, ameturuhusu kutumia uwezo wetu na haiba yetu wenyewe katika huduma yake. Tunapokubali kufuata utamaduni wa kisasa tunakuwa tunaweka matatani uwezo wa mtu mmoj mmoja aliopewa na Mungu.

Wakristo lazima washikilie mstari katika Maisha yao yote, tusikiliza maonyo ya mtume paulo: ***"Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu"*** (Warumi 12:2). ***"Kama akili zetu tunaziunda kwa juhudi kila siku kupitia kumfuata Kristo, tutaanza kuwabadilisha wale walio karibu yetu pia."*** Ndani ya kanisa maadili ni zao la kweli, kuwajenga watakatifu katika utakatifu, hivyo ushawishi wetu wa kanisa utaenda mbali zaidi. Tuna fursa kubwa ya kuwa chumvi na nuru kwa pamoja katika dunia ukiacha giza. **Afadhali kuliko mtindo wa kisasa ulionyamza na kutulia katika maji na wakati huo huo tamaduni, ujasiri wetu unapaswa kutuongoza kusema kwa uthabiti thamani ya Ukristo.**

Umuhimu wa juhudi zetu ni wajibu wetu kujadili haya mambo katika familia zetu, kuwa na Wakristo na kuzuia ushawishi wa dunia. Kuudhibiti ushawishi wa nje ndio hatua ya kwanza muhimu. Zaidi hata kufikia hatua ya hitaji la kuzielimisha familia kufanya Ukristo ndio uchaguo lao katika kufanya maamuzi yao.

## Hatari ya sisi kunyamaza ni kubwa sana

Watu wa Mungu wanapaswa kuwa na ujasiri kuhusu haki ya maadili Kibiblia. Bila kuwa mwenye haki, mambo haya tuna wajibu wa kushirikisha dunia iliyopakwa matope na kuchafuka na kupotea. Lazima tuepuke kushindwa kiakili wakati tunaposhughulika na swala la tamaduni. .

**Greg Tidwell ni mhubiri wa kanisa la Kristo Fishinger na Kenny huko Columbus, Ohio, Marekani.**

Paulo alifanya kila njia kuwaleta watu wa tamaduni zote kwa Kristo kwa kutumia tamaduni zao bila yeye mwenyewe kutekwa. ***"Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria. Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine."*** (1 Wakorintho 9:19-23). Hii haimaanishi kuwa Paulo aliweka rehani sheria ya Mungu ili awapate watu, HAPANA, bali alitumia mbinu zilizokubalika na tamaduni hizo bila kuvunja amri za Bwana. Fundisho kubwa hapa ni, katika kila tamaduni kuna jambo la kuanza nalo ili kumhubiri Kristo, tumia hilo bila ya kuanza na kebehi.

**Shadrack S. Msambaza**

## Kanisa

# Ukristo – Matembezi ya Furaha Pamoja na Mungu

**Thomas R. Dohling**

***"Mfanyieni Bwana shangwe, dunia yote; Mtumikieni Bwana kwa furaha; Njoni mbele zake kwa kuimba; Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; Tu watu wake, na kondoo wa malisho yake. Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; Nyuani mwake kwa kusifu; Mshukuruni, lihimidini jina lake; Kwa kuwa Bwana ndiye mwema; Rehema zake ni za milele; Na uaminifu wake vizazi na vizazi."*** ( Zaburi 100).

Nina shauku ya kumjadili Yesu Kristo, Bwana na Mokozi wetu aliyetupenda sisi, akafa kwa ajili yetu, ili kwamba tuweze kuokolewa kutoka dhambini. Mungu amejenga mji mahali mbinguni katika Kristo Yesu (Waefeso 2:6).

Kulikuwa na mashaka makubwa katika akili yangu kwa sababu maisha yamekuwa ya taabu, yenye machungu, na magumu. Hata hivyo shukurani zangu kwa Mungu ambaye amekuwa Mchungaji wangu [amekuwa kila kitu kwangu] na amenileta mahali ambapo najifunza kumtegemea yeye. Amenifundisha vitu vingi kwa kadiri ninavyo tembea pamoja naye, kuzungumza naye na kutafuta mapenzi yake. ufumbuzi ni **kumtegemea Mungu**. Kwa umakini tafakari yafutayo kutoka kwa ***Maana atakuwa kama fukara nyikani, Hataona yatakapotokea mema; Bali atakaa jangwani palipo ukame, Katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu. Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana, Ambaye Bwana ni tumaini lake. Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, Uenezao mizizi yake karibu na mto; Hautaona hofu wakati wa hari ujapo, Bali jani lake***

***litakuwa bichi; Wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, Wala hautaacha kuzaa matunda."***

Tazama tofauti! jinsi gani amelaaniwa mtu amtegemeaye mwanadamu [ ikiwa ni pamoja na yeye mwenyewe] na kuondoka kwa Mungu; jinsi gani tasa maisha yake yalivyo tupu! Amebarikiwa mtu amtegemeaye Mungu! amejazwa na kumwagika!

Tunapomwamini Mungu tunamwambia kila kitu, tunashirikiana naye mapungufu yetu, mambo mabaya kuhusu sisi wenyewe, mawazo mabaya, tamaa, hofu, shauku na n.k, na kumtazama yeye kuongoza maisha yetu. Anashauku ya kufanya hivyo, na atafanya kwa sababu ni Mwaminifu, na pia kwa sababu ya upendo wake! Tafakari ni kwa namna gani alitupenda… ***" Akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele"*** (Yohana 3:16) Alitaka kutuokoa ili kwamba tuwe na uzima tele (Kiroho) maisha ambayo ni mazuri na bora kuliko maisha ya kimwili.

Sasa naelewa kwamba Ukristo ni ***"Kutembea na Mungu katika Bwana Yesu Kristo"*** hivyo ni fursa ya kumjua Mungu. Hili linafurahisha zaidi, kuliko tu kujua kuhusu Yeye. Kama jinsi mtu mmoja alivyosema; "Biblia ni Ushahidi kuhusu Mungu. Tunahitaji kuwa na mizizi na kuzungukwa na upendo wa Mungu (Yohana 4:8b)." Katika neno, tunahitaji msingi wetu kuwa katika Yesu, ambaye ni Mungu alionesha upendo wake!

Tafakari sala ya Paulo kwa Wakristo wa Efeso (Waefeso 3:16-21) ***"awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani. Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu. Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;***

***naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina."***

Aliomba kwamba Mungu aweze kuwapa nguvu wakristo wa Efeso kupitia Roho Wake kuwa ndani ya mwanadamu ambaye Kristo anaweza kukaa ndani ya mioyo yao [ndani ya mwanadamu] kupitia Imani ili kwamba ,wawe na mizizi na kuzungukwa na upendo, ili waweze kuwa na nguvu na ufahamu kupita kiasi, alama ya upendo wa Kristo kwao ambao ni ushindi wa maarifa. Haiwezi kuwa ufahamu wote, kukubali haki zaidi, unyenyekevu na furaha, na kujaza wema wa Mungu wote amabaye anauwezo wa kukujaza zaidi na zaidi kile ulichokiomba au kufikiri.

Kila siku tunapokuwa na dhamiri ya kutembea na Mungu, anaruhusu mapenzi yake yafanyike katika maisha yetu, tunamfahamu Mungu na kuwa bora zaidi [kiutendaji]. Theolojia ni nadharia kuhusu Mungu, hatuishi katika nadharia, tunamjua Mungu alivyo kwa uzoefu [experience], na pale tunapodhani tunamjua, tukidhani hivyo, Anafanya jambo lisilotarajiwa, jambo fulani la kushitua na kutupiga kwa mshangao na kutufanya tutambue kwamba hatumjui vyakutosha.

Alituonesha kwamba yupo mbali, juu ya nadharia ya mwanadamu kuhusu yeye, Mungu mwenyewe alisema, ***"Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu."*** (Isaya 55:8-9).

Tembea pamoja naye kila siku, (zungumza) shirikiana naye kwa kila pumzi unayovuta na kumtegemea yeye kukutendea vizuri na utamfahamu yeye aliyeko, si kwa kila kitu bali alichokichagua kukuonesha kuhusu uwepo wake. Kuna mengi katika maisha ambayo ni ya kimwili, Mungu ametufanya kwa mfano wake, kwa sura yake na akatupa uwezo wa kumfahamu katika njia ya kidunia, katika utu wa ndani, ndani ya roho zetu ili kwamba uzoefu wa kila mtu uwe kwa Mungu mwenyewe. Hakuna mtu atakayeweza kukuelezea. Ni kati yako

wewe na Mungu. itakuwa ni uzoefu wa kipekee, ni safari! Kumbuka kusoma Neno lake na kulishika [kwa kusoma Biblia, Ushahidi kuhusu Mungu] na urahia uzuri wa kutembea na Mungu katika dunia hii hadi wakati atakapokuita moja kwa moja nyumbani kwake kukaa pamoja naye kila wakati. Ndiyo, kupitia njia rahisi na njia ngumu, juu ya milima (mafanikio katika maisha) na mabonde (hali ngumu katika maisha), atakuzingira kwa upendo wake na kukubeba na kukupitisha katika njia za haki kwa ajili ya jina lake (kwa sababu anataka hivyo), kama utamruhusu tu yeye! Furahia maisha pamoja na Mungu, anayetamani kuwa Baba yako, na Yesu Kristo ***"Yeye kwa kuwa ni mng'ao wa utukufu wake"*** {Waebrania 1:3}, ambaye anaongoza, (na kukusaidia) kupitia Roho Wake na Neno lake.

Kama Baba yetu! Mungu anapenda kutushangaza! Kuwa ni upendo, anatafuta wema wetu na upendo na kutuona wenye furaha kwa kadiri tunavyotembea pamoja naye, kwa kutafuta mapenzi yake. Kuna siku za huzuni, na kuna siku za kutisha, lakini tunajifunza kutoka katika kutembea pamoja na Mungu na hayo ndiyo yanayotegemewa katika dunia hii. Kupitia nyakati hizi ngumu na mazingira haya, tunajifunza kwamba Mungu ndiye Msaada wetu, Mfariji wetu, na Mwamba wetu, na kwamba Imani yake ndiyo tunayoihitaji kumtegemea yeye. Hata hivyo, nyumbani kwa Baba yetu vitu ni tofauti kabisa! Kule hakuna huzuni, majonzi wala maumivu. Kule kutakuwa na kuabudu na kusifu, shangwe na furaha kwa kadiri tutakavyomtazama yeye katika utukufu na wema wake. Je, nifuraha iliyoje kuwa na Mungu mwema! Utukufu una Mungu sasa na daima katika Kristo Yesu Bwana wetu! Amina.

**Thomas Dohling ni mwalimu wa darasa la Biblia huko New Delhi, India**

(Yeremia 17:5-8) ***"Bwana asema hivi, Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, Amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake Na moyoni mwake amemwacha Bwana…"***

# MAMBO MAGUMU AMBAYO HAYAPO KATIKA KANISA LA KRISTO:

**Morris S. Chiuyo**

- Hakuna mtu anayeweza kuwa mshirika wa kanisa bila kuokoka. (*Mk-16:15-16)* hatujiungi kama kujiunga na vyama.
- Hakuna Ibada inayoweza kufanyika bila maagizo ya Mungu. (*Kol-2:23)*
- Hakuna kanisa ambalo linaweza kuwa mali ya mtu. Maana kuna watu wanasema makanisa au madhehebu yao ni ya mtu fulani (*Mt-16:18, Mdo 20:28)*
- Hakuna ubatizo wa aina nyingi ili ufanyike kuwa Mkristo au kuokoka.(*Efe 4:5)*
- Hakuna huduma inayolipiwa kanisani, kama ubatizo, maombi au kumwona kiongozi.(*Mt. 10:8)*
- Hakuna mtu anayeweza kuokoka bila kubatizwa. (Yn-3:3-7)
- Hakuna wokovu wa Sala ya toba kibiblia.(*Mk-16:15-16)*
- Hakuna Askofu wala Mchungaji mwanamke katika Kanisa kwa mujibu wa Biblia.(*1Tim-3:1-2, Tit-1:6-7)*
- Hakuna Shemasi mwanamke katika Kanisa.(*1Tim-3:8-12)*
- Hakuna kuchanganya uongozi wa torati na injili katika Ibada ya Kanisa.(*Rum-7:1-6, Gal-3:10-14)*
- Hakuna Askofu au mchungaji asiyekuwa na mke kwa mujibu wa Biblia (*1Tim-3:1-2)*
- Hakuna mwanamke anayehubiri mbele ya kanisa (kusalisha ibada) (*1Kor-14:34-35,1Tim-2:8-11) isipokuwa Kanisa liwe na wanawake tu.*mtume Paulo alisema ***"Basi wapendwa wangu, kama vile mlivyotii siku zote. Si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka."*** ( Wafilpi 2:12).

**Morris S. Chiuyo ni mwalimu wa Biblia katika shule ya Biblia iliyopo Temeke, D'Salaam, Tanzania. Pia ni mchungaji mstaafu wa kusanyiko la Temeke.**

# Maswali 4

Doug Greenway NA David A.Sargent

Kwa siku kadhaa Doug Greenway aliulizwa maswali manne mara kwa mara ili kupima hali yake. Aliandika: "Nilifayiwa upasuaji wa ubongo Disemba 11 na kukaa ICU siku nne na kila baada ya dakika 30 mmoja wauguzi alikuja na kuuliza maswali ambayo niliona kuwa haya maana. Walijua kuwa nina matatizo ya shinikizo la damuu tangu wakati wa upasuaji na hawakutaka wakosee hilo kama ningeanza kurukwa na akili."

**Maswali hayo manne yalikuwa:**

**Je, unaweza kuniambia jina lako?**

**Je, unafahamu mahali ulipo?**

**Je, unafahamu kwa nini upo mahali hapa?**

**Je, unaweza kunipa dole gumba?**

**Tafakari jinsi ya kutumia kiroho maswali haya ya msingi:**

**Je, unaweza kuniambia jina lako**? Wewe ni nanni? Uwezo wako wa kuliita jina lako unaweza kuwa ni dalili ya afya yako, lakini ni kitambulisho chako katika ushirika wako na Kristo na hilo ni muhimu sana. ***"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."*** (Matendo 4:12). Hilo jina ni "**Yesu Kristo**." Kupitia Yesu pekee tunaweza kuokolewa (Yohana 14:6).

**Je, unafahamu mahali ulipo?** Je, upo ndani au nje ya Kristo? Katika Kristo tunapata baraka zote za kiroho (Efe 1:3). Nje ya Kristo hakuna tumaini (Efe2:12). Waumini wenye kutubu walibatizwa katika Kristo (Mantendo 2:38 Gal3:26-27). **Je, upo ndani ya Kristo?** Je, una mfuata kwa uaminifu?

**Je, unafahamu kwa nini upo mahali hapa?** Watu wamekuwa wakifikiri kujibu hilo swali kwa njia nyingi tangu kuanza kwa ulimwengu. Jibu sahihi ni: Tupo hapa kumtukuza Mungu aliyetuumba. ***"Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu."*** (1Kor. 10:31). Tunamtukuza Mungu kupitia Kristo, wafuasi wa Kristo (1 Petro 4:16).

**Je, unaweza kunipa dole-gumba?** Je, unaishi vizuri katika kumpa Mungu kipaumbele? Mtume Paulo alitoa "dole-gumba" karibu na mwisho wa maisha yake. ***"Kwa maana, mimi sasa namiminwa, na wakati wa kufariki kwangu umefika. Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda; baada ya hayo nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake."*** (2Timotheo 4:6-8).

Kiini cha kujibu swali hili kwa usahihi ni Kristo, kwa kuwa Mungu anatupenda sana hata akamtoa Mwanawe kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu (Yohana 3:16). Ni kwa kupitia zawadi ya Yesu tunaielewa kusudi la maisha na jinsi ya kupokea uzima wa milele kupitia Yeye.

Mungu atatuokoa na kutupa uzima wa milele kwa wale ambao wana Imani na kumtegemea Yesu (Matendo 16:30-31) wakiziacha dhambi zao katika toba (Matendo 17:30:31), wakimkiri Kristo mbele za watu (Warumi10:9-10), na wakabatizwa (kwa kuzamishwa) katika Kristo kwa msamaha wa dhambi zao (Matendo 2:38). Ataendelea kuwasafisha kutoka katika dhambi wale ambao wataendelea kutembea katika nuru ya Neno lake. ***"bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote."*** (1Yohana1:17). Hivyo, jiulize mwenyewe maswali hayo manne, na uyajibu kwa kusema "ndiyo" kwa Yesu kupitia kumtegemea na kumtii.

**David A. Sargent ni mtumishi wa kanisa la Kristo Creekwood huko Mobile, Alabama, Marekani.**

## Fundisho La Kuishi Kwalo

# Nipeleke Mlangoni, Bwana

**Patrick Morrison**

Huenda ni moja ya sheria ya ajabu kupatikana katika ukurasa huu wa Biblia Takatifu iliyorekodiwa katika kitabu cha Kutoka 21:4-6 chini ya sheria ya Agano la kale. Waisraeli walitakiwa kuwaachia watumwa wa Kiebrania baada ya miaka sita ya kutumika. Waebrania wengi ambao walikuwa watumwa walifayika kutokuwa na umuhimu mara nyingi. Walijifanya watumwa wenyewe ili kulipa deni kubwa. Baada ya miaka sita ya kutumika walikuwa huru Kwenda au kutokwenda hata kama deni limelipwa kabisa. Hata hivyo, watumwa wa Kiebrania walikuwa na uchaguzi wa kuanzisha maisha mapya kama raia huru, au angeweza kubaki kwa bwana wake kwa maisha yake yote.

Unaweza kujiuliza mwenyewe kwa nini mtumwa achague kubaki kuwa mtumwa badala ya Kwenda kuwa huru? Kama mtumwa anampenda bwana wake, ana haki kisheria kubaki na bwana wake kwa maisha yake yote. Kwa kufahamu shauku yake ya kubaki na bwana wake, mtumwa alikuwa akipelekwa kwenye miimo ya mlango. Basi bwana wake atamtoga sikio na msharasi, hapo atawafanya watu wote wamwonao huyu mtumwa kufahamu kuwa uamuzi aliofanya ni kubaki katika kumtumikia bwana wake.

Na ndiyo sababu watumwa hao bado wapo leo ulimwenguni kote. Kama wapo au hawapo kila mtu anatambua hilo, watu wote duniani ni watumwa. Ama anamtumikia Mungu, au ni mtumwa wa dhambi. Hakuna kukaa kati (Mathayo 6:24). Utumwa wa dhambi huleta aina fulani ya uhuru, uhuru mbali na Mungu (Isaya 59:1-2), uhuru kutoka katika baraka ambao unaweza kupatikana kwa Kristo pekee (Efe 1:3) na ni uhuru kutoka katika wokovu (Warumi 6:23). Kumtumikia Kristo pia kuna uhuru wake, uhuru kutoka katika hatia ya

dhambi (Matendo 2:38) na uhuru kutoka katika mateso ya Shetani ya Jehanamu (Yohana 3:16).

Tuna deni kubwa kwa Mungu ambalo kamwe halitawezekana kulipwa, na si katika miaka sita, si katika miaka 6000 na hata miaka milioni 6, ni uchaguzi wetu kubaki na Mungu ambaye wote tu wadeni, au tutembee katika njia ya dhambi, hapo tutajikuta tupo wenyewe kwenye matokeo ya kuteseka chini ya mzigo wa dhambi na taabu. Mungu hatatushika kinyume na mapenzi yetu, lakini Shetani atatujaribu na kutukamata katika maovu yake. Na ndiyo sababu Shetani hajali jinsi watumishi wake wanavyomtendea, lakini Mungu ana wahesabu wale ambao wanamtumikia kama wanawe badala ya watumwa (Luka 5). Wale ambao wanamtumikia Mungu wanaweza kushuhudia kuwa Mungu kweli ni wa rehema na ni Bwana wa upendo.

Je, unampenda Bwana? Kama kweli tunampenda Bwana, tungefanya kile alichotuamuru kufanya katika Neno lake (Yohana14:15). Wote tufanye maamuzi ya kumtumikia Bwana kwa kadiri tutakavyoishi katika ulimwengu huu. Na ulimwengu wote uone kwamba tumefanya maamuzi ya kubaki pamoja na Bwana wetu milele. Ulimwengu lazima uone kwamba tumetogwa masiko na msharasi wa Bwana, kiroho. Wote ambao waliochagua kubaki pamoja na Bwana, kamwe hawatasahau ni kwa nani wametoa utii wao. Je, utachagua kuwa raia huru wa ufalme wa Mungu kwa kujitoa mwenyewe katika huduma yake? Bwana amesimama mlangoni anakusubiri. Hebu maisha yetu ya zungumze na Bwana, Kusema; "Bwana nichukue nipeleke mlangoni leo hii."

**Patrick Morrison ni mhubiri wa kanisa la Kristo Sixth Avenue huko Jasper, Alabama, Marekani.**

**Kutoka 21**

**"6 ndipo hapo huyo bwana wake atamleta mbele ya Mungu na kumleta mlangoni, au penye mwimo wa mlango; na bwana wake atalitoboa sikio lake kwa uma; ndipo atamtumikia sikuzote."**

# Maisha Mapya Utakapobatizwa

**Owen D. Oibricht**

Mtu mmoja aliniambia kwamba ubatizo haukuwa wa lazima ili kuokolewa kwa sababu alifahamu watu waliokuwa wamebatizwa ambao hawakuishi maisha ya Ukristo. Tathimini yake haikuthibitisha ujumbe wake kwamba ubatizo si muhimu. Tokea hapo watu ambao hawaishi maisha mapya baada ya ubatizo wanaweza wasielewe mafundisho ya Biblia kuhusu ubatizo.

Ubatizo ni ***"kuzikwa…..kwa njia ya ubatizo."*** (Warumi 6:4) ambao pia ni ufufuo (Wakolosai 2:12). Je, yote hayo yanahitaji ubatizo? Katika Warumi 6 Paulo anasema upo uwezekano wa kutokuelewa kwa kile kilichoandikwa katika sura ya 4 na 5 alianza kwamba Yesu mwenye haki ***"bali na kwa ajili yetu sisi mtakaohesabiwa vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu; ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na kufufuliwa ili mpate kuhesabiwa haki."*** {Warumi 4:24-25} Mawazo ya Paulo hayakuishia kwenye sura ya nne. Aliendelea ***"Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani,"*** {Warumi 5:1}. ***"Lakini sheria iliingia ili kosa lile liwe kubwa sana; na dhambi ilipozidi."*** {Warumi 5:20}. Hoja ya Paulo ilikuwa kwamba kwa kuzikwa na kufufuka, Yesu aliandaa mpango wa rehema amabao ungeondoa dhambi zetu zote.

Tena Paulo anasema upo uwezekano wa kuwa na hitimisho lisilo sahihi. Kama rehema inatosha kutuondolea dhambi zetu zote, basi tunaweza kutenda dhambi zaidi ili kwamba rehema izidi kuwa nyingi. Paulo alilikemea hili kwa kusema kwamba dhumuni la neema sio kutupa kibali cha kutenda dhambi, kwa maana tuliifia dhambi (Warumi 6:1-2) pindi tulipozikwa pamoja na Yesu katika ubatizo katika kifo cha dhambi na kufufuliwa pamoja naye, ***"…vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."*** (Warumi 6:3).

Kueleweka vizuri, ubatizo ni hatua ya kugeuka katika maisha yetu tunapofia maisha yetu yaliyopita ili tuishi maisha mapya pamoja na Kristo. Ubatizo si tendo tu la kuzikwa ndani ya maji na kutolewa ndani ya maji. Si hivyo tu vinavyohusika katika ubatizo. Unahusisha si tendo la nje tu bali pia mwitikio wa ndani, mlitii ***"kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake"*** (Warumi 6:17-18). Matokeo ya utii wetu kutoka moyoni katika ubatizo yanapaswa kuwa uhuru kutoka katika maisha ya dhambi, baada ya kujihesabu kuwa tumezifia dhambi. (Warumi 6:11).

Ikiwa tutaelewa ushiriki wetu wa kiroho katika ubatizo, tutatambua kuwa ni kuzaliwa upya (Yohana 3:5), ambao baadaye tunakuwa na utu upya, si utu wa kale tuliokuwa nao. Kabla ya ubatizo tunazifia dhambi, lakini kupitia imani na Mungu kufanya kazi, tunapofufuliwa pamoja na Kristo katika ubatizo tunafanywa kuwa hai na ouvu wetu wote unasamehewa (Wakolosai 2:12-13).

Katika sura inayofuata, Paulo anarudia mawazo yake, na kuandika ***"Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko"*** (Wakolosai 3:1). ***"Mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake"*** (Wakolosai 3:9). Utu wetu wa kale unaisha tunapobatizwa na maisha mapya yanaanza kwa kila mmoja wetu. Kama hatulielewi hili tunakosa fundisho ambalo katika ubatizo ambao tunashiriki na Yesu, kufa na kufufuka kwake. Tunaingia katika utu upya kama alivyoingia katika utu upya alipofufuka. Hivyo, tunaacha uovu upite na kuwa mtu mpya.

Kama mtu anayebatizwa hatambui kuwa anaufia utu ule ambao alikuwa nao na kuwa mtu mpya, hawezi kuwa mpya, bali ataloa tu. Ubatizo ni zaidi ya tendo la mwili pekee, kwa kuwa utaleta kuzaliwa upya kiroho kwa yule anayebatizwa (Yohana 3:6).

**Owen D. Olbricht ni mhubiri na mwandishi, anaishi Sherwood, Arkansas, Marekani.**

# Maoni ya Haraka Katika Aya Muhimu

**(1 Petro 5:6-9)**

**6 Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake;**

**7 huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.**

**8 Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze.**

**9 Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani.**

Hili ni somo linalokinzana baina ya kujihusisha kwa Mungu katika maisha yetu na majaribio ya udanganyifu ya Shetani yasiyokoma na kuwaharibu wana wa Mungu. Kwanza, tunahakikishiwa kwamba tunaishi chini ya mkono wa Baba mwenye nguvu. Ikiiwa tutajisalimisha Kwake vikamilifu, Atatufanikisha katika maisha yetu cho chote tunachokihitaji (furaha, maumivu, majaribu, ushindi, vifaa mbalimbali) ili kututengeneza tuwe aina ya wana anaoweza kuwatumia katika ufalme wake, na ahadi ipo kwamba ni hakika tutashinda katika siku ya kukwezwa!

Mungu anachohitaji kutoka kwetu, katika mchakato wa kutengeneza, ni kwamba Imanii yetu inatuwezesha kuwa na hali ya kumjali Mungu. Kwa nini? Kwa sababu Mungu anatupenda na anataka kilichobora kwetu.

Lakini kuna adui ambaye muda wote anatafuta roho dhaifu ili aweze kuzipoteza kwa kutumia vifaa vyote alivyonavyo: majaribu, tamaa, kukata tamaa, kushindwa, hata mafanikio yanaweza kumgeuza mtu asiwe na moyo wa kumtumikia Mungu.

Tunapaswa kufanya nini? Kwanza, ni lazima tukatae kila kitu Shetani anachotutupia, kwa nguvu zetu zote kujumuisha nguvu za Roho Wake aliye ndani yetu. Kisha tujichunguze mioyo yetu na kuhakikisha tunasalimisha kila kitu chetu kwa Mungu, tukiamini katika uangalizi wake, na kung'ang'ana na imani bila kujali magumu yote na changamoto zinazotujia, kwa sababu mateso yatakuja, lakini changamoto hizo pekee zitatusogeza karibu na Mungu. **Warumi 8 ina hoja nzuri kuhusiana na mawazo haya.**

# KUHUBIRI KATIKA TAMADUNI ZA LEO

Andy Robin

Katika maeneo mengi, nimehubiri kipengele hiki, na sasa inaonekana wakati wa kuendeleza katika maandishi. Acha nianze kwa kusema dhahiri. Tamaduni za Marekani za mwaka 1955 ni tofauti na zile za leo. Kipindi hicho, wengi walikuwa waenda kanisani, na wengi walidai kuwa wamefungamana na Kristo. Hivyo, msukumo wa kanisa la Bwana, ulikuwa ni kuwaongoa watu kutoka kwenye uongo wa kimadhehebu. Lengo ni kuwaunganisha waaminio katika ukweli wa wakristo wa Agano Jipya uliorejezwa. Vita hivyo bado vinatakiwa kupiganwa leo! Hata hivyo, tamaduni za sasa zinatofautiana.

Marekani ya leo, watu wachache isivyo kawaida ndio wanaoenda katika kanisa lo lote lile. Wengi humkana Mungu kuliko ilivyokuwa hapo awali. Vizazi na vizazi vya familia hawajawahi kukanyaga katika eneo la kuabudia. Wengi wanaendelea katika upagani: Uislamu unazidi kupenya. Maandamano ya kuelekea kukosa maadili ya wazi yanafagia taifa [na dunia], kisheria na kimahakama. Majengo ya makanisa ya kimadhehebu yanakuwa matupu taratibu.

Hii inamaanisha nini kwa uinjilisti? Kwanza, haimaanishi kuibadili Injili. Hakika, ukweli wa Injili hauwezi kubadilishwa, bali kupotoshwa tu, na hilo lina matokeo ya huzuni ya milele (Wagalatia 1:6-9). Mafundisho ya Mungu kuhusu maadili, wokovu, uhuru wa kanisa, umoja, upendo, ndoa, maisha na masomo yote yanabaki kuwa yale

yale (Mathayo 28:20; Yuda 3)! Bado mabadiliko katika tamaduni yana athari katika mtazamo wetu wa kufundisha.

Wakati Paulo akihubiri katika tamaduni za Kiyahudi huko Antiokia katika Pisidia. Sehemu aliyoanzia ilikuwa, ***"Enyi waume wa Israel, nanyi mnaomcha Mungu, sikilzeni. Mungu wa watu hawa Israeli aliwachagua baba zetu……"*** (Matendo 13:16-17). Tena akahutubia kuhusu historia ya Waisraeli na kuendelea kuelekea kwa Kristo. Sijawahi kuanza hotuba kwa maneno yanayofanana kwa sababu sijawahi kuhubiri katika tamaduni za Kiyahudi. Paulo alipohubiri huko Athene, Ugiriki kipindi hicho hakukuwa na jamii ya Kiyahudi, lakini kulikuwa na waabudu sanamu wengi. Mji ulikuwa na sanamu zilizowekwa kila mahali, na wanafilosofia walijadili kila kitu kipya. Mitume wangekabili hadhira iliyochanganyikiwa na hatimaye kufukuzwa kama angeanza na ***"Mungu wa Israeli amewachagua baba zetu…."*** Badala yake alianzia pale walipokuwa pamoja na kukiri kutambuliwa kwa mambo yao ya kiroho na mazungumzo kuhusu sanamu yao iliyowekwa ***"Kwa Mungu asiyejulikana"*** (Matendo 17:22-23). Hivyo, alipata umuhimu.

Alithibitisha kwamba alikuwa ni Mungu ambaye ni Mungu wa kweli, Muumba wa vyote. Alijadiliana nao kutoka kwa wanafilosofia wao na akili zao wenyewe kabla hajaendea masomo ya biblia. Hata hivyo, aliishia kuwahubiri injili ile ile kamili, akiwaambia watubu na kujiandaa kwa ajili ya hukumu (Matendo 17:30-31). Tamaduni yetu ya sasa inaakisi zaidi Athene, Ugiriki na Antiokia katika Pisidia. Inafanya vizuri kidogo kumwuliza mtu kuhusu kujifunza Biblia wakati (a) hana Biblia (wengi hawana) (b) haiamini kwanza. Kwa nini, hamwamini Mungu? Inawezekana kuwa vijana wengi wenye miaka zaidi ya kumi na nane wanajikuta kwenye maumivu ya kubadili tamaduni (hawakujua za zamani, wanaathiriwa na mpya) wamepotea hata baada ya malezi mazuri ya kwenda kanisani kwa sababu tu anaweza akawa amekosa sehemu hii. Labda tumefanya vizuri katika kuhubiri injili kutoka katika

sehemu ya kuwajibu marafiki zetu wa kimadhehebu. Hata hivyo, labda, katika baadhi ya mambo (kusamehe kwa ujumla wa kutoa hoja), vita ambavyo vijana wanapigana si pamoja na madhehebu, bali na wasiomwamini Mungu, wanamageuzi, wanadamu, Madhehebu au hata wapagani. Hapa si kushtaki dhambi au kosa. Watu wazima na kila mmoja bado wanahitajika kujiandaa kwa ajili ya vita ambamo walilelewa (sawa na Antiokia).

Hata hivyo, mambo yamebadilika kwa haraka. Ninaweza kushauri kwamba labda mabadiliko yamekuwa ya haraka sana na ya ghadhabu (katika tamaduni za Athene) ambazo zilitupa shida kuzifuata. Mara, nilipokuwa na uzoefu unaoumiza wa kumpoteza mwongofu mpya katika fundisho la mageuzi. Hivyo, nikaamua kuandaa kusanyiko lote dhidi ya udanganyifu huu. Nilihubiri baadhi ya hotuba kuhusu ushahidi wa Kikristo. Kwa nini tuamini kwamba kuna Mungu? Nilipomaliza mzee wa kanisa akatoa wazo, “Tunafurahi umelimaliza; tayari tunaamini hilo.” Labda ni kwa namna nilivyolitoa; labda kwa namna nyingine ni kosa langu. Kwa upande mwingine inaweza kuwa wazo la namna hiyo lilikuwa (hata bila hatia) kutokuwa na maono katika kuandaa kizazi kipya kwa ajili ya changamoto zao?

Ukamilifu wa Injili una majibu ya kila changamoto! Katika baadhi ya watu wa dunia, wahubiri wanaanza kuhubiri dhidi ya ibada za mababu. Sijawahi kufanya hivyo, lakini katika tamaduni hizo, wanafanya hivyo. Mara zote Injili inafaa! Ni juu yetu kujifunza Injili, kujifunza tamaduni na kuonesha umuhimu. Injili inapaswa kukingwa katika kila hatua kuanzia mahali ambapo kila mtu alipo. Tunaweza kuifanyia kazi Injili kuwa muhimu katika umri wetu, bila kubadilisha maudhui yake? Kufanya hivyo ni zaidi ya kibiblia. Ni lazima.

**Andy Robison ni mhubiri wa kanisa la Kristo Hillview Terrace na ni Mkurugenzi wa Shule ya Mahubiri ya West Virginia huko Moundsville, West Virginia, Marekani.**

# ACHA NURU YAKO IANGAZE KATIKA JAMII

Martha Lynn Rushmore



Kama Wakristo, tunawezaje kufanya nuru yetu iangaze katika jamii zetu? Je, tumemvaa Kristo kama **nuru** ya maisha yetu? Hatuwezi kuwa washawishi ambao tunataka tuwe ilimradi tu tumefanyika Wakristo. Hivyo, ni lazima tulifuate Neno la Mungu ili tuwe wana wa Mungu. Hebu tutafute ni namna gani mtu anafanyika kuwa mwana wa Mfalme!

Kwanza, mtu anapaswa kulisikia neno la Mungu kama ilivyoelezwa katika Warumi 10:17, ***"Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo."*** Pili, mtu lazima aamini neno la Mungu kama ilivyonukuliwa katika Marko 16:16, ***"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."*** Tatu, mtu atahitajika kutubu

dhambi zake. Lazima kuwe na badiliko la moyo (akili) na badiliko la matendo. Luka 13:3, 5 inasema ***"Nawaambia sivyo, lakini msipotubu ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo."*** Hili lazima liwe la muhimu kwa Kristo aliponena maneno haya mara mbili akisisitiza kwamba mtu - si hatakiwi – lazima atubu. Nne, ni muhimu kukiri kwamba Yesu ni Kristo ni Mwana wa Mungu. Warumi 10:9-10 panasema, ***"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."*** Mwisho, muumini aliyetubu lazima abatizwe katika Kristo, halafu, Bwana wetu amzidishe katika kanisa lake. Katika Matendo 2:38 tunapapata pameandikwa, ***"Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*** Baada ya kufanya yale yote yanayohitajika, Kristo ndiye pekee anayetuongeza katika kanisa lake. Matendo 2:47 pameandikwa, ***"Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote, Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."***

Tunawezaje kuifanya nuru yetu iangaze? Lazima tumuige Kristo kwa namna tunavyoongea na kutenda. Tunaangaliwa na wale wote wanaotuzunguka. Maisha yetu ni kama kurusha kokoto ndogo katika bwawa la maji; mawimbi yanaendelea na kuendelea. Hatujui ni nani au ni namna gani tunawashawishi wale wanaotuzunguka kwa matendo na maneno yetu. Hakuna mtu anayeishi au kujifia mwenyewe (Warumi 14:7). Hivyo wote tunene na kutenda kama Kristo alivyofanya alipokuwa duniani.

**Martha Lynn Rushmore ni Mhariri wa jarida la Sauti ya Kweli Kimataifa na Gospel Gazette la mtandaoni. Yeye pamoja na mume wake ni wainjilisti wa ndani na kimataifa. Wanaishi Winona, Mississippi, Marekani.**

# SIKIA NA MTII BWANA YESU

**Tim Childs**

Karibia na hitimisho la Hotuba ya Mlimani iliyotolewa na Yesu kwenye kundi la watu. Alithibitisha, ***"Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa Mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni"*** (Mathayo 7:21). Hiki ni kifungu ambacho kinapaswa kukaa akilini mwetu. Hatupaswi kuimaliza siku bila kutafakari maana yake na umuhimu katika maisha yetu na wengine wanaotuzunguka.

Neno ***"Bwana"*** limetafsiriwa kutoka katika neno la Kiyunani *kurios*, kulingana na ufafanuzi, ni cheo cha mtu ambaye ni ***"mkuu katika mamlaka, ambaye ni mtawala."*** Thayer aliongezea kwamba wenyecheo ni wale ***"wenye heshima, utii na ukuu, ambao watumwa huwasalimu wakuu wao."***

Yesu alikuja hapa duniani, kwa sehemu, kuleta ujumbe wa mapenzi ya Mungu kwa watu wote ili tusiishi na kufa katika ujinga. Katika maombi yake kwa Baba, Yesu alisema, ***"Kwa kuwa maneno uliyonipa nimewapa wao…"*** (Yohana 17:8). Mungu hapepesi macho tena katika ujinga, bali anawaamuru watu wa kila mahali watubu (Matendo 17:30).

Sauli wa Tarso aliuliza swali sahihi alipomwuliza Yesu, "Bwana wataka nifanye nini?" (Matendo 9:6). Anaonesha hekima kuu, Sauli, alifanya kama vile Bwana alivyomwambia afanye. Alikwenda katika mji wa Dameski na kumsubiri Anania. Mwishowe Sauli alisamehewa dhambi zake zote alipooshwa kwa damu ya Kristo kwa kuitii sauti ya mjumbe wa Mungu, Anania (Matendo 22:16).

Yesu hataki kusikia kazi isiyo na maana. Je, Yesu angeweza kutuuliza mimi na wewe swali hilo hilo alilouliza katika baadhi ya nyakati zake? ***"Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo"*** (Luka 6:46)?

**Tim Childs ni mhubiri wa kanisa la Kristo Warner Robins huko Warner Robins, Georgia, Marekani.**

# Mmeuzunguka Mlima Huu Kiasi Cha Kutosha

Jeff Archey



Mungu anathibitisha maelekezo matakatifu kupitia Musa, ***"Mlivyouzunguka mlima huu vyatosha…"*** (Kumbukumbu 2:3). Kwa maneno mengine, Israeli, mmezunguka kingo za mlima huu kwa siku kadhaa; ni wakati wa kuendelea mbele sasa!

Kwa maana nyingine, kuna "milima" tunayopita katika maisha au kuzunguka tena na tena. Tunabaki katika mwelekeo wa zamani, lakini tunahitaji kumsikiliza Mungu na kugeukia mwelekeo mzuri. Marafiki! Kwa nini tusiamue kufanya hivyo? Tunajipa changamoto ya kufuata kile ambacho Mungu anatuelekeza leo. Ni wakati ambao tunaacha kuzunguka milima!

Kupoteza muda ni mlima ambao tunauzunguka. ***"Mkiukomboa wakati maana zamani hizi ni za uovu"*** (Waefeso 5:16). Kama Robertson alivyoiweka, ***"Wote tuna wakati unaofanana."*** Paulo

anakwenda katika soko lililo wazi na kulinunua kwa kulitumia kihalali.” Kuna sababu: ni muhumu kutumia muda wetu kwa hekima na kwa usahihi. Mungu anatukataza tusiwe kama Feliki katika Matendo 34:34-35. Alituma kwa ajili ya Paulo, lakini baadaye alitetemeka kwa kile alichokisikia. Hakuna mfano kutoka kwenye Maandiko ambapo Feliki anamwendea Kristo. Tunazunguka huku na huku bila kutumia muda kwa hekima. Pangilia kwa makini na uweke vipaumbele kwa umuhimu.

Kutojali. Kutokujali tu. Unaweza kufikiri? Hakuna hisia, hakuna huruma hakuna kujali chochote wala mtu yoyote. Katika Ufunuo 3:14-16, kanisa linaruhusu mambo ya dunia kuongoza jitihada zao, Bwana akawaamuru watubu! Hakika mlima ambao unatuzungusha huku na kule bila kuwa na mwelekeo wala kujali. Ah, “geukia upande wa kaskazini” rafiki!”

Hofu ni dira ambayo haina mwisho. Huku na huku ukiwa na hisia itatatuka. ***“Msijisumbe kwa neno lolote, bali katika kila neno kwa kusali, na kuomba pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu”*** (Wafilipi 4:6). Zielekeze zote kwa Bwana – shida, hofu na migogoro. Siku zote kumbuka kanuni hiyo kuhusu hofu: ikiwa hutafanya chochote kuhusu hilo, hofu haitaibadili njia, na kama utafanya jambo kuhusu hilo, fanya kazi na usiwe na hofu.

Ujinga ni mlima (Hosea 4:6). Ujinga ni usumbufu. Wale Waberoya hawakuruhusu ujinga kupenya katika maisha yao (Matendo 17:10-11). Ujinga na kukataa kujifunza ni kama yule ***“daima hujifunza, na kamwe asipate ujuzi wa kweli”*** (2 Timotheo 3:7). Hebu na tukuwe katika ujuzi wetu na tuuweke katika matumizi (2 Petro 3:18).

Kupoteza wakati wenye thamani, kutojali, hofu na ujinga. Kuna mengi yaliyoko duniani ambayo yanazunguka milima hii na kutofika popote. Sifa ni kwa Mungu kwamba tuna mwelekeo wa kwenda! Rafiki mpendwa, je, una mwelekeo na mpango sahihi?

**Jeff Archey ni mhubiri wa kanisa la Kristo East Side huko Cleveland, Tennessee, Marekani.**

# BURUDANI NA IBADA YA KWELI

Basil Overton

Kuna aina nzuri na aina mbaya za burudani. Kiasi chochote cha aina mbaya ni kingi sana. Pia burudani nzuri inaweza ikafanywa kupitiliza. Tunaishi katika kipindi ambacho kinaweza kuitwa "kipindi cha burudani."

Mtu mmoja aliyekuwa maarufu sana katika vipindi vya usiku vya Runinga alianza kufanya kazi katika Runinga nyingine ya mtandaoni. Watu wa mtandaoni walisema alipata malipo yaliyozidi kutoka dola milioni saba kwa mwaka hadi dola milioni kumi na nne kwa mwaka. Mshahara wa raisi wa Marekani ni dola 200,000 ya mapato ya kodi kwa mwaka. Pamoja na mahitaji na ugumu wa kazi yake. Nina uhakika raisi anapata kila shilingi yake.

Pamoja na kuwa mshahara wa raisi unalipwa na walipa kodi, ukilinganisha na mshahara wa dola milioni 14 kwa mwaka, mshahara wake ni mwonekano wa kawaida wa vipaumbele vya Marekani havina usawa. Ni sawa na huyu mtangazaji wa Runinga aliyetajwa hapo juu atalipwa zaidi katika miaka miwili zaidi ya maraisi wote wa Marekani waliolipwa katika miaka 200 tangu George Washington alipokuwa raisi. Ni kama vile mapato ambayo mtangazaji huyu atalipwa yatakuwa zaidi ya fedha zinazotosha kulipa mshahara wa raisi.

Ann Landers alisema katika moja ya safu zake kuwa mshindani wa tuzo Evander Holyfield alilipwa dola milioni 60 mwaka 1990. Pia alisema Loe Montana alilipwa dola milioni tatu na nusu mwaka 1991 na kukosa baadhi ya michezo kwa sababu ya kiwiko kuumia. Orodha ya wanariadha hao wakubwa wanaolipwa sana itakuwa ndefu sana kuchapishwa hapa.

## Wanaweza kulishawishi kanisa

Tamaa ya burudani inaweza kuwa tayari imeathiri kanisa. Inaweza kuwa kipindi hiki cha burudani kimezungukwa sana, kimejaa na kutiishwa na watu wengi ambao baadhi katika kanisa wanatarajia kuburudishwa katika vipindi vya ibada. Inaonekana kuwa mapumziko mafupi kutoka kwenye burudani yanahusisha baadhi ya wanaoingia vipindi vya ibada inaonekana kuwasababishia kutofurahia kwa sababu hawaburudiki.

Wanaweza kusema “sikupata cho chote katika ibada” huenda baadhi hawaelewi chochote kwenye ibada kwa sababu hawazingatii kwenye ibada. Zaidi ya hayo Wakristo hawapaswi kuhudhuria vipindi vya ibada kwa mtazamo walio nao wa kujifurahisha katika ibada. Badala yake wanapaswa kuhudhuria na mtazamo kuwa wapo pale kwa ajili ya kumwabudu Mungu na kufanya vizuri katika kusifu na kumwomba Mungu.

Kama muhubiri si wa kisasa na baadhi yao wanachoka. Anahubiri neno la Mungu, na kile ambacho watu wanahitaji kusikiana, na si kuwaburudisha baadhi ya watu. Kama muhubiri hafundishi njama, mbinu za kuiba, kununng’unika, kusimulia habari za kidunia/ za mtaani kila wakati anapoanza somo lake, tena anawasimulia zaidi habari kama hizo katika somo lake, kwa mtu mwingine zinachosha.

Nimewahi kusikia kuhusu muhubiri aliyekuwa akijitahidi kusimulia habari za kutisha za kusulibiwa kwa Mwana wa Mungu, na kugundua kwamba watu walikuwa hawamsikilizi vizuri. Baadhi yao walikuwa wakisinzia. ghafla mhubiri akaanza kusimulia habari aliyoitunga kuhusu mbwa, wakaanza kumsikiliza; Mhubiri akasema; “nilikuwa nawasimulia habari za Mbarikiwa Mwokozi aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu mkasinzia. Nimeanza kuwaburudisha na habari ambayo si ya kweli kuhusu mbwa aliyekufa, na nikapata usikivu wa kila mtu.

Nimewahi kusikia kanda/CD iliyorekodiwa ikizungumza (siwezi kuita ni mahubiri) ambayo ilitengenezwa na mhubiri wa madhehebu

katika mkutano wao mkubwa wa injili uliokuwa ukifanyika huko Nashvile Tennessee. Pamoja na mambo ya dhihaka aliyosema “alisisitiza kwamba ibada inapaswa kuwa sherehe. Alisisitiza hili katika mazingira ambayo aliweka wazi zaidi kuwa huduma ya ibada inapaswa kuwa ya kuburudisha. Alisema kuwa watu hawavutiwi na mafundisho, lakini hakusema lo lote kuhusu mafundisho yaliyopo katika vifungu vya Agano Jipya ambavyo vinasisitiza umuhimu wa mafundisho ya kweli. Alikuwa akitumia mafundisho ambayo si ya kweli. Ambayo hayakuwa na umuhimu kwao. Aliweka wazi kuwa tunahitaji kuwa na ulimwengu wa burudani katika ibada zetu kama tunataka kuwashawishi watu. Bila shaka tunapaswa kuwa marafiki katika huduma zetu za ibada lakini pia **kuwa machachari na kupiga makofi kwa furaha au hisia kali hakuthitishi kuwa ni ibada ya roho na kweli.**

## Ibada ya Kweli

Kwa miaka iliyopita, nimeona mambo mengi ikiwa ni pamoja na wahubiri wa madhehebu kusisitiza kile tunachoweza kupata kutoka katika Ibada, ndiyo Wakristo wa kweli wanaweza kupata kitu kutoka katika Ibada, lakini hilo lisiwe ndio kusudi katika ibada. Kusudi la kuabu ni kile tunachokiweka katika kuabudu na kugeuza mioyo yetu kwa Mungu Baba yetu na Muumbaji wetu na kujitoa katika kumsifu na kumtolea, na kukubali kuwa bila Mungu sisi ni bure.

Yesu alisema tunapaswa kumwabudu Mungu ***“katika roho na kweli”*** (Yohana 4:24) katika mafundisho ya kifungu hiki cha Agano Jipya, tunafahamu kwa maana hii kuwa lazima tumwabudu Mungu katika mtazamo sahihi na katika njia ambayo Mungu amesema tumwabudu yeye. Kama mtu anachoka anapomwabudu Mungu kama Mungu alivyosema tumwabudu, kwani yeye si masikini wa roho.

**Basil Overton (1925-2013) alikuwa Mhariri wa muda mrefu wa Mwinjilisti wa Ulimwengu na kuishi huko Florida, Alabama, marekani.**

# Je, Upo Tayari Kwenda Umbali Kiasi Gani ili Ukaabudu?

**Mark T. Tonkery**

Naifahamu familia moja ambayo ilikuwa ikisafiri umbali wa masaa mawili na nusu kwenda kupata huduma ya ibada. Walikuwa wakiishi Marekani na hilo ndilo lililokuwa kusanyiko la karibu kabisa kwao la Kanisa la Kristo. Hii familia ilikuwa imejitoa na kuazimia kumwabudu Mungu. **Je, ni umbali gani mahali ambapo upo tayari Kwenda kuabudu?**

Katika Biblia tunasoma habari za mtu mmoja ambaye alikuwa amejitoa katika kumwabudu Mungu katika kitabu cha Matendo ya Mitume 8:26-40 tunasoma Habari za Towashi.

Maandiko yanatuambia kwamba Towashi alikuwa akisafiri kurudi nyumbani Ethiopia baada ya kwenda Yerusalemu kuabudu. Alikuwa akiweza kusafri mamia ya kilomita kwa gari la wanyama kwenda tu katika Hekalu, ili kumwabudu Bwana. Wakati huo, kipindi kile angeweza kwenda tu barazani kwa mataifa kwa sababu hiyo ndiyo iliyokuwa kazi ya matowashi. Hii ingekuwa kama vile leo mtu asafiri mbali na masaa mengi kwenda kwenye mkutano wa Injili ili afike kwenye jengo la Kanisa na kuruhusiwa kusimama kwenye mimbari. Lakini Towashi aliamua kwenda hivyo hivyo kumwabudu Mungu. Wakati Towashi alipokuwa akirudi nyumbani, aliendelea kuikuza Imani yake kwa kujifunza Biblia, na kusoma katika kitabu cha nabii Isaya.

Katika kujifunza Biblia pekee kulimwongoza kuongolewa na Filipo, ambapo Towashi aliamini na kubatizwa (Matendo 8:35-40).

Hebu fikiria kama huyo Towashi angesema kati ya haya yafuatayo: “Ni mbali sana kwenda kuabudu” “Kwa nini niende kuabudu”, “sipati cho chote kwenye hiyo ibada”, “Nina nguvu ya kutosha kiroho kiasi

kwamba sihitaji kwenda kuabudu", "Nimechoka sana, au nina usingizi mzito siwezi kwenda kuabudu." Mamia ya watu wanaudhuru unaofanana na huo leo. Je, unafikiri tungeweza kuzungumza kuhusu Towashi kama angetoa udhuru kama baadhi ya watu wanavyofanya leo? Je, unafikiri tungeweza kuwa na mfano wa mazungumzo yake kama hakuwa tayari kwenda kuabudu na kujifunza Maandiko? Je, unafikiri angeweza kukiri Imani yake na kubatizwa kama moyo wake haukufunguka kupokea ujumbe na kusikiliza ujumbe wa Mungu?

Mara nyingi watu wamekuwa na udhuru wa kila aina wa kutokuja kuabudu na kujifunza Biblia. Hata hivyo umewahi kufikiria kuhusu kile unachokosa unapoacha kwenda kuabudu? **Kwanza,** tunakosa fursa ya kumwabudu Bwana. Mungu anataka tumwabudu Yeye (Yohana 4:23). **Pili,** tunakosa fursa ya kuwa na ushirika na Mungu. Filipo na Towashi wasingeweza kuwa na ushirika kama Towashi asingekwenda Yerusalemu. **Tatu**, tunakosa nafasi ya kujifunza zaidi kuhusu Mungu na Maandiko. Towashi alikuwa akisoma Maandiko. **Nne,** tunakosa nafasi ya kuwa mfano kwa wengine kiroho. Towashi alikuwa na uwezo wa kuonesha mfano wake kwa sababu alikuwa tayari kumwabudu Bwana, lakini vipi kuhusu sisi? Ni aina gani ya mfano tunaouonesha katika famila na marafiki tunapoacha kwenda kuabudu? **Tano,** tunakosa nafasi ya kusogea karibu na Mungu. Kama Towashi asingeenda kumwabudu Bwana, asingeweza kufundishwa kile alichokihitaji na kufanyika kuwa Mkristo.

**Je, ni mbali sana tunapokwenda kuabudu wakati dhamiri zetu zinapokuwa na maswali?** Ni nini tunachohitaji ili twende kuabudu na kujifunza Biblia siku ya Jumapili na siku nyingine zilizopangwa na kusanyiko? Kama Towashi alikubali changamoto ya kusafiri kilomita nyingi, wakati wa joto, vumbi na barabara mbaya jangwani kwa kupitia gari la kukokotwa na wanyama hazimkumzuia yeye kwenda kuabudu. Kwa nini sisi tunaruhusu changamoto kututenganisha na ibada na Bwana Mwokozi wetu? Fikiri kuhusu hilo!

# Je, Ni Sahihi Kupiga Makofi Katika Ibada?

**T. Pierce Brown.**

Maswali ya msingi yalikuwepo kuhusu kupiga makofi katika huduma ya ubatizo. Mtu aliyeuliza swali kama hilo inaonekana kuwa kauli yake ni sawa kusema "ameni" mwisho wa sala kwa yule anayeomba na inathibitisha tu kwamba amekubaliana na kile kilichokuwa kikifanyika kwa wakati huo. Kama ilikuwa sawa kushika mkono na kusema "Nimefurahia utii wako," nisingekuwa na sababu ya kupinga hilo. Hata hivyo, inahusisha umuhimu wa sheria zingine.

Acha tuchunguze na kuja na baadhi ya majibu ya Maandiko katika swali hili. Tunaposema "majibu ya Maandiko" hatusemi kwamba tunafahamu moja kwa moja Maandiko yanayoendana na swali, bali kwa kuwa kulikuwa na mfano wa uthibitisho wa waliyofanya Wakristo wa karne ya kwanza, au kulikuwa na amri ambayo ilionesha utaratibu wa hilo, tusingetaka kujadili hii mada. Kama tungepata Maandiko yanayosema kwamba "Tusipige makofi" tusingehitaji kujadii mada hii. Hivyo, lazima tuchunguze kwa upana mada hii katika kanununi za Maandiko na kujitahidi kuwa na majibu yenye maana katika kutekeleza hili. Kwanza acha tutazame dhana ya kupiga makofi, hakuna zaidi ya kuonesha kukubali ujumbe au jambo linaloendelea kama vile "amina," inaweza ikawa hivyo. Wakati hadhira inapopiga makofi na kelele inakubali onesho la Michael Jackson, Je, uthibitisho huu unahusu kitu kile kile kama hadhira itasema "amina?" Maana ya msingi ya neno "Amina" ni "Na iwe hivyo." Kuna tofauti ndogo mbali mbali katika muktadha nyingine, lakini wazo la msingi ni kukubali alichosema mwingine. Kusudi la kupiga makofi katika jamii zetu ni

kuonesha kukubali utendaji wa mtu ikiwa ni pamoja na umahiri na uwezo.

Wakati mtu anapobatizwa kwa usahihi, anamkubali Mungu na anajitoa kwa Mungu. Wakati mtu anapoomba inavyostahili, na kushiriki meza ya Bwana au kuimba isivyostahili ni kitu kile kile, Je, tunapaswa kupiga makofi kwenye kila jambo kila wakati? Kama ndivyo, kwa nini?

Fahamu vitu viwili au vitatu muhimu, kama mwimbaji maarufu ana onesho la mziki na hadhira wanapiga makofi, na kwa kawaida washiriki wanapiga makofi wakati wa onesho. Kuna kitu cho chote katika neno la Mungu kinachopelekea mtu afikiri kuwa wakati mtu anapoongoza nyimbo, sala, au anapohubiri katika Ibada, Je, utendaji wake unahitaji kupigiwa makofi? Je, ni mhubri au utendaji wake ndiyo kiini cha usikivu, au je, usikivu wetu unapaswa uwe katika ujumbe wa Kristo, ambao ujumbe wake tunapaswa kuuendeleza?

Kweli, kama mtu atapiga makofi, wakati mtu mwingine anaongoza sala katika meza ya Bwana na kuondoa kifuniko cha chupa ya tunda la mzabibu, kuna mtu ye yote atapiga makofi kuwa huyu mtu aliongoza sala vizuri sana yenye fanaka ambayo aliweza kuondoa mfuniko bila kubamiza meza au ni kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yetu? Labda makofi ni kwa ajili yao kwa namna walivyojitoa? Hasa ni kwa sababu ulisema “amina” wakati mhubiri anatoa sala, na unakubali kilichokuwa kinaendelea, unakubali kwamba Mungu pia amekubali kilichokuwa kinaendelea. Je, utakuwa tayari kupiga makofi kwa wakati huo? Kama kuna kubishana kuhusu kupiga makofi, itakuwa sawa kusema “amina” wakati bado mnabishana? Kama ungekuwa umesimama chini ya msalaba, wakati Yesu alipokufa na kufahamu kusudi la Yeye kufa, Je, utaweza kukubali dhabihu yake ya upendo? Kama ndivyo, utalikubali hilo kwa kupiga makofi kama askari alivyochoma mkuki ubavuni mwa Bwana wetu? Kama huwezi kuona, kwa nini, haipaswi kuwa vigumu kwako kuona?

Kuna kanuni nyingine zinahusika katika onesho la mwimbaji au mpiga kinanda jukwaani, inapaswa onesho lake kuvuta usikivu ambao ni ustadi au uwezo wa msanii ambaye anaimba. Hivyo, kupiga makofi kunakubalika au kutokupiga makofi kwa namna ulivyotathimini ustadi wake au uwezo wa onesho lake. Hilo si kweli kulingana na tendo la ubatizo, mahubiri, sala, uimbaji katika ibada au kusubiri meza ya Bwana. Kama mtu anapiga makofi katika ubatizo, anaweza kupiga makofi kwa sababu ya ustadi wa mbatizaji aliyebatiza mtu ndani ya maji bila yeye kulowa. Nimewahi kumwona mtu akimbatiza mtu sehemu fulani kwa kumshika shingo kwa mikono yake miwili na kumzamisha ndani ya maji bila kusaidiwa na kumwinua mzima mzima bila kuogopa. Hivyo, naweza kupiga makofi kwa sababu ya ustadi wake wa kubatiza. Maana yangu hapa ni nini? Kupiga makofi wakati wo wote ni kuvuta usikivu wa mtendaji, hata hivyo, tendo linaweza kuwa katika ubatizo, mahubiri, sala, n.k. Tunapaswa kuvuta usikivu kwa rehema na upendo wa Mwokozi wetu aliyeidhinisha hayo, n.k.

Wakati mhubiri anapohubiri na nikasema "amina" sivuti usikivu wa utendaji wa mhubiri, bali katika ujumbe wa Kristo anaouendeleza. Wakati mtu anaposali na nikasema "Amina" sivuti usikivu wa lugha yake nzuri yenye kushawishi na kutaja majina ya watu bali uhalali unaostahili katika kuomba. Kama nikipiga makofi nitakuwa na vuta usikivu wake katika utendaji. Hili halikubaliki na halina nafasi katika mkusanyiko wa kumwabudu Mungu. Wakati mtu anapobatizwa nakubali tendo lake la ubatizo kuwa yupo katika utii wa amri za Bwana, aliyesema, ***"Aaminiye na kubatizwa ataokoka;"*** (Marko 16:16). Pia nakubali tendo la mtu anayebatiza, kama anambatiza kupitia mamlaka ya Kristo, katika njia ya amri za Kristo na kwa kusudi la Kristo jinsi alivyoamuru. Kama kupiga makofi, na hakuna jambo la zaidi ya kusema "amefanya hivyo kwa ajili ya utukufu wa Mungu" sina sababu ya kujitoa katika hilo. Bado tangu hapo neno la Mungu linatuonesha kwamba anataka kutukuzwa kwa njia hiyo, na tangu

hapo kuwa aina hii ya kupiga makofi kila wakati inatumika kuvuta usikivu wa mtendaji kwa kile anachokifanya badala ya Mungu au kwa kusudi la kile alichokiamuru Mungu kutenda, nitajitoa katika hilo.

Kama unafikiri inakubalika kupiga makofi katika ubatizo kwa sababu tu unaonesha kuwa umefurahi au umeshuhudia tendo la ubatizo na bado unafikiria hivyo basi jaribu kutoa jibu lenye maana katika swali hili. Ni wakati gani katika ibada au katika huduma ya Mungu hauhitaji kupiga makofi au kwa kupiga mikono, kwa kuwa umelikubali kila tendo kimaandiko? Je, unapaswa kupiga makofi baada ya kuimba, baada ya mahubiri au baada ya sala, au baada ya meza ya Bwana, au baada ya kusoma neno au muda wo wote na kila unapojisikia una furaha?

**T. Pierce Brown Brown (1923-2008) aliishi na kuhubiri huko Cookeville, Tennessee, Marekani.**

**Ujumbe wa Mhariri:** Zaidi ya hayo kupiga makofi pamoja na kuimba wakati wa kuabudu ni kuongeza kitu kwenye huduma ya uimbaji kitu ambacho hakijaamriwa (Wafeso 5:19, Wakolosai 3:16). Pia, kupiga makofi vyovyote vile katika sehemu ya kukutania inatokea katika mlipuko wa hisia wa kawaida wa papo hapo wa asili ambao ni kinyume na kanuni za ibada na kimaandiko, wakati Mkristo anapoabudu. Hivyo, Ibada yetu inapaswa kuwa katika **"roho"** (mtazamo sahihi na kuwa na hisia za kweli) na **"kweli",** Mamlaka (uhakika) ni kitu ambacho hakibadilishwi na kupuuziwa katika Neno la Mungu.

Amosi 5:23

**"Niondoleeni kelele za nyimbo zenu; kwa maana sitaki kuzisikia sauti za vinanda vyenu."**

Wakolosai 3:17

**"Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye."**

# MITHALI 17:22



Niliamua kuacha kuliita bafu "John" na kulipa jina la "Jim."

Najisikia vizuri sana kusema kwamba nilienda Jim asubuhi hii.



Baadhi ya watu wanaweza kuuliza maswali ambayo yatakufanya utikise kichwa chako kwa mshangao.

Kwa mfano, ndugu huyu aliuliza, "Hivi, Kangaruu anaweza kuruka juu zaidi kuliko nyumba?"

Swali gani hili! Ndiyo bila shaka, Kangaruu anaweza kuruka juu zaidi kuliko nyumba! Kwani umeshawahi kuona nyumba inayoruka?



Tukizungumzia juu ya wazo la pili la kuchagua seheme ya kula. Nilienda katika eneo hili huko Abilene, Texas na nikamwambia mhudumu, "Nina njaa, naweza kula hata falasi." Akatabasamu uku akinipa orodha ya vyakula na kujibu, "Sawa…umekuja katika eneo sahihi."



Meneja mwajili alikuwa akimfanyia usaili msichana mmoja kwa ajili ya nafasi iliyo wazi katika kampuni yake. Akataka kujua jambo fulani kuhusu ufahamu wa msichana, kwa hiyo alimuuliza, "Ikiwa ungeweza kuwa na mazungumzo na mtu fulani, akiwa mzima au amekufa, angekuwa nani?"

Msichana akajibu kwa kujiamini kabisa, "Aliye mzima!"

Nilimwambia mwanangu, “Utamwoa msichana nitakayemchagua.”

Akajibu “Hapana.”

Nikamwambia, “Yeye ni binti wa Bill Gates [Yule tajiri maarufu]”

Akanijibu, “Ndiyo, [nitamwoa]”

Nikampigia simu Bill Gates na kusema, “Nataka binti yako aolewe na kijana wangu.”

Bill Gates akasema, “Hapana.”

Nikamwambia Bill Gates, “Kijana wangu ni Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Dunia.”

Bill Gates akasema, “Sawa, [wataoana]”

Nikampigia simu raisi wa bengi ya dunia na nikamwomba amfanye kijana wangu kuwa Mkurugenzi.

Akanijibu, “Hapana.”

Nikamwambia, “Mwanangu ni mkwe wa Bill Gates,” Akasema, “[Kama ni hivyo] sawa.”

Na hivi ndivyo siasa inavyofanya kazi!

Jamaa mmoja alikodi Taksi ili kutalii mji wa London na alikuwa na haraka. Na walipoufikia Mnara wa London, dereva akamwelezea kuhusu huo Mnara ya kwamba ulianza kujengwa katika mwaka wa 1346 na kukamilika mwaka wa 1412. Jamaa akasema, “Ah! Mnara mdogo kama huo? Kwetu Houston tungeufanya usimame kwa wiki mbili tu!”

Baada ya hapo wakapita kwenye jengo la bunge lililoanza kujengwa mwaka 1544 na kukamilika mwaka 1618. Jamaa akasema, “Tulijenga kubwa zaidi kuliko hilo kwa mwaka mmoja pekee!”

Walipokuwa wakiendelea kupita huko Westminister Abbey dereva alikuwa kimya. “Duh! Jengo gani lile pale?” Aliuliza jamaa. Dereva akajibu, “Sijui, jana halikuwepo.”

# Je! Unapimaje?

Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. Lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe.

Mkilaumiwa kwa ajili ya jina la Kristo ni heri yenu; kwa kuwa Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia. Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji, au mwivi, au mtenda mabaya, au kama mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine. Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo. Kwa maana wakat umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya  Mungu utakuwaje?



**1 Petro 4:12-17**

# Hamasa

Arlis Richardson

Wote tunahitaji kutiwa moyo katika mienendo yetu katika maisha. Wahusika wengi wa Biblia wamepitia matatizo kama hayo ya kukata tamaa ambayo na sisi tunayapitia katika kipindi hiki.

Mtu mmoja amechaguliwa na Mungu kukamilisha kazi kubwa kuliko nyingine yo yote ambayo wanadamu wanaijua. Alikuwa akiwaongoza watu kutoka utumwani, kuwasaidia kuwapanga katika taifa, na kuwapeleka katika ardhi inayotiririka maziwa na asari kwa wingi. Kazi ilikuwa nzuri, lakini Mungu alikuwa pamoja naye. Kwa bahati mbaya, alipata shida, na tunamsoma akishindwa kumpa Mungu sifa. Baadae, aliambiwa kwamba asingeruhusiwa kuingia nchi ile ya ahadi akiwa na wale aliokuwa akiwaongoza. Inahuzunisha kiasi gani kutumia muda wa uhai wa mtu kufanya kazi fulani ili tu ikataliwe kwa sababu ya kushindwa kwa mtu! Bado, hiyo ilikuwa hukumu dhidi ya Musa.

Je, Musa alikata tamaa? Hapana! Alijua ya kuwa kuna kitu bora zaidi baada ya maisha haya kama ataendelea kufanya mapenzi ya Mungu. Kwa hiyo, aliendelea kuwaongoza Israeli kwenda nchi ya ahadi na kukitia moyo kizazi kipya, alikuwa akiwatia moyo hasa warithi. Kabla ya Musa kuondoka katika maisha haya, alisimama mbele ya kizazi hiki kipya cha wana wa Israeli na kusema, ***"Yoshua mwana wa Nuni asimamaye mbele yako ndiye atakayeingia; mtie moyo; kwa kuwa yeye atawarithisha Israeli"*** (Kumbukumbu 1:38). Ni mtazamo mzuri kiasi gani! Ni kwa kiasi gani Yoshua alitiwa moyo kwa kuwa na kiongozi

huyu mkubwa, wakati wa huzuni kuu binafsi, akiwaomba watu aliokuwa akiwaongoza wamtie moyo. Pamoja na kwamba Musa hakuwa na mazishi rasmi ya kibinadamu, alikuwa na viongozi bora wa mazishi ambao hawajawahi kujulikana. ***"Basi Musa, mtumishi wa Bwana akafa huko, katika nchi ya Moabu, kwa neno la Bwana. Akamzika bondeni, katika nchi ya Moabu, kukabili Beth- peori; lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo"*** (Kumbukumbu 34:5-6).

Ni kutiwa moyo kwa aina gani kwetu sisi sote. Pamoja na kwamba tunashindwa, tuna tumaini ikiwa tutaamua kuwa tutakwenda kufanya kazi kwa ajili ya kitu zaidi ya maisha haya. Tunaweza kupoteza vitu vingi katika maisha haya, lakini ahadi za Mungu bado zipo. Tunatiwa moyo kwa msemo, ***"Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi tu maskini kuliko watu wote"*** (1 Wakorintho 15:19). Ni mpangilio mzuri kiasi gani wa mazishi ambao umewekwa kwa ajili ya Musa? Ni vizuri kiasi gani kujua kuwa Mungu atajali vitu kwa wakati unaostahili.

Wakati mwingine mizigo ya kuchanganyikiwa inaonekana kutuzidi. Bado, hatuhitaji kujijali wenyewe wakati tunapowatia moyo wengine. Ni vizuri kiasi gani kutiwa moyo kunatokea kusikojulikana.

**Aris Richardson amekuwa mhubiri wa kanisa la Kristo kwa miongo huko Marekani na sasa amestaafu.**

**II Mambo ya Nyakati 35:2**

"Akawasimamisha makuhani katika malinzi yao, **akawatia moyo** kufanya utumishi wa nyumba ya Bwana."

**Matendo 13:43**

"Sinagogi ilipofumukana, Wayahudi na waongofu watauwa wengi wakashikamana na Paulo na Barnaba; ambao, wakisema nao, **wakawatia moyo** kudumu katika neema ya Mungu."

# Mambo Ya Kila Siku

Derek Broome



Unapoamka asubuhi, ni kitu gani cha kwanza huwa unakifanya? Kuoga? Kupata kifungua kinywa? Kupiga mswaki? Watu wengi wana utaratibu wanaoufuata kila siku, isipokuwa matukio kama sikukuu na mwisho wa wiki. Sasa kwa baadhi ya watu utaratibu wao ni wa afya na wenye tija. Wametafuta njia bora zaidi za kujishawishi wenyewe kila siku na kutumia utaratibu wao ili wafikie tija ya juu. Bado, kwa wengine, utaratibu wao ni wa hatari, uvivu na kuzalisha nguvu za kutosha kupata kwa shida. Tunapoangalia mbinu hizi mbili tofauti katika maisha, labda tunaweza kutambua mabadiliko tunayohitaji kufanya katika maisha yetu ya kiroho?

Katika Mathayo 23, watoza ushuru na Mafarisayo waliishi maisha yao kwa namna waliyotaka wao. Walikuwa wakiwaambia watu waishi njia hii na wao wakiishi njia ile waliyokuwa wakitaka wao. Walikuwa wakijifanya wao waonekane wema kwa nje wakati kwa ndani walikuwa wamejaa rushwa. Walikuwa wakishika sehemu ya sheria wakati walikuwa wakisahau sehemu nyingine. Katika Mathayo 23:27-28, Yesu aliendelea kuchunguza maisha yao na alisema walijaa unafiki na uasi. Ni dhahiri, maisha yao yalikuwa hayampendezi Mungu.

**Ni lazima Kristo awe kitovu cha maisha yetu, na kama watu wake watakatifu, tunapaswa kujitahidi kufanya mapenzi yake kila siku.**

Vipi kuhusu maisha yetu ya kiroho? Je, tunaishi kama watoza ushuru na Mafarisayo? Je, tumejaa unafiki na uasi? Wakristo wengi leo wamekumbwa na wimbi baya la kutokumuishia Yesu. Kwa wengi, siku yenye mafanikio kama Mkristo haimaanishi kutokujua jambo lo lote baya. Tunakuwa na utaratibu wa kuamka kila siku, bila kufanya dhambi yo yote watu watatuita na kwenda kulala wakijisikia vizuri wakiridhika kila usiku. Tunakwenda kwenye madarasa ya Biblia na ibada kila wiki, tunakaa kwenye viti vyetu vya kawaida, tukiimba, tukisali na kushiriki meza ya Bwana. Mwishowe tunajihisi tunafanya sahihi. Hata hivyo, vipi kuhusu kuishi kwa ajili ya Yesu?

Ninaamini wote tunaweza kutambua maeneo katika maisha yetu ya kiroho ambayo yanahitaji mabadiliko, lakini tunatakiwa kutaka kubadilika kwa ajili ya Bwana. **Kristo lazima awe kitovu cha maisha yetu, na kama watu wake watakatifu, tunapaswa kujitahidi kufanya mapenzi yake.**

**Derek Broome ni mhubiri mshirika katika kanisa la Kristo Siwell Road huko Jackson, Mississippi, Marekani.**



# Alexander Mwenye Hasira

Bill Dillon

Alexander Mkuu alikuwa ni mmojawapo wa watu washindi katika historia. Hakushinda tu Ugiriki bali Misri na Uajemi pia. Pia alisafiri mpaka India ya mbali. Katika umri wa miaka 33, alikuwa ni kiongozi asiye mbishi. Ingawa Alexander alitawala ulimwengu, hakuweza kujishinda yeye mwenyewe.

Rafiki mkubwa wa Alexander alikuwa Kletus. Walicheza na kukua pamoja katika utoto wao. Zaidi ya hayo, walipigana pamoja katika vita mbalimbali na kampeni. Zaidi sana, katika tukio moja Kletus alikuwa ameokoa maisha ya Alexander kishujaa.

Katika kipindi fulani ambacho akikuwa na ulinzi kwenye karamu ya pombe, Kletus alimwudhi Alexander kwa maneno yasiyofaa. Alexander alikasirika na kuchukua mkuki na kumrushia Kletus na Kletus alikufa pale pale. Alexander alilia kwa uchungu na kujutia, lakini hata Alexander Mkuu hakuweza kumrudishia uhai mtu aliyekufa. Alexander aliushinda ulimwengu, lakini hakuweza kujidhibiti mwenyewe. Aliweza kuamuru kikosi, lakini alishindwa kuzizuia hisia zake. Aliweza kulinidhamisha jeshi, lakini alishindwa kunidhamisha hasira zake.

Hakuna kifungo cha mapenzi au urafiki wenye nguvu kuweza kuwashikanisha marafiki pamoja mbele za walevi na hisia za hasira.

Inahuzunisha kwamba Alexander Mkuu hakujifunza ukweli uliotawala wa Mithali 16:32 unaosema, ***"Asiye mwepesi wa hasira ni mwema kuliko shujaa, na mtu aitawalaye roho yake kuliko mtu atawalaye mji."***

**Bill Dillion ni mhubiri wa kanisa la Bwana huko Cotter, Arkansas, Marekani.**

# Fursa Ya Maombi

Jack W. Carter

**Sala** kwa kweli **ni fursa.** Ni ahadi kwa waaminifu wa Mungu. Ni uhakika si tu kwamba Mungu anawaangalia watoto wake tu, bali huwasikiliza pia.

Sala si ahadi kwa mtu ye yote tu. Vifungu vingi vya Maandiko vinazungumzia jinsi maombi ya mwenye dhambi, muasi na mvivu hayasikilizwi. Mungu anasema kuwa hayapenyi katika mawingu, ni machukizo kwake na pia majanga yanapokuja hatawasikia.

Wengi wana wakati mgumu kulikubali hili. Mungu ni Mungu wa upendo, sawa? Sisi ni watoto wake, ingawa hatumtumikii vyema, sawa? Hakika hawezi kugeuza sikio lisilosikia hata kwa ubaya tulio nao tunapolia katika dhiki, sawa?

Na tumruhusu Mungu wetu atujibie maswali haya.

***"Kwa kuwa nimeita, nanyi mkakataa; Nimeunyosha mkono wangu, asiangalie mtu. Bali mmebatilisha shauri langu, wala hamkutaka maonyo yangu. Mimi nami nitacheka siku ya msiba wenu; nitadhihaki hofu yenu ifikapo; hofu yenu ifikapo kama tufani, na msiba wenu ufikapo kama kisulisuli, dhiki na taabu zitakapowafikia. Ndipo watakaponiita, lakini sitaitika; watanitafuta kwa bidii wasinione. Kwa kuwa walichukia maarifa, wala hawakuchagua kumcha Bwana. Hawakukubali mashauri yangu, wakayadharau maonyo yangu yote. Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao, watashiba mashauri yao wenyewe."*** (Mithali 1:24-31).

Kama hili ni onyo kwa wasio haki, pia ni kiapo kwa waaminifu. Majanga yanapokuja, Mungu atasikia! Si kwamba Mungu atasikia tu, pia atatenda.

Tena na tena hili limehakikishwa. Tena na tena wenye haki watabadilisha mwenendo wa tukio kupitia sala.

# Sifa Za Nyumba Nzuri

**Mithali 31:10-31**

**Jimmy Clark**

***"Mke mwema, ni nani awezaye kumwona? Maana kima chake chapita kima cha marijani"*** (Mithali 31:10). Kifungu hiki, pamoja na mistari inayofuata hadi mwisho wa sura hii inamwelezea mwanamke mwema. Hata hivyo, kuna watu wengi wametajwa kuliko huyu mwanamke katika sehemu hii. Kuna mume wake (Mithali 31:11, 23, 28). Kuna watoto wake (Mithali 31:28). Kuna watumishi wake wa nyumbani (Mithali 31:15). Mengi ya yaliyomo katika sehemu hii yanatoa ufahamu wa sifa za nyumba nzuri.

**#1 UAMINIFU**

***"Moyo wa mumewe humwamini, wala hatakosa kupata mapato. Humtendea mema wala si mabaya, siku zote za maisha yake"*** (Mithali 31:11-12). Kanuni ya msingi ya ndoa yenye mafanikio na nyumba iko kwenye neno "uaminifu." Ujasiri mkubwa katika uaminifu wa maneno ya viapo ambayo yanawekwa katika siku ambayo wawili wanakuwa kitu kimoja. Kuwa na imani kwa mwingine wakiwa mbali mbali ni amani ambayo kila mmoja anapaswa kujua. Hata hivyo, inasikitisha kumwona mume ambaye anadhibiti na kutilia shaka kila neno na hatua ya mke wake. Vile vile uharibifu huja kwa uchunguzi wa mke katika kila tendo la mume wake ili aone kama ni mkweli na mwaminifu katika ndoa. Shughuli kama hizo kwa wote ni za kukasirisha na kuchukiza. Uaminifu unaruhusu kila mmoja kuwa mbali na mwenzi wake katika shughuli tofauti za siku na hata kujua kwamba kila mmoja anafanya kazi kwa lengo maalum: maisha yenye furaha na tija kwa pamoja.

## #2 TAABU

***"Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake; wala hali chakula cha uvivu"*** (Mithali 31:27). Sehemu hii imejaa maneno ya kazi za kuzalisha. Kuna maneno *"hutafuta"* na "hufanya kazi kwa moyo" (Mithali 31:13). Kuna maneno *"hupanda mizabibu"* (Mithali 31:16). Mwonekano wa kawaida wa maisha ya mwanamke huyu ungeonesha kwamba hakuwa na muda wa kukaa kivivu kwa uzalishaji wote anaoutoa. Anashughulikia mahitaji ya sasa na kujiandaa kwa mahitaji ya baadae. Mwisho wa sehemu hii inamzungumzia, ***"Mpe mapato ya mikono yake; na matendo yake yamsifu malangoni"*** (Mithali 31:31). Ikiwa wote watafanya kazi kwa faida ya nyumbani mwao, nyumba nzuri inazalishwa. Kujenga nyumba kunahusisha nguvu nyingi (Mithali 14:1).

## #3 HURUMA

Hakuna nyumba nzuri ambapo huruma haipo. Imesemwa kwa huyu mwanamke mwema, ***"Hufumbua kinywa chake kwa hekima. Na sheria ya wema i katika ulimi wake"*** (Mithali 31:26). Anawahurumia wale wasiobahatika walio nje ya nyumba yake (Mithali 31:20). Kuonesha rehema na ukarimu ni kuwa karibu na sifa za Mungu mwenyewe (Tito 3:4-5). Upendo na huruma vinapaswa kutafutwa sana kuliko utajiri wa vitu. Sulemani aliandika mahali pengine katika Mithali, ***"Chakula cha mboga kwenye mapendano; ni bora kuliko ng'ombe aliyenona pamoja na kuchukiana"*** *(Mithali 15:17).* ***"Afadhali mego kavu pamoja na utulivu; kuliko nyumba yenye karamu nyingi pamoja na magomvi"*** (Mithali 17:1). Mungu huwaunganisha wawili pamoja katika ndoa (Mathayo 19:6) na ***"Ametuita katika amani"*** (1 Wakorintho 7:15). Kwa kuwa Bwana alifanya nyumba kuwa baraka kwa mwanadamu, lazima tujue kwamba Bwana anajua lililo bora kwetu. Laiti kila nyumba ingekuwa ladha ya Mbinguni Duniani.

**Jimmy Clark ni mhubiri wa kanisa la Kristo Bethel huko Athens, Alabama, Marekani.**

# JINSI YA KUBORESHA HALI YA KIROHO YA FAMILIA YAKO

Ken Tyler

Katika ulimwengu wenye shughuli nyingi, ni rahisi kupoteza mwelekeo wetu. Kwa mfano, wazazi wengi wanawakimbiza watoto wao katika shughuli za michezo mmoja baada ya mwingine. Inaonekana kuwa na muda mdogo kwa ajili ya vitu vingine. Inachukua jitihada maalum kudumisha na kuboresha hali zetu za kiroho. Nataka kutoa baadhi ya njia rahisi za kukusaidia kuboresha hali ya kiroho ya familia yako.

1. **Inaanza na shauku.** Ni lazima utake kuboresha hali ya kiroho ya familia yako.
2. **Ombeni pamoja katika mlo.** Maarifa ambayo unatambua kwamba baraka zako zinatoka kwa Mungu na kwamba unashukuru kwa ajili ya baraka hizo (Yakobo 1:17). Pamoja na mlo wao ukiwa hotelini usisahau kuomba.
3. **Ikusanye familia yako pamoja kwa ajili ya kusoma Biblia na kusali kabla ya kwenda kulala.** (2 Timotheo 3:15). Hii itawaweka karibu kwa kila mmoja wenu na karibu na Mungu. Kama siku imekuwa ngumu, itaipa familia yako amani inayohitaji.
4. **Kama familia, nendeni, tembeleeni na mumsaidie mtu mwenye hitaji maalum** (Wagalatia 6:10). Unaponyanyua mzigo wa mtu, familia yako itatambua baraka za utumishi. Watoto wetu sasa wamekuwa, na ninaona sasa tabia ya kujali kwa wengine kwa kuwa tulifanya hivi kadri walipokuwa wanakua.

Kuboresha hali ya kiroho ya familia yako ni lazima kiwe kipaumbele cha juu. Muda wetu kweli ni mdogo inapofikia kuhusu watoto wetu. Ninakusihi uchunguze mwelekeo na shauku yako, halafu kuwa na shughuli nyingi.

# *NENO KWA WAKE*

**Dalton Key**

Socrates alisumbuliwa na mke msumbufu ambaye mara nyingi alikuwa akimpiga ulimi kisha kummwagia maji baridi kichwani mwake. Mwanafilosofia anaelezea tabia kama hiyo kwa kusema, “Baada ya dhoruba, mvua.”

Tulipouliza kwa nini alimuoa Zantipa, Socrates alijibu, “Wale wanaotaka kuendesha vizuri farasi mwenye utulivu kwa sababu, ikiwa atayaweza haya, atayaweza mengine. Nataka kujifunza kushiriki na wanadamu wote, na nimemchagua Zantipa, nikijua kuwa ikiwa nitaiweza jamii yake, nitaweza kuwa na kila mtu.” Socrates anaweza kuwa amechukua zaidi ya kile anachoweza kushughulikia!

Inasemekana Abraham Lincoln alikufa kifo cha taratibu na chenye hisia kabla ya Booth kuvuta kifyatulio kwenye ukumbi wa michezo wa Ford. Inasemekana mke wake alikuwa akimpinga na kulalamika kiasi kwamba Lincoln hakuweza kufanya cho chote machoni pake. Alipochaguliwa kugombea uraisi, alisimama kutoka alipokuwa amekaa, akachukua kofia mkononi mwake na kusema kimya kimya, “Ninataka kushiriki hili na mwanamke ambaye ananipenda……. Mama yangu.”

Hapana, wake wote si mzigo mzito. Wake wengi wa Kikiristo ni wema, wazuri na wasaidizi wazuri kwa waume zao (Mwanzo 31:10). Sulemani alikuwa na wake wema akilini mwake alipoandika, ***“Mke mwema ni nani awezaye kumwona? Maana kima chake chapita kima cha marijani”*** (Mithali 31”10). Je, wewe ni mke wa aina gani?

**Dalton Key ni mhariri [wa jarida la] Mapito ya Kale na mhubiri wa kusanyiko la Rockford huko Tulsa, Oklahoma, Marekani.**

# Sifa Sita za Uongozi Bora

Neal Pollard

Katika Kumbukumbu la Torati, Musa ameanza kwa kuonesha matukio ya miaka arobani iliyopita-yaliyotokea na kusababisha kuzunguka jangwani na mambo yalitokea walipokuwa huko. Katikati mwa sura ya kwanza, anazungumza kuhusu wakati alipokuwa akifanya kazi kwa baba mkwe. Yethro alikuwa na mipango ya kutatua matatizo kadhaa ambayo yaliukuwa yakija kutoka kwa Waisraeli. Aliwaita baadhi ya wanaume "waamuzi" akawaandaa wanaume pamoja na wanawake ambao watachukua nafasi hizo na kuwaleta watu na kuanzisha vizazi baada ya Musa, ambaye ana sifa tunazozihitaji (Kumbukumbu la Torati 1:15-17) inasema, ***maakida ya elfu elfu, na maakida ya mia mia, na maakida ya hamsini hamsini, na maakida ya kumi kumi, na wenye amri, kwa kadiri ya kabila zenu. Nikawaagiza wakati ule waamuzi wenu, nikawaambia, Sikizeni ninyi maneno kati ya ndugu zenu, mkaamue kwa haki kati ya mtu na nduguye, na mgeni aliye pamoja naye. Msitazame nafsi za watu katika hukumu; muwasikilize wadogo na wakubwa sawasawa; msicheke uso wa mtu awaye yote; kwa kuwa hukumu ni ya Mungu; na lile neno liwashindalo mniletee mimi, nami nitalisikiza."***

**Walipaswa kuwa na hekima.** Aya ya kumi na tatu inaongeza pia "wenye akili na ufahamu maarifa ni msingi wa chini ya hekima" na akili ni kuwa na uwezo wa kuitumia hekima. Kutatua matatizo, na kutatua matatizo walihitaji hekima.

**Walipaswa kuwa na uzoefu wa kutokuwa na woga.** Walipaswa kuthibitisha uwezo wao wa kufanya maamuzi na kutambua hali au matatizo magumu.

**Walipaswa kufanya maamuzi ya haki.** Katika ugomvi kila mtu hufikiri kuwa yupo sahihi na mwingine ndiye mwenye makosa. Ni kwa jinsi gani hawa viongozi walikuwa wakiamua? Kwa kufanya akili na hisia zao kutoka katika mtazamo hasi na kuweza kufanya maamuzi na kutatua tatizo vizuri zaidi.

**Walipaswa kuwa waadilifu.** Upendeleo ulikuwa sawa na uhalifu. Ugomvi ulikuwa ukitatuliwa kwa haki ya juu sana.

**Hawakupaswa kukataa tatizo dogo au kubwa.** Walikuwa wakishughulikia tatizo kubwa au dogo sawa, kama lilikuwa ndani ya uwezo wao. Kama tatizo lilikuwa kubwa sana kwao walikuwa wakimwita Musa, makubwa yalikuwa yanawekwa wazi kwao hata yangekuwa madogo ya dhihaka yalikuwa yanaonekana ya muhimu kutatua. Wale waliokuwa wakipitia matatizo makubwa walikuwa wakiwasaidia vile vile na wale wenye matatizo madogo bila shaka nao walikuwa wakisaidiwa kwa jinsi walivyoliona katika macho yao.

**Walikuwa hawamwogopi mtu ye yote.** Walikuwa wanaweza kukabiliana na vitisho, waonevu, watoaji rushwa na kufukuza wasiostahili. Hata hivyo, Mungu kupitia Musa aliwapa wasio na sifa kuwa na sifa za kusimama imara bila woga katika hali yo yote.

Mfumo huu uliwekwa na Mungu baada tu ya kutoka Misri na kabla ya safari ya jangwani hauko sambamba moja kwa moja na mfumo wa uongozi wa Mungu leo. Hata hivyo, kifungu hiki kinaonesha taratibu na kanununi walizotumia. Sifa hizi ni zile zile zitakazomsaidia kiongozi wa Mungu kuwa kiongozi bora leo. “Ekklesia” ni neno la Kiyunani lenye maana ya “Kanisa”, katika Agano Jipya neno hili limetajwa mara 115 hasa katika kitabu cha Matendo.

**Neal Pollard ni mhubiri wa kanisa lililoko Bear Valley huko Denver, Colorado, Marekani.**

***“Basi nikatwaa vichwa vya kabila zenu wenye akili, waliojulikana, nikawafanya wawe vichwa juu yenu,..”***

# Msaka Tonge

**Waefeso**

**Rebecca Rusmore**

**( Jibu maswali yote)**

1. Ni wakati gani Mungu atakusanya pamoja kila kitu kwa Kristo?
2. Nani ni jiwe kuu la pembeni?
3. Ni akina nani warithi pamoja na Wayahudi?
4. Ni kwa jinsi gani Kristo anakaa ndani yetu?
5. Taja majina saba yaliyoorodheshwa katika sura ya 4.
6. Kwa nini tunawasamehe wengine?
7. Je, Kanisa linapaswa kumtii nani?
8. Je, imani inafananishwa na kifaa gani cha kujilinda?
9. Neno la Mungu linalinganishwa na silaha gani?
10. Ni nani Paulo aliyemtuma Efeso kuwajulisha jinsi anavyoendelea?

# Watu Waliosahaulika Katika Biblia: Yethro

**Rebecca Rusmore;**


Tunafahamu mambo mengi sana kuhusu watu mbalimbali katika Biblia. Na watu kama hao mara nyingi wamekuwa somo kwetu kujifunza na wakati mwingine tunapata habari zao katika sura moja au katika kitabu, na somo tunaloweza kujifunza kwao. Kuna watu waliotajwa kwenye Biblia ambao tunawafahamu kwa sehemu ndogo. Hawa watu wanaweza kuwa wametajwa katika kifungu cha Maandiko au wanapatikana katika sehemu moja au mbili katika Biblia. Hawa watu wanatazamwa zaidi. Hata hivyo, wametajwa kwa kusudi fulani.

Yohana 20:30-31 Maandiko yanatuaambia kuwa kuna mambo mengi aliyofanya Yesu ambayo hayakuandikwa katika Biblia. Haya mambo yaliyoandikwa ni kwa ajili ya kuimarisha Imani yetu. (2Timotheo 3:16-17). Maandiko yanatuambia kwamba kila kitu katika Biblia kinatoka kwa Mungu na ni kwa ajili yetu kujifunza. Kwa ufahamu huu, bila shaka kwa haya machache tunayofahamu, watu waliosahaulika wanaume na wanawake katika Biblia wanaweza kutufundisha somo lenye thamani leo.

Katika Agano la Kale tunasoma habari za watu wengi ambao Mungu aliwatazama kuwa ni watu wenye Imani kubwa (Waebrania 11). Miongoni mwa hao watu ni Musa ambaye alishauriwa na mtu ambaye si Mwisraeli. Ni nani angemkubali na kumpa sheria atoe kwa watu na kuitwa na Mungu? Jibu ni Yethro baba mkwe wa Musa. Kwa mara ya kwanza huyu mtu ametajwa katika kitabu cha Kutoka 2:16-21. Hapa tunaona Musa akikimbia Misri kwa ghadhabu ya Farao na

kwenda nchi ya Midiani. Katika kisima Musa aliwasaidia mabinti saba wa kuhani wa Midiani. Baba yao Reueli alimkaribisha Musa kuwa mgeni wao na baadaye akampa Musa binti yake mmoja kuwa mke wake. Sehemu nyingine tunayosoma habari za baba mkwe wake Musa ni Kutoka 3:1 pale anapomwita Yethro. Na vifungu vingine vya huyu mtu ni katika kitabu cha kutoka ambacho kinamtaja kama Yethro.

Tunajifunza nini kutoka kwa huyu kuhani wa nchi ya kigeni ambaye alimshauri mtu wa Mungu? Kwanza Yethro alikuwa mkarimu. Wakati Musa alipowasaidia mabinti wa Yethro, walirudi kwa baba yao bila kuwa na Musa. Baba yao alihitaji kumfahamu huyu mtu aliyewasaidia na kuwatuma mabinti zake warudi wakamlete Musa ili waweze kupata chakula kwa pamoja



(Kutoka 2:20). Katika Kutoka 3:1 tunaona kwamba Musa alifanya kazi kwa Yethro ya kuchunga kondoo. Yethro kwa haraka alimpa mgeni chakula na malazi. Hata sisi pia tunawasaidia wengine kwa kuonesha ukarimu wetu (1Petro 4:9).

Yethro alikuwa ni mtu wa kuwaheshimu wengine. Katika Kutoka 18:1-8 tunasoma jinsi Yethro alivyomletea Musa mkewe na wanawe baada ya kuondoka Misri.***"Basi Musa akatoka nje ili amlaki mkwewe, akasujudia na kumbusu; nao wakaulizana habari; kisha wakaingia hemani"*** (Kutoka 18:7). Musa anaonesha kwamba Yethro alikuwa na

heshimama. Sisi kama Wakristo tunaelekezwa kuwa na mwenendo mzuri ili wengine watuheshimu na kumtukuza Mungu ***"Mwe na mwenendo mzuri kati ya mataifa, ili iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa"*** (1 Petro 2:12).

Pia Yethro alikuwa ni mtu mwenye furaha na watu wa Mungu. Alitoa dhabihu kwa Mungu na vitu vyake, mambo mazuri aliyofanya na kutoa ushauri mzuri kwa mkwe wake. Baada ya Musa na Yethro kuwa katika matukio kila mmoja aliondoka kwa furaha. Yethro alifurahi kuwa Mungu amefanya mambo ya ajabu kuwatoa watu wake utumwani. Kutoka 18:9-11 panasema: ***"Yethro alifurahi kwa ajili ya wema wote Bwana aliowatendea Israeli, kwa alivyowaokoa mikononi mwa Wamisri. Kisha Yethro akasema, na ahimidiwe Bwana aliyewaokoa na mikono ya Wamisri, na mkono wa Farao; aliyewaokoa watu hao watoke mikononi mwa Wamisri. Sasa najua ya kuwa Bwana ni mkuu kuliko miungu yote; naam, katika jambo hilo walilowatenda kwa unyeti."***

Hatimaye Yethro anamtukuza Mungu, alitoa dhabihu za kuteketezwa kwa Mungu. Haruni, Musa na wazee wengine wa Israeli waliungana na Yethro katika kupata chakula kufuatana na dhabihu, tena walionesha heshima kwa kuwa na mtu wa kigeni (Kutoka 18:12). Hata sisi pia hatupaswi kusahau mambo ambayo Mungu amefanya kwetu. Maisha yetu lazima yawe ni maisha yenye shukrani kwa Mungu (Wakolosai 2:7,3:17), na kuwa tayari kuabudu pamoja na watu wa Mungu (Waebrani 10:25).

Katika siku ya pili katika kambi ya wana wa Israeli, Yethro anamtazama Musa alivyokuwa muamuzi kwa watu waliokuwa wakija kwake kwa ajili ya kupata msaada, baadaye akampa Musa ushauri. Yethro aliona kuwa Musa amezidiwa na watu wenye mahitaji. Alikuwa na hofu kwa ajili ya Musa na watu wangeweza kuchanganyikiwa kwa hatua walizokuwa wakipitia na kumfanya Musa kuwa mwamuzi wa

matatizo yao yote. Kwa ufahamu huo, Yethro alimpa Musa ushauri. Alipendekeza kuwa Musa achague watu wenye uwezo awafundishe kuwa waamuzi katika matatizo madogo ili kwamba Musa aweze kushughulikia matatizo makubwa (Kutoka 18:13-22). Si hilo tu alilolifanya Yethro, pia alimpa ushauri, alitambua kuwa Musa alipaswa kupeleka matatizo kwa Mungu kabla ya kutumia ushauri wake. ***"Kwamba utafanya jambo hili, na Mungu akikuagiza hivyo, basi utaweza kusimama wewe, na watu hawa wote nao watakwenda mahali pao kwa amani."*** (Kutoka 18:23). Huyu mtu alikuwa na uwezo wa kuona tatizo na utatuzi wa tatizo hilo wakati huo akijua kuwa Mungu ndiye mwenye mamlaka yote. Sisi pia tunahitaji ushauri wakati mambo yanapokuwa magumu katika maisha haya. (Mathayo11:29-30, Wafilipi 4:6).

Kweli Yethro alikuwa mtu wa kuheshimiwa. Alieshimiwa na watu wengine na kuonesha tabia njema kwa Mungu na watu wake. Huyu mtu aliyesahaulika katika Biblia alijifunza kufurahi na watu wengine katika furaha yao na kutafuta ushauri wa Mungu katika kila jambo maishani. Itakuwa vizuri kama tukiwa mfano mzuri wa sifa hizi nzuri.

**Rebecca Rushmore ni mwandishi katika jarida la Sauti ya Kweli Kimataifa na ni mwalimu wa shule. Anaishi huko Cllierville, Tennessee, Marekani.**

## Una Lipi La Kufanya Ukumbukwe?

Shadrack S. Msambaza

Nehemia 13:14,22,31. ***"Unikumbukie hayo, Ee Mungu wangu, wala usifute fadhili zangu nilizozitenda kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu, na kwa taratibu zake. Kisha nikawaamuru Walawi wajitakase, nao waje kuyalinda malango, ili kuitakasa siku ya sabato. Unikumbukie hayo nayo, Ee Mungu wangu, ukaniachilie sawasawa na wingi wa rehema zako. na matoleo ya kuni nyakati zilizoamriwa, na malimbuko. Nikumbuke, Ee Mungu wangu, ili unitendee mema."***

Nehemia 5:19 ***"Unikumbukie, Ee Mungu wangu, kwa mema, yote niliyowafanyia watu hawa."***

# Sababu za Kuwa na Furaha katika Majaribu

**Gary C.Hampton**

Kila mtu hupitia majaribu katika maisha. Kutoka katika mtazamo wa mwanadamu ni ngumu kuchukulia kama kitu cha kawaida bali ni maumivu. Hata hivyo, Yakobo amefungua waraka wake kwa kutafakari sababu za kuwa na furaha katika majaribu. Kabla ya kutazama sababu, itakuwa vizuri kufahamu kuwa Yakobo aliokuwa akiwaandikia. Yakobo aliwaandikia watu wa Mungu waliokuwa wametawanyika.

Kuna watu wanne wanaoitwa Yakobo katika Agano Jipya. Anaweza akawa ni Baba yake Yuda alifahamika sana, angeweza kuandika waraka huu na kuuita kwa jina lake (Luka 6:16, Matendo 1:13). Mwingine mbali na baadhi ya taarifa kuhusu familia yake, tunajua kidogo kuhusu Yakobo mwana wa Alfayo (Matendo 1:13, Luka 16:5, Marko 3:18, Mathayo 10:32). Hivyo, haiwezekani kuwa ndiye mwandishi wa waraka huu. Yakobo mwana wa Zebedayo na ndugu wa Yohana alifahamika vizuri lakini aliuawa na Herode kati ya mwaka 44 B.K (Baada ya Kristo}. Hivyo tunahitimisha kuwa Yakobo ndugu wa Bwana wetu ndiye mwandishi wa waraka huu. (Mathayo13:55, Marko 6:3). Ndugu yake Kristo ambaye hakumwamini Yesu katika huduma yake mwanzoni (Yohana7:1-5, Marko 3:31-35). Hata hivyo, baada ya kufufuka kwake Yesu, ndugu zake walikuwa chumba cha juu ghorofani wakiomba pamoja na mitume (Matendo 1:12-14). Ufufuko wake uliwashawishi kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu (1 Wakorintho 15:7).

Katika salamu yake, Yakobo amechagua neno la salamu lilimaanisha “furaha kwenu.” Aliendelea kuwaambia wasomaji wake kuwa wanapaswa kuwa na furaha hata katika hali yo yote ngumu na

majaribu (Yakobo 1:2). Hii si furaha ya kuigiza bali furaha ya kweli kwa sababu ya matokeo ya kushinda majaribu ambayo yatakuwa ni matokeo ya kupokea ahadi (Waebrania 10:32-39). Yesu anasema ***"Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu."*** (Mathayo 5:1-12).

Robertson alisisitiza kuwa mtu anapoangukia katika majaribu bila kudhamiria "hakutegemea" na hana kosa katika majaribu anayopitia ni ni kama mtu aliyeangukia katika kundi la wezi (Luka 10:30). Angalia, Yakobo alijua kuwa majaribu yatakuja. **Kufanyika kuwa Mkristo haimanishi kuwa umejikinga na matatizo ya maisha.** Yesu aliwaambia wanafunzi wake ***"Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu."*** (Yohana 16:33). Karibu na mwisho wa safari ya kwanza ya Paulo ya umisheni, Paulo alienda katika makusanyiko na kufanya kazi ya kuwaimarisha ndugu katika imani. Alisema ***"Wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile Imani, na ya kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi."*** (Matendo 14:22). Pia Petro aliwaambia ndugu kuwa wasishangae pale wanapopitia majaribu. Kwani aliwasihi wafurahi kwa sababu wamethibitisha thamani yao ya kuteseka kwa ajili ya Bwana.

Sababu ya kufurahi unapokuwa katika majaribu ni, huleta saburi [ustahimilivu] (Yakobo 1:3). Neno "kujaribiwa" hapa limefafanuliwa kama kukosa mahitaji, au kuwa na changamoto za kifedha au uchumi (1 Petro 1:6-7). Haya ni kama majaribu ya kuthibitisha usafi au uimara wa Imani (Mwanzo 22:1-14). Majaribu kama haya yanatengeneza ubora wa kushinda majaribu mengine, ni kama kuwa na uzoefu wa kukimbia mbio ndefu. Zaidi ya hapo uvumilivu utakufanya kuvumilia hadi mwisho, hakika mtu wa Mungu atakuwa amekuwa katika Imani

yake (Yakobo 1:4). Guy N. Woods alisema kuhusu maneno haya, “Hujakosa cho chote,” “kimsingi neno hilo linaonesha ukweli kwamba **wale ambao wanaendelea kuwa Wakristo wakomavu hawajaachwa na ye yote**.”

**Gary C. Hampton ni mhubiri wa kusanyiko la Siwell Road huko Jackson, Mississippi, Marekani.**

# Sarafu za Kenney

Kwa Mungu wokovu wangu, na utukufu wangu; Mwamba wa nguvu zangu, Na kimbilio langu ni kwa Mungu (Zaburi 62:7). Ni huzuni kiasi gani wakati mtu anapoamua kuacha Imani na kwenda zake mbali na Bwana au Kanisa lake? Nani ataweza kuwasaidia watu kutoka katika utumwa wa dhambi? Ni nini Kilichotokea katika mapigo yao? Shukurani zangu kwa Mungu ambaye hakutuweka rehani wala kutuacha.

Luka 10:17,20.***“Ndipo wale sabini waliporudi kwa furaha, wakisema, Bwana, hata pepo wanatutii kwa jina lako…Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni.”***

**Fungu hilo la Maandiko linatufundisha mambo mawili ya msingi:**

(1) Kile wakati fulani tunachodhani kuwa kinastahili furaha yetu yote kumbe kwa uhalisia sivyo, bali jambo linalostahili furaha yetu yote ni majina yetu kuandikwa Mbinguni.

(2) Yesu aliwahakikishia wanafunzi wake hao kuwa majina yao yalikuwa yameandikwa Mbinguni. Hivyo, na sisi, tukiwa wanafunzi wake halisi na waaminifu, tunaweza kuwa na uhakika kuwa majina yetu yameandikwa Mbinguni. Je, hii ni furaha iliyoje?

**Shadrack S. Msambaza**

# Mkristo Ni Nani?

**Maxie B.Boren.**

Kuna mkanganyiko wa kuzingatiwa kwenye akili za wengi juu ya kile kinachomfanya mtu kuwa Mkristo. Watu wengi wanadhani kwamba mtu ye yote anayekiri kumwamini Kristo kwa kiwango cho chote, au anayedai kuwa ni Mkristo, basi ni Mkristo. Je, hilo ni kweli? Hakuna mengine zaidi yanayohusika zaidi ya hivyo?

Biblia inafundisha kuwa Injili ya Kristo ni uweza wa Mungu uletao wokovu (Warumi 1:16). Ili mtu aweze kuwa Mkristo, si lazima asikie tu na kuamini Injili, bali lazima atii Injili! Tazama Kristo mwenyewe alichosema. *"**Aaminiye** (Injili) **na kubatizwa ataokoka**"* (Marko 16:16). Angalia hilo katika sura ya 6 katika kitabu cha Warumi Wakristo walikuwa huru kutoka katika dhambi wakati walipotii mafundisho kwa mioyo yao (aya ya 16-17). Mafundisho hayo yalikuwa ni Injili, wakaitii na kubatizwa katika mauti ya Kristo na kufufuka kutoka katika kaburi la maji kama jinsi Kristo alivyofufuka kupitia nguvu za Mungu (aya ya 6-11).

Wakati watu wengi wanapoangalia Warumi 5:1 ili kuthibitisha kuwa wokovu ni kupitia Imani tu, wanakataa sura ya 1:5 na sura ya 16:26, mistari yote hii inazungumzia **Utii wa Imani**. Ikiwa imani ya mtu binafsi inamuongoza kutii amri za Kristo (kwa mfano amri iliyopokelewa ***"imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu,"*** Yuda 1:3). Hatimaye anakuwa Mkristo. Hivyo, ubatizo ni kwa waaminio katika Kristo (Wagalatia 3: 26-27).

Zingatia imeoneshwa kwa uwazi kabisa katika kitabu cha (Matendo 2), Injili ndiyo iliyokuwa ikihubiriwa (aya ya 22-36). Na wale walioamini waliuliza ***"tutendeje ndugu zetu"*** (Mstari 37). Waliambiwa ***"Tubuni mkabatizwe"*** kwa mamlaka ya Kristo, ili kupata ondoleo la

dhambi zenu (Mstari 38). Wale waliofanya hivyo (Mstari 41) waliongezwa katika kanisa la Bwana (Mstari 47) ambalo ni mwili wa Kristo (Waefeso 5:23) na kupatanishwa na Mungu (Waefeso 2:16).

Wengine wanapinga dhana ya utii kwa kuamisha mawazo yao katika neema ya Mungu. Bila shaka ni jambo zuri Kwa kwa umakini kuhitajika kuelekezwa katika neema Yake kwa sababu Biblia inafundisha kwamba “kwa neema yake” wokovu ulikuja (Waefeso 2:8-9, Tito 3:7) Hatuwezi kuondoa hilo, bali tunafuraha katika neema ya Mungu! Mungu. Hata hivyo ni dhana ya uwongo ya kufanya mwavuli wa neema ya Mungu kuwa ni jumuishi bila kumwacha mtu ye yote! Biblia inawaondoa wale wanaokataa kusikia na kuuona ukweli (Mathayo 13:15). Wale ambao wanakataa kuamini ukweli (Yohana 3:18,36, Marko 16:16) na wale wasiotii Injili (2 Wathethalonike 1:8-9). Zaidi ya hayo Yesu mwenyewe alifundisha kwamba wale wanaoabudu kutokana na mafundisho ya mwanadamu wanaabudu bure (Mathayo 15:7-9).

Moja ya matatizo makubwa nililonalo na baadhi ya Wakristo ni tabia yao ya kujidai kuwa na elimu kubwa na kukataa mpango wa mafundisho ya Biblia na kujishughulisha na makosa ya madhehebu. Na kusisitiza sana kuhusu nehema ya Mungu na kuonekana kushawishika wenyewe kwamba nehema ya Mungu haimbagui ye yote kutokana na mafundisho ya uwongo. Ingekuwa vizuri kwao kusoma tena katika vifungu vya Maandiko katika kitabu cha Warumi 2:5-11, 16:17; Wagalatia1:8-9; 1 Timotheo 4:1, 2 Timotheo 4:3-4, 1 Yohana 4:1; 2 Yohana 9-11; Ufunuo 2:2, 14-16,20-25.

Ndugu, hili kwa kweli lina umuhimu mkubwa! Kwa kuchunguza kwa umakini, tunaweza kujua ukweli (2 Timotheo 2:15; Yohana 8:32). Hebu sisi tuamini ukweli kwa mioyo yetu yote, na kila siku tuishi katika ukweli na tuhubiri kwa upendo (Waefeso 4:15), fanya kazi maadamu ni mchana (Yohana 4:9) ili kuwafikia waliopotea katika dhambi.

**Maxie B. Boren (1932-2016) alikuwa mhubiri wa Injili na mchungaji katika kusanyiko la Brown Trail huko Bedford, Texas, Marekani.**

# Je, Mkristo Mwaminifu Ataokolewa Kwa Shida?

Dennis Gulledge

Petro aliandika, ***"Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje? Na mwenye haki akiokoka kwa shida, yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi?"*** (1 Petro 4:17-18). Mistari hii huja akilini mwangu pindi Mkristo anapokuwa na shaka juu ya hatma ya wokovu wake. Mawazo ya wengine ni kwamba kama mtu ameokoka itakuwaje shida kuokoka? Hili limeeleweka vibaya kabisa.

Hukumu imetumika hapa kwa mtazamo wa "moto" majaribu ambayo Mkristo ameyapitia (Mstari 12). "Nyumba ya Mungu maana yake Kanisa (1 Timotheo 3:15) ambalo litadhurika katika hili ni majaribu. Kwa Shida ambayo itatokea kwa taabu kubwa. Kifungu hiki hakizungumzii siku ya hukumu, lakini kinazungumzia kipindi cha matatizo ambayo yatawadhuru Wakristo kwa muda mfupi. Hivyo, mtume hakuwa akizungumzia kwamba Mkristo mwaminifu, kama ameokolewa, kwamba ataokolewa kwa shida! Tuondoe shaka hilo katika akili zetu.

Mapema kabisa Petro alisema; ***"Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo."*** (2 Petro 1:11). Maneno haya yaliandikwa muda mfupi tu kabla ya kuanguka kwa Yerusalemu mwaka 70 Baada ya Kristo. Matatizo yalianza mbali na kuenea kote (Mathayo 24:21-22). Katika maelekezo ya Yesu kuondoka katika mji wa Yerusalem, Wakristo waliepuka kifo lakini kilikuwa kipindi cha matatizo makubwa katika Kanisa.

**Dennis Gulledge ni mhubiri wa kanisa la Kristo huko Mabelvale, Arkansas, Marekani.**

# Kwa nini Wengi Hujifunza Bila Kuufikia Ukweli?

**Ardron Hinton**

Ukweli ni kwamba watu wengi wanatumia Biblia sana lakini hawathibitishi wanajifunza nini na wanahitaji kufahamu nini. Baadhi ya ukweli kwenye Biblia hausomwi kwa ufasaha. Kwa mfano Waathene walifahamika kama wasomi wa kipindi kile lakini dini yao kubwa ilikuwa ni upagani. ***"Kwa maana Waathene na wageni waliokaa huko walikuwa hawana nafasi kwa neno lo lote ila kutoa habari na kusikiliza habari za jambo jipya."*** (Matendo 17:21). Walitaka dini yao iwaburudishe. Kama vile walivyokuwa ***"…wakijifunza siku zote, ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli"*** (2 Timotheo 3:7). Haya ni maneno ya Paulo, waliishi maisha ya utauwa. Lakini hawakutafuta ukweli halisi wa Mungu ambao ndio huu. Huu ukweli unapatikana katika Biblia, Neno la Mungu, lakini walichagua kuamini kile kinachowapendeza wao. Katika Hosea 4:6, tunajifunza matokeo ya kutokufahamu tofauti ya ukweli na makosa. ***"Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa."***

Kinyume ni *"**Heri wenye njaa na kiu ya haki; Maana hao watashibishwa**"* (Mathayo 5:6) ***"Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa"*** ( Mathayo 7:7-8) ***"Basi kukawa njaa katika nchi yote ya Misri na Kanaani, na dhiki nyingi, wala baba zetu hawakupata chakula cha kuwatosha"*** (Matendo 7:11). ***"Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake; huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu."*** (1 Petro 5:6-7).

Tumeona mistari hii miwili ni muhimu kufungua fahamu zetu na kuwa tayari kukubali ukweli wa neno la Mungu.

**Ardron Hinton (1929-2015) alikuwa ni mhubiri wa muda-mrefu wa Injili huko Oklahoma, Marekani.**

# KUHUDHURIA KWA UAMINIFU!

**Mark N. Posey**

**Waebrania 10:25**

**UTANGULIZI**

Kuhudhuria kwa uaminifu katika mikusanyiko yote ya ibada huleta ukuaji wa kiroho ambao ni wa thamani usioweza kuelezeka. Tambua faida zifuatazo za uaminifu.

**MWILI**

I. **Ibada ya Mungu hubadilisha.** Mkristo amebadilishwa kuwa *"kiumbe kipya"* (Warumi 12:1-2). Utakaso unaoendelea ni muhimu kwa ukuaji wa kiroho (2 Petro 3:18).

II. **Upendo wa Mungu Unavutia.** Ni *"Upendo wa Kristo"* unaotuvutia kujitahidi kupata *"wema na rehema"* hapa na kukaa katika *"nyumba ya Bwana milele"* (Zaburi 23:6).

III. **Familia ya Mungu inatia moyo.** *"Tunaonyana"* katika kuimba, *"tukichocheana kila mmoja kupenda na matendo mema,"* na *"kujengana"* kwa Neno la Mungu. Twakushukuru Mungu kwa familia yetu ya kanisa .

IV. **Wana wa Mungu wana Njaa.** Raia wa ufalme *"wana njaa na kiu ya haki*" (Mathayo 5:6). Tangu Injili ifunue *"haki ya Mungu"* (Warumi 1:17) tunajua kuwa ni Mungu ambaye tuna kiu na njaa yake.

V. **Adui wa Mungu Ana Zungukazunguka Akiwinda.** Kama simba angurumaye, Shetani anatafuta mawindo yake (1 Petro 5:8). Hivyo, kiasi na bidii yetu ni muhimu katika uwanja mzuri wa kuishi kwa uaminifu kwa ajili ya Bwana.

**HITIMISHO**

Shauku yetu ya kuwa na Mungu na watu wake lazima iwe imara, aminifu na salama.

# Harakati Za Urejeshaji Ni Kitu Gani?

**Jimmy R.Canup**

Baadhi ya watu katika ulimwengu huu hawajawahi kusikia kuhusu harakati za marejesho. Wengine wamesikia, lakini hawaelewi maana na kusudi lake. Bado wengine wamesikia, lakini wameitafsiri vibaya. Ni kusudi letu kuweka maana ya harakati za marejesho, na kufafanua maana yake. Makanisa ya Kristo leo yana uhusiano na harakati za marejesho.

Takribani mwaka 33 Baada ya Kristo, katika mji wa Yerusalemu na katika siku ya Pentekoste, kanisa la Bwana wetu lilianza. Hili lilitokea baada ya mahubiri ya mitume walipokuwa wakitoa Injili kwa mara ya kwanza. Yote haya yameandikwa katika Matendo 2. Tangu kuanzishwa kwake, kielelezo cha kanisa la Bwana kimefunuliwa katika Agano Jipya. Kila sehemu ya kanisa imewekwa wazi. Kipindi, mahali na tukio, yote yamewekwa wazi. Kazi ya kanisa imewekwa wazi. Namna Mungu anavyotarajia sisi tumwabudu imewekwa wazi. Mungu ametupa mwongozo wa mpangilio kwa ajili ya kanisa. Katika Waebrania 8:5, Musa alielekezwa kujenga Hema kulingana na vielelezo alivyopewa katika mlima Sinai. Kanuni hiyo hiyo ya kufuata kielelezo kinashikilia kweli kwa kanisa la Biblia.

Yesu na mitume wake walionya kuwa watu wataiacha kweli. Kuacha huku kulianza katika siku za mitume. Katika karne ya pili, idadi ya walioacha ilianza kiasi kwamba wachache walibaki katika kanisa halali. Kutokana na hali hii, ukaanza Ukatoliki. Katika mwaka 606 Baada ya Kristo, Boniface III alipewa cheo cha Papa wa ulimwengu wote. Hili lilitupeleka katika kipindi kilichojulikana kama Kipindi cha Giza. Katika kipindi hiki, Ukatoliki ulitawala akili za watu na Biblia zilifungiwa mimbarini.

Katika miaka ya 1500, watu kama Martin Luther, John Huss na wengine walianza harakati ili kujaribu kugeuza hali ya kidini iliyokuwepo. Hili linajulikana kama Harakati za marejesho. Mbali na harakati hizi, kulihusisha idadi kubwa ya taasisi zilizoanzishwa na wanadamu zilizojulikana kama madhehebu ya Kiprotestanti. Walikuwa "Waprotestanti" kwa sababu walikuwa "wanaandamana" kupinga Ukatoliki. Yalikuwa ni "madhehebu" kwa sababu waligawanyika kwa mafundisho na matendo ya kila mmoja.

Katika miaka ya 1800, harakati nyingine zilianza. Zilijulikana kama Harakati za Kmarejesho. Watu kama Thomas na Alexander Campbel, Barton W. Stone, John Smith pamoja na wengine wengi walitoa ombi katika ulimwengu wa kidini kwa watu kwenda zaidi ya mafundisho, imani na mashirika ya wanadamu, na kurejeza kielelezo cha kanisa linalopatikana katika Agano Jipya. Mbali na harakati hizi, ukaja msemo wa kibiblia uliotolewa na Alexander Campbel. Msemo ulikuwa, "kusema pale Biblia inaposema na kunyamaza pale Biblia inaponyamaza." Msingi wa hili unapatikana katika 1 Petro 4:11 ***"Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu."*** Ombi lingine au msemo mwingine uliowekwa ulikuwa, "Kuviita vitu vya Biblia kwa majina ya Biblia na kufanya vitu vya Biblia katika njia za Kibiblia."

Ombi na harakati hizi ni halali hata leo kama ilivyokuwa wakati yamesemwa kwa mara ya kwanza. Maombi haya bado yanatolewa leo na makanisa ya Kristo. Alexander Campbel pamoja na watu wa kipindi chake hawakuona kanisa jipya. Waliwaita watu kurudi katika Agano Jipya katika mambo yote yanayohusu hali yetu ya milele. Hawakuwa watu wasio na makosa, walikosea, lakini hakuna mtu anayekosea anapofuata Agano Jipya pekee.

Hebu fikiria mchezo wa mpira ungeachwa kuchezwa duniani kwa miaka elfu moja. Miaka elfu moja baadaye baadhi wakapata kitabu cha mwongozo wa mpira, kikionesha almasi na tena kulingana na kitabu kile kile cha sheria wakaanza kucheza mchezo ule wa mpira. Watu

wote wenye busara wangekubali kwamba hawakuanza kucheza mchezo mpya, bali wameurejesha mchezo ule wa mpira.

Hili ni sawa na kanuni za leo katika makanisa ya Kristo. Hatujaribu kuwa kanisa jipya. Wala hatudai kuwa sisi ni madhehebu. Kwa upole na unyenyekevu tunawaomba wanaume na wanawake kuungana nasi kwa moyo na kuliendea Agano Jipya ambalo ni mwongozo wetu mmoja na mkamilifu kutufikisha mbinguni baada ya maisha haya kuisha. Je, utakubali ombi na changamoto yetu?

Katika Warumi 16:16, Paulo alisema, ***"….makanisa ya Kristo yawasalimu."*** Tafadhali leo chunguza ni nini makanisa ya Kristo yanachofundisha na kufanya. Muda mrefu uliopita, nabii Yeremia aliliita taifa la Israeli ili kuwarejeza kwa kusema, ***"Simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani. I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema, hatutaki kwenda katika njia hiyo."*** Usiruhusu kukataliwa huko kwa njia za Mungu kuwa mtazamo wako pia! Hatima yako ya milele inahusika. Usiruhusu nafasi yo yote upoteze nafsi yako.

## Sarafu za Kenny

***"Basi ndugu zangu, nawaarifu ile injili niliyowahubiri, ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama. Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko: na ya kuwa alizikwa, na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko."*** (1 Wakorintho 15:1,3-4).

Uhai, maziko na ufufuo hayakuandikwa tu katika injili, bali yalitabiriwa katika Agano la Kale. Wale wanaofundisha kwamba kwa Wayahudi kumkataa Masihi hakukupangwa akilini mwa Mungu yalikuwa si sahihi kabisa. Maandiko hayo hayo yanayotabiri kuja kwa Masihi, Ufalme wake na utawala wa milele unaozungumzia kukataliwa kwa Masihi pia. Mpango huu ilikuwepo kabla ya msingi wa dunia!

# JICHUNGUZE MWENYEWE KAMA UPO KATIKA IMANI NDANI YA KANISA

Ernest S. Underwood

Maandiko Matakatifu yanafundisha kwa uwazi kwamba kuna kanisa moja, na kanisa moja tu, haliwezi kukataliwa kabisa. Paulo, katika Waefeso 4:4 aliandika, ***"Mwili mmoja, na Roho mmoja kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu."*** Katika waraka huu huu aliandika, ***"akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa ambalo ndilo mwili wake anayekamilika kwa vyote katika vyote"*** (Waefeso 1:22-23). Kwa kusoma maandiko ya historia ya mwanahistoria ye yote wa kawaida wa kanisa, mtu anaweza kufuata bahati ya kanisa hili moja. Mara baada ya kuisha karne ya kwanza, ukengeufu ulianza, kufikia miaka mitano baadae katika shirika lenye mtu mmoja anayedai kuwa mkuu wa kanisa. Karne nyingi baadae, watu wakaibuka na wazo la kurejeza hilo shirika lililokengeuka. Vitendo hivi vilisababisha harakati za urejeshaji. Mimba na kuzaliwa katika harakati ilikuwa dhana ya madhehebu.

Katika taifa letu leo, kuna mashirika ya kimadhehebu au makanisa zaidi ya mia nne. Kwa kuwa mafundisho ya mtume aliyevuviwa ni ***"Jichunguze mwenyewe kama upo katika Imani,"*** inaonekana kila mmoja anapaswa ajiulize mwenywe kuhusu kanisa ambalo yeye ni mshirika wake. Kwa maneno mengine, ninaweza kuthibitisha kwa Maandiko kwamba kanisa ambalo nimo ndani yake ni Mwili mmoja uliosemwa na Paulo? Kanisa ambalo mimi ni mshirika wake ni lile ambalo Yesu alisema angelijenga na lile ambalo alilinunua kwa damu yake (Matendo 20:28)? Mhubiri wako atakuwa tayari kusema "Kanisa ambalo nashiriki ni kanisa moja la Agano Jipya, na ninaweza kulithibitisha kwa Maandiko? Kama mshirika wa kanisa hilo una haki ya

kumwuliza swali hilo? Kama ni hapana, kwa nini? Agano Jipya linalielezea kanisa kama mtindo ambao mtu anaweza kuyachukua Maandiko na kutambua Mwili huo mmoja.

Hebu tuangalie kanisa la Agano Jipya. Katika Agano Jipya, neno ***"kanisa"*** halirejelei jengo lo lote la kimwili, lakini linatambua wale walioitwa kutoka dhambini kwa utii wao wa Injili. Hivyo, kanisa lina wale waliookolewa (Matendo 2:47; Wakolosai 1:13-14).

Yesu alisema, ***"Juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu"*** (Mathayo 16:18). Kila mwanafunzi wa lugha atagundua kwamba kirai ***"nitalijenga"*** cha sentensi ile ni wakati ujao. Katika Matendo 2:47, tunawaona waliookolewa wakiongezwa katika kanisa. Muda fulani kati ya kauli ya Yesu na matukio katika Matendo 2 kanisa lilianza. Katika Marko 9:1, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa ufalme utakuja kwa nguvu. Katika Mtendo 1, Yesu anaeleza nguvu hiyo ni Roho Mtakatifu akiwajia mitume. Hili limeandikwa katika Matendo 2. Siku hiyo, wale waliotii amri za Roho Mtakatifu, kama zilivyosemwa na Petro, waliongezwa katika kanisa.

Je, hili ni kanisa ambalo wewe ni mshirika wake? Je, unaweza kulithibitisha katika Maandiko? Je, Mungu anakubali namna ambavyo unatumia Neno lake kulithibitisha? Kwa maneno mengine, mtu anahitaji kuuliza, je, ninapotosha Maandiko, au ninayatumia katika mazingira yake kuthibitisha kwa Maandiko kuwa kanisa ambalo mimi ni mshirika ni lile kanisa moja?"

**Ernest S. Underwood ni mhubiri na mmishonari huko India.anaishi Daraville, Georgia, Marekani.**

# Je, Wajua?

Kipindi cha Agano la Kale, mapango yalitumika kama mahali pa makaburi (Mwanzo 23:9) na wakati mwingine kama makazi (Mwanzo 19:30) na kama sehemu za kujificha (Yoshua 10:16)?

## Historia ya Kanisa

# Njiani Kuelekea Derbe

## Majaaliwa ya Mungu katika Kazi katika Nyakati Zote

**Dokezo la Mhariri:** Ifuatayo ni hadithi ya kihistoria, kuondoka kutoka katika muundo fulani uliozoeleka, kwa kusudi la kutoa hoja kuheshimu majaliwa ya Mungu kuhusiana na uhifadhi wa Neno la Mungu – Biblia.

***"Lakini Paulo akamchagua Sila akaondoka akiombewa na wale ndugu apewe neema ya Bwana. Akapita katika Shamu na Kilikia akiyathibitisha makanisa. Basi akafika Derbe na Listra, na hapo palikuwa na mwanafunzi mmoja jina lake Timotheo…"*** (Matendo 15:40-41; 16:1).

Paulo na Sila walikuwa wakitembea katika barabara ya Rumi kati ya Listra na Derbe. Kulikuwa na joto na njia ilionekana kuwa ndefu. Paulo alionekana mwenye mawazo. "kama ilivyo vigumu kusafiri katika joto, ingekuwa ni vigumu zaidi kama Warumi wasingejenga hizi barabara, kuunganisha falme pamoja."

"Ni baraka kiasi gani kwamba Wayunani walieneza lugha yao kila mahali, na sasa wanacho Kiyunani kama moja ya lugha zao. Hiyo ni zana kubwa katika kazi!" Sila alisema.

"Fikiria tu ni karne ngapi zimepita, Mungu hata katika uthibitisho wake, aliandaa njia kwa ajili yetu kufanya kazi aliyoiamuru Yesu, ***"Enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe!"*** Paulo alishangaa.

"Njia nzuri na lugha ya kawaida vilifanya iwe rahisi kusambaza nakala ya barua zenu kwa makanisa yaliyoenea kila mahali, na nyaraka

za baadhi ya mitume na ndugu Luka kuandika maisha ya Yesu," Sila aliongeza.

"Lakini bado, ni changamoto kubwa kumfikia kila mtu, ndiyo maana hii kazi si yetu tu pamoja na mitume, ni ya kila Mkristo kuwaambia habari njema kila mtu wanayemjua. Ni jambo zuri kiasi gani, kwamba Yesu alikufa kwa ajili yetu na kila mmoja wetu ana msamaha wa dhambi ikiwa tutamwamini na kumtii!"

Sasa, fikiria kidogo Paulo na Sila wangekuwa katika kipindi chetu cha sasa. "Ah, msongamano wa magari!" Sila alicheka, aliporukia pembeni gari la ajabu likiwapita. "Kilikuwa ni kitu gani?"

"Sijui!" Paulo alisema, akiangalia kwa mshangao. "Kila kitu kimebadilika! Angalia mji mkubwa uliopo mbele yetu! Na kile kinachozunguka ni mawingu?"

"Na tukimbilie Derbe na kutafuta kinachoendelea! Sila aliita alipoanza kukimbia. Kuwa makini kukaa katika benki ya nyasi kando ya barabara yenye wasafiri sana, mara walifikia maduka ya kwanza nje kidogo ya mji.

"Angalia! Hili linaonekana ni 'duka la vitabu'" Paulo alisema. "Tuingie tukaangalie ni kitu gani kinaendelea!" Muuza duka alikutana nao mlangoni. "Niwasaidie nini?" Aliuliza.

Paulo alipokuwa anataka kujibu, Sila, aliyekuwa mbele yake alishangaa, "Hiki ni kitu gani? Alisema, "Biblia Takatifu'!" "Oh, hiyo ni Biblia," muuza duka alijibu. "Biblia?" aliuliza Sila, akichukua mojawapo ya vitabu." Paulo! Paulo!" alisema kwa sauti, akimpa Paulo kitabu. "Angalia!" hii hapa barua yako kwa kanisa la Efeso! Na Kolosai! Oh! Paulo, hapa kwa jina "Matendo ya Mitume" ni hadithi ya kuokolewa kwako njiani kwenda Dameski!"

Paulo alinyakuwa kitabu, kwa heshima, akakifungua katika kurasa za kwanza. "***Mwanzo! 'Hapo mwanzo Mungu aliziumba...'*** Na, Sila! Sila! Angalia: Mathayo, Marko, Luka na Yohana! Nyaraka za kuzaliwa

kwa Bwana wetu na mafundisho yake, kufa na kufufuka kwake! Sila! **Yote yako hapa kwenye kitabu kimoja!"**

Muuza duka aliangalia kwa mshangao. "Ndiyo," alikubali, "hiyo ni Biblia yote, kuanzia Mwanzo hadi Ufunuo. Pia ninazo zinapatikana katika lugha nyingine, kama hamtaridhika na Kiyunani. Imetafsiriwa na kuchapwa katika lugha karibia zote za duniani."

Ghafla, sauti inasikika kutoka nyuma, "Ni nini hicho?" aliuliza Sila. "Ah, ni kipindi cha Runinga huwa nakiangalia kila siku," alijibu muuza duka. "Mtu ambaye jina lake ni Paulo, kama lako, akihubiri kutoka kwenye Biblia. Yuko makini sana kufundisha ukweli hasa kama ulivyoandikwa kwenye Biblia. Ni muhubiri katika kanisa hapa Derbe."

"Je, yupo katika hilo sanduku dogo?" Paulo aliuliza?

"Ah, hapana! Muuza duka alicheka. "Hamjui kuhusu Runinga? Masomo yake yameandikwa, tena katika Runinga watu wa nchi wanaweza kuwaona. Pia kuna vipindi ambavyo vinaonekana katika nchi nyingine." "Ooh," Paulo alitamka kwa mshangao mkubwa. "Tunazo njia nyingi za kufundisha sasa hivi," muuza duka alifafanua. "Njoo hapa nitakuonesha." Akaonesha kisanduku kidogo. Ikiwa hujui, hiyo ni redio." Aliiwasha, ikaanza kuongea. "Mimi ni sehemu ya kanisa la Kristo," muuza duka alifafanua. "Tunavyo vipindi vya redio ambavyo vinaweza kusikika duniani kote." "Lakini ni kwa namna gani watu husikia na kuyaona mambo haya?" Paulo aliuliza. "Oh, watu wengi wana redio na Runinga pia. Unajua jinsi ilivyo; wakati vitu vipya vinapokuja, hata walio mafukara watapambana ili wavipate!"

Muuza duka alionekana mwenye mawazo. "Ni hakika utakuwa nyuma ya wakati!" alicheka. "Unajua kuhusu kompyuta na mtandao?" "Hapana" Paulo alijibu pamoja na kuuliza kwa sauti, "Ni nani hao?" "Hiki ni kipindi cha mawasiliano ya duniani kote!" muuza duka akaanza kufafanua. "Kanisa hapa linaandika ibada ya mkusanyiko katika kompyuta, halafu wataiweka mtandaoni, na ye yote atakayeenda mtandaoni ataweza kuona na kusikia ibada yote! Pia tunaweka makala

nyingi mtandaoni pamoja na masomo ya Biblia. Kama mtu atataka kujifunza Biblia atajiandikisha, halafu ndugu na dada katika kusanyiko watamsaidia masomo. Kwa njia hiyo, watu, hata katika nchi ambazo Ukristo hauruhusiwi, wanaweza kufanyika Wakristo! Ni njia nzuri ya "kwenda ulimwenguni kote" kama vile Yesu alivyotuaambia tufanye."

"Na wewe ni Mkristo?" Sila aliuliza.

**"Ndiyo," muuza duka alijibu.** "Kuna makanisa katika miji na katika nchi nyingi. Hata hivyo, ni jambo baya, kwamba wengi wanaomwamini Kristo wamefundisha mafundisho mengine na kuanzisha makanisa yao wenyewe, hivyo kuna mgawanyiko mkubwa kati ya watu ambao wanadai na wanajiita kuwa ni Wakristo."

"Roho Mtakatifu pia alionya pia hata katika miaka michache ya kwanza baada ya kanisa kuanza kwamba baadhi watafanya hivyo," Sila akasema "inahuzunisha, kwa sababu watu watachanganyikiwa, na hiyo ni njia ya Shetani ya kuwapofusha katika kweli ambayo kupitia hiyo Yesu alikufa."

**"Lakini, Sila aliangalia kile ambacho Mungu alikifanya ili kila mtu aijue Injili!** Hakuna atakayetembea mji hadi mji sasa au kupanda punda! Angalia jinsi watakavyosafiri haraka! Na kitabu chote cha Mungu, kuna mikono ya watu ili waweze kujifunza wakati wo wote na njia zote hizi za kuhubiri na kufundisha kila mmoja ulimwenguni, Sila! Mungu ametoa zana ili kwamba kila mtu ajue kwamba wanaweza kuokolewa kupitia Yesu! Je, unajua hii ina maana gani?

**"Huyo Yesu aliahidi kuwa pamoja nasi siku zote, bado ni kweli,"** Sila akajibu kwa tabasamu la ushindi. **"Hajawahi kuwaacha watu wake peke yao."**

**Betty Burton Choate ni mjane wa J.C. Choate, mhariri mwanzilishi wa jarida la Sauti ya Kweli Kimataifa, anaishi Winonna, Mississoppi, Marekani.**